ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni

20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe.Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake

48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Thalathini na Tatu – Tarehe 30 Julai, 2011

(Kikao Kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika *(Pandu Ameir Kificho)* alisoma dua

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar

(*Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, awali ya yote nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema muumba mbingu na ardhi na vilivyomo, kwa kutujaalia kumaliza kupokea kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara zote za Serikali, kazi iliyotuchukua takriban siku 40 chini ya uongozi wako.

Mhe. Spika, uwasilishwaji na mijadala ilikuwa ya aina yake na jamii nzima ya Zanzibar iliwasisimua waliifurahia sana na wanaipongeza, tuna haki wajumbe wako wa Baraza lako tukufu haki ya msingi ya kujipongeza, kazi yetu hii ilisisimua kila Mzanzibari na kila Mtanzania na wengine walijiuliza sheria na kanuni za Zanzibar zimebadilishwa. Lakini hazikubadilishwa ni utaratibu mpya tuliojiwekea na bila ya shaka watu walipenda waone mabadiliko ni mabadiliko hayo ambayo leo atunapongezwa na kufurahiwa nchi nzima.

Mhe. Spika, nataka nikupongeze wewe mwenyewe binafsi kwa namna ulivyoendesha kikao hiki ukisaidiwa na Naibu Spika, na wenyeviti wako wawili, vile vile kwa kupitia kwako nataka niwapongeze Mawaziri wenzangu wote na Manaibu wao na watendaji wao wakuu katika Wizara, Maidara na Mashirika kwa kazi nzuri hii waliyoifanya kwa pamoja.

Mhe. Spika, baada ya kazi hiyo kubwa ngumu lakini nzuri tena nzuri sana kwa kawaida yetu tunachotegemea ni kumsikia Makamo wa pili wa Rais akitoa hotuba ya kufunga baraza hili na kutoa hoja kwamba baraza hili liahirishwe, lakini Mhe. Spika, utaratibu wa mara hii umebadilika. Mara hii haikuwa hivyo wajumbe wako wote hivi sasa wako tayari kuendelea kujadili miswada miwili ya Sheria hadi hapo miswada hii miwili itakapojadiliwa na kupitishwa na Baraza lako ndipo wajumbe wako watakuwa wamemaliza ngwe ya mkutano huu wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, moyo huu unaonyeshwa na wajumbe wako ni wa kupigiwa mfano wajumbe wako wameona endapo miswada hii itaahirishwa hadi kikao kijacho ni sawa na kuwacheleshea Wazanzibari maendeleo yao, kwa niaba yangu na watendaji wa Wizara yangu nataka kwanza nikushukuru wewe mwenyewe kwa kukubali na kuruhusu hatua hii kufanyika, kwani usingekubali hili lisingefanyika. Lakini pia wajumbe wako watukufu kukubali kuendelea na kazi hii kwa moyo wa kizalengo na

kulenga kuhakikisha maendeleo ya wa Zanzibar ambao wana kiu ya maendeleo endelevu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, viwanja vya ndege hapo zamani vilikuwa vikiendeshwa kama Idara ya serikali na hali hiyo kuufanya utendeshaji na ufanisi wake kuwa wa tabu na mashaka, aidha katika hali hiyo imewafanya watumiaji wa huduma zinazotolewa kwenye viwanja hivyo kutoridhika na huduma hizo, lakini zaidi kutokana na viwango duni vilivyokuwa vinatolewa. Hali kadhalika wadau wa sekta hii ndogo ya usafiri wamekuwa wakilalamikia mfumo mzima wa uendeshaji wa viwanja vya ndee pamoja na huduma zinazotolewa na Idara hii ya serikali, kwa kuwa haiendi na wakati na kwamba haikidhi mahitaji na matakwa ya wadau wa sekta hii.

Wengi wa wadau wamekuwa wakilalamikia idara kushindwa kutekeleza wajibu wake ilihali mapato ya kutosha yanaendelea kuwa katika maeneo hayo, aidha wao wenyewe wakiwa kama wadau na wateja wanazilipia sawa sawa huduma wanazopewa na Idara hii.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine wafanyakazi wa idara wamekuwa wakilalamikia idara kushindwa kuwapatia vitendea kazi muhimu pamoja na stahili zao, hali hii kwa ujumla yake ndio iliyosababisha mfumo wa uendeshaji wa viwanja vya ndege Zanzibar kuangaliwa upya, aidha haja ya kuwa na mifumo ya uendeshaji kwa viwanja vya ndege unaolingana na hadhi ya Afrika ya Mashariki na ulimwenguni kote unachangia katika kufikia uamuzi huu wa leo kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha Mswada wa kuundwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na mambo yanayohusiana nayo.

Mswada huu wa sheria chimbuko lake ni sera ya usafiri ya Zanzibar na mpango mkuu wa usafiri Zanzibar unaokusudia kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, jumuiya ya kimataifa ya usafiri wa anga duniani *(IKAO)* na Jumuiya ya Viwanja vya Ndege vya Kimataifa *(ACI)* zimekuwa zikisisitiza kubadili mifumo ya uendeshaji wa viwanja vya ndege kutoka katika Idara za Serikali na kuwa Mamlaka zinazojitegemea ili kuvifanya viwanja hivyo kuwa na ufanisi na kupata maendeleo endelevu ya haraka.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inaomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar katika baraza lako tukufu, ili wajumbe wako waweze kuujadili na kutoa mapendekezo yao ambayo wataliwezesha Baraza lako tukufu kutunga sheria hii ambayo itasimamia maendeleo ya usafiri wa anga Zanzibar, pamoja na uendeshaji wa viwanja vya Ndege vya Unguja na Pemba.

Kwa ujumla Mhe. Spika, Mswada huu wa Sheria umegawika katika sehemu kuu nne na ina jumla ya vifungu 34.

Sehemu ya Kwanza ya. (Utangulizi)

Utangulizi wa sheria inaeleza masharti ya kiutangulizi yanayohusiana na jina la Mswada wa Sheria kuanza kutumika kwa Sheria hii, matumizi yake na ufafanuzi wa maneno na misemo yenye maana maalum katika sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya pili. (Utawala na Kazi za Mamlaka)

Uanzishwaji, Utawala na Kazi za Mamlaka, sehemu ya pili yenye vifungu 16 inazungumzia masuala ya uanzishwaji wa Mamlaka, Utawala Mamlaka, pamoja na kazi zake. Mswada unaelekeza wajibu wa mamlaka ya kuendesha na kusimamia maendeleo ya Viwanja vya Ndege vya Unguja na Pemba kwa viwango vya Kitaifa na Kimataifa. Uendeshaji wa Mamlaka utakuwa chini Mkurugenzi Mkuu atakayeteuliwa na Mhe. Rais kwa madhumuni ya kuleta ufanisi na usimamizi wa kazi za mamlaka kutakuwa na bodi ya wakurugenzi itakayokuwa na wajumbe wasiozidi watano watakaoteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya viwanja vya ndege. Mwenyekiti wa bodi hiyo atateuliwa na Mhe. Rais uwezo wa waziri mwenye dhamana na kazi hii Bodi ya Wakurugenzi na Mkurugenzi Mkuu pia nao umeelezwa katika sehemu hii.

Sehemu hii pia imeweka masharti yanayofafanua uwezo wa Mamlaka katika utekelezaji wa Majukumu yake pamoja na kuandaa taratibu mbali mbali katika viwanja vya ndege na kuvisimamia. Mamlaka itakuwa na uwezo wa kumiliki eneo kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa Viwanja vya ndege viliopo au kuanzisha vyengine.

Kadhalika sheria hii itawapa uwezo Maafisa mbali mbali wa Mamlaka katika kusimamia shughuli za kila siku viwanjani hususani masuala ya uimarishiaji ulinzi na usalama.

Sehemu ya Tatu. (Masuala ya Fedha)

Sehemu ya ta tatu ya Mswada huu ni masuala ya fedha. Mhe. Spika, sehemu hii ya Mswada huu wa sheria yenye vifungu vitano inazungumzia masuala ya fedha za Mamlaka vianzio vya mapato vya Mamlaka na namna vitakavyopatikana na kusimamiwa, pamoja na uwezo wa mamlaka wa kukopa kutoka Taasisi nyengine. Masuala ya bajeti ya mapato na Matumizi ya Kila mwaka ya Mamlaka, utunzaji wa mahisabu na ukaguzi wake, taarifa za utekelezaji za kila mwaka pamoja na uwekezaji mtaji pia nayo yameelezwa katika sehemu hii.

Sehemu ya Nne. (Mambo Mengineyo)

Mhe. Spika, sehemu hii ya nne na ya mwisho ya Mswada huu wa Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ina vifungu 11 na inazungumzia mambo mengineyo yanayohusiana na Mamlaka hiyo kwa ujumla wake ambayo ni haya yafuatayo.

1. Makosa na adhabu
2. Masuala ya wafanyakazi wa Idara ya Anga watakaohamishiwa kwenye Mamlaka
3. Kodo *conduct*
4. Uendelezaji wa adhabu zilizotolewa kwa wafanyakazi wa Idara
5. Masuala ya Kinga dhidi ya Wafanyakazi
6. Uhamishaji wa Mali za Idara

7. Uwezo wa Mhe. Waziri Kutengeneza Kanuni kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa Masharti na Madhumuni ya Sheria hii.

Mhe. Spika, sheria hii ina makusudi ya kuunda mamlaka ambayo itakuwa na uwezo wa kisheria kusimamia uendeshaji wa shughuli za viwanja vya ndege kwa ufanisi mkubwa na kutoa ushindani wa kibiashara kwa viwanja vya jirani kwa vile maumbile ya shughuli za viwanja ni biashara.

Mhe. Spika, kupitishwa sheria hii inayopendekezwa kutasaidia mno kuifanya viwanja vya ndege kufikia hadhi inayopaswa kuwa navyo, kiuendeshaji, kiufundi na kiusalama. Kiwanja cha ndege cha Kimataifa ya Abeid Amani Karume ni kiwanja cha kimataifa kama kinavyotambulikana ulimwenguni kote, hadhi hii mara nyingi imekuwa ikitiliwa mashaka na wananchi walio wengi kwa vile ziko baadhi ya huduma huwa hazipatikani katika kiwanja hiki ambazo hupatikana katika viwanja vyengine vya kimataifa vinavyofahamika na wengi.

Mhe. Spika, ni tegemeo letu kwamba patakuwepo na mamlaka ya viwanja vya ndege huduma zile chache ambazo sasa hivi zinakosekana ziataweza kuwekwa na hivyo kuziba pengo ambalo ndilo linalowakera wananchi na wasafiri wanaotumia viwanja vyetu. Kwa upande mwengine tunategemea mapato ya viwanja vya ndege na ubora wa huduma zake pia zitaongezeka kwa kasi na kiwango kikubwa sana.

Mhe. Spika, ni matumaini yangu kwamba Wajumbe wa Baraza lako tukufu wataujadili mswada huu wa sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar na kutoa ushauri wao ipasavyo na hatimae kupitisha kwa kauli moja, Mswada huu kuwa Sheria iliyotungwa na Baraza hili la kutunga sheria.

Mhe. Spika, leo ni mwezi 28 Shaban tuna siku moja au mbili kuingia katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, sheria hii inakuja wakati mzuri sana Mhe. Spika, kwa niaba yangu mwenyewe na Wizara yangu naomba niwatakie funga safi itakayotakabaliwa na Mwenyezi Mungu, funga ambayo *Inshaallah* kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu itakuwa ndio ndege ya kuingia katika pepo za Firdaus wewe mwenyewe, wajumbe wako na wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Nami kwa niaba ya wajumbe naitikia Amin, pamoja na waislam wengine wote. *(Makofi)*

Mhe, Rashid Seif Suleiman (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi naomba ruhusa yako kusoma hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kuhusu mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zaznibar na mambo menine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kabla sijaanza hotuba hii naomba nitoe tanbihi kamba jana ilitolewa karatasi yenye kurasa tano ambazo kuna marekebisho ya vifungu kwa vifungu kwa hivyo naomba wajumbe waizingatie karatasi hiyo kwani hotuba yetu haitokuwa na *ditel* ya karatasi hiyo.

Mhe.Spika, naomba nimshukuru Mwenyezimungu kwa kutujaalia uzima na afya njema iliyotuwezesha kukutana na kujadili mswada huu muhimu wa kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar.

Baada ya kumshukuru Mwenyezimungu, nitangulie kusema kuwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inaunga mkono uamuzi wa serikali wa kuleta mswada huu mbele ya Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kuwa na taasisi yenye hadhi zaidi na itakayofanya kazi kwa ufanisi zaidi kuliko ilivyo sasa ambapo taasisi inayoshughulika na viwanja vya ndege inafanya kazi ikiwa ni idara miongoni mwa idara za wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe.Spika, kutokana na kukua kwa sekta ya utalii na sekta ya usafiri kwa ujumla, ni dhahiri kuwa kuna haja kubwa ya kuharakisha kuimarisha sekta ya usafiri Zanzibar, hasa milango ya kuingilia watalii hao ambayo ni bandari na viwanja vya ndege. Ingawa jitihada zimekuwa zikifanywa katika kuimarisha viwanja vyetu vya ndege, bado tuna kazi kubwa mbele yetu ya kuhakikisha tunakwenda sambamba na kasi ya ongezeko la watalii na watumiaji wengine wa usafiri wa anga, lakini pia haja ya kuwa na huduma zinazohitajika katika kiwango cha kimataifa.

Mhe.Spika, kwa mujibu wa Mswada huu, Mamlaka imepewa uhuru katika mambo ya uendeshaji wa taasisi hiyo na pia uhuru katika masuala ya vyanzo na usimamizi wa fedha za Mamlaka. Uhuru huo ni muhimu sana katika kuendesha taasisi hiyo kitaalamu na kwa ufanisi zaidi. Ni imani ya Kamati yetu kuwa uwezo itakaopewa Mamlaka ya Viwanja vya ndege baada ya kupitishwa kwa mswada huu, utatumika kama inavyotarajiwa ili kujenga taasisi yenye hadhi itakayosaidia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi Zanzibar.

Mhe. Spika, kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano na Ujenzi ilipitia Mswada wa Sheria wa kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo. Naomba niwatambue wajumbe wa Kamati hao walioshiriki kwa ukamilifu katika kahi hiyo.

1.	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Rashid Seif Suleiman	-	M/ Mwekiti
3.	Mhe. Subeit Khamis Faki	-	Mjumbe
4.	Mhe. Salum Amour Mtondoo	-	Mjumbe
5.	Mhe. Shawana Bukheti Hassan	-	Mjumbe
6.	Mhe. Hassan Hamad Omar	-	Mjumbe
7.	Mhe. Salma Mussa Bilali	-	Mjumbe
8.	Ndg. Mussa Kombo Bakari	-	Katibu
9.	Ndg. Aziza Wazir Kheir	-	Katibu

Mhe.Spika, sasa naomba uniruhusu nieleze mbali ya marekebisho madogo madogo, baadhi ya mapendekezo ya marekebisho ya msingi ya mswada huu yaliyofanywa na Kamati yetu baada ya kuupitia mswada huu kama ulivyotuelekeza.

Mhe.Spika, Kamati yetu katika kifungu cha sita cha mswada huu kinachohusiana na wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka imependekeza mambo kadhaa kama ifuatavyo:-

a) Kumuondoa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na masuala ya fedha na badala yake kuweka Mjumbe mmoja kutoka wizara hiyo. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Katibu Mkuu anakuwa na kazi nyingi sana, jambo ambalo linaweza kuathiri ufanisi wa vikao vya bodi endapo mara kwa mara Katibu Mkuu huyo atashindwa kuhudhuria vikao hivyo.

b) Kamati pia inapendekeza kuondolewa kwa Katibu Mkuu au mwakilishi wake kutoka wizara yenye dhamana na mambo ya viwanja vya ndege kwa kuzingatia kuwa kuwepo kwao kunaweza kuathiri maamuzi ya Bodi ya Wakurugenzi. Kamati inadhani kuwa ni vyema maamuzi ya bodi katika mambo kadhaa, kabla ya kufikishwa ngazi ya wizara kwa ajili ya kuidhinishwa na waziri mwenye dhamana na mambo ya viwanja vya ndege, yawe huru bila ya ushawishi wa namna yoyote wa wizara hiyo.

c) Aidha Kamati inapendekeza kuwemo katika bodi ya Wakurugenzi, mjumbe mmoja kutoka wizara yenye dhamana na mambo ya utalii. Hii ni kutokana na uhusiano wa karibu uliopo baina ya uimarishaji wa sekta ya utalii na haja ya kuimarisha sekta ya usafiri wa anga ambapo viwanja vya ndege vinatumika kama mlango wa kuingilia watalii nchini. Mjumbe huyo tunaamini ataisaidia Bodi katika kuimarisha viwanja vyetu vya ndege ili kukidhi haja iliyopo hasa kuhusiana na watalii wanaoingia nchini.

d) Kutokana na umuhimu wa kuishirikisha na kuthamini mchango muhimu wa sekta binafsi, Kamati inapendekeza kuwemo katika Bodi ya Wakurugenzi, miongoni mwa wajumbe wawili wanaoteuliwa na Waziri chini ya Kifungu cha 6(1)(f), mjumbe mmoja kutoka sekta binafsi.

Mhe.Spika, Kamati yetu pia inapendekeza kurekebishwa kifungu cha 9 cha mswada kwa kuweka kwa uwazi zaidi, sifa za Katibu wa Bodi ambazo hazikuwa zimeainishwa vizuri. Hivyo Kamati inapendekeza Katibu wa Bodi awe angalau na shahada ya kwanza katika fani ya sheria na pia uzoefu katika fani hiyo wa angalau miaka mitatu.

Mhe.Spika, aidha Kamati inadhani kuwa adhabu iliyowekwa chini ya kifungu cha 26 cha mswada huu kwa makosa ambayo hayakutajwa wazi wazi ama ndani ya sheria hii au Kanuni zitakazotungwa, ni kubwa na hivyo tunapendekeza ipunguzwe. Hivyo Kamati inapendekeza adhabu hiyo iwe ni faini isiyozidi shilingi laki tano badala ya faini isiyozidi shilingi milioni mbili na laki tano au kifungo kisichozidi miezi mitatu badala ya kifungo kisichozidi miezi sita.

Mhe. Spika, mwisho tunaiomba Mamlaka itakayoanzishwa pamoja na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambayo ndiyo itakayokuwa na dhamana na Mamlaka hiyo, kuijenga taasisi ya kitaalam yenye wafanyakazi wenye ujuzi, uadilifu na uwezo mkubwa wa kuisaidia taasisi hiyo ili iweze kujiendesha kwa ufanisi badala ya kuwa na wafanyakazi wengi wasio na tija kwa taasisi.

Mhe.Spika, baada ya kueleza hayo, tunawaomba Wajumbe wenzetu wauchangie mswada huu kwa kutoa mawazo yatakayosaidia katika kuufanya uwe bora zaidi na hatimaye kuupitisha.

Mhe.Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kwanza nami niweze kutoa maoni yangu katika majadiliano yanayotendele. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima salama na amani, lakini pia nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia, tatu namshukuru Mhe. Waziri pamoja na watenaji wake kwa kuweza kutupatia mswada huu ambao umetengenezwa vizuri na uko makini sana.

Lakini pamoja na matengenezo ambayo yamekwisha kukamilika maatizo na dosari za hapa na pale zinakuwa hazikosekani, kwa upande wangu nianze kuchangia kwa kueleza haya yafuatayo. Kwanza kabisa nashukuru kwa hatua nzuri ambayo Zanzibar tumeweza kufikia kwa mara ya kwanza kabisa tokea Mapinduzi ya mwaka 1964 kuwa na wazo la kutengeneza Mswada wa Sheria utakaowezesha kuratibu masuala ya anga, mswada ambao utakapopitishwa utakuwa sheria kwa jumla.

Mhe. Spika, katika kupembua pembua maelekezo na maoni yaliyopo katika upande huu nimegundua jambo moja tu kwa upande wangu ambalo bado lina tatizo kidogo, sehemu zote ambazo zimekwisha kuonyeshwa katika mswada huu nimezikubali na sina mashaka nazo. Isipokuwa katika sehemu ile ya usalama anga, sehemu zote zimeelezwa kwa uwazi kabisa nakuonyehsa uhalisia wa hali itakavyokuwa katika maeneo yetu.

Mhe. Spika, jambo ambalo sikuliona humu ni namna ya kuweza kudhibiti uingizwaji na upitishwaji wa madawa ya kulevya, mimi sikuliona hilo katika Mswada huu, kwa hivyo ningeliomba Mhe. Waziri hilo aliangalie vizuri sana.

Halafu kwa upande wa mswada ambao umepitishwa kwa lugha ya kiingereza mimi kidogo nimepata tatizo na hili neno a*erodrome* hili neno hili kidogo linanipa mashaka kwa sababu katika *dictionary* ambalo ninajaribu kulitafuta tukiangalia neno a*erodrome* tunakuta ni kiji *air port* kiduchu ndio inakuwa na maana ya neno hili tukiangalia neno *aerodrome* tunakuta kwamba ni kiji *air port* kiduchu ndio inakuwa ina maana ya neno hili. Sasa sisi tunataka kutengeneza *Air Port* ya kimataifa ndani ya nchi yetu. Ningelipenda kupata ufafanuzi hasa wa neno hili ambalo limetumika katika huu Mswada wa kiingereza. Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, miye sina ziada isipokuwa naunga mkono Mswada huu na kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kikwajuni nakubaliana na hoja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Wakati tunasubiri wachangiaji wengine na Mhe. Waziri anaangalia *note* niliyompelekea ina mambo yanayohusiana na kama aliyoyazungumza Mhe. Mahamoud. Majadiliano yanaendelea.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii angalau kusema maneno machache sana katika Mswada huu, huku nikiwaachia wenzangu wakizidi kujiandaa. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Waziri na serika kwa jumla kwa kuona umuhimu wa kutengeneza hii Mamlaka ya viwanja vya ndege . Nasema hivyo kwa sababu nilijaribu kuangalia kazi za Mamlaka na changamoto ambazo tunanzo katika viwanja vyetu vya ndege. Nikaona kumbe suluhisho ya changamoto zile ni kupatikana kwa mamlaka hii.

Kwa mfano niliposoma kazi Nam. 1 inasema ni kuviendesha, kuvisimamia, kuvitunza na kuviendeleza viwanja vya ndege vya serikali katika Zanzibar. Hii ni changamoto kwa sababu ukiangalia mimi nilikuwa nasema usimamizi ni mdogo kwa sababu viwanja vyetu kwa kweli haviridhishi huduma zake. Mara nyengine unakuta yale mazingira yaliyovizunguka vile viwanja si mazuri. Ukiukagua ule uwanja unaweza ukaona ni hatari sana mle.

Ukiangalia kazi nyengine (c) kuhakikisha kwamba sera za viwanja vya ndege vya Zanzibar, kanuni na taratibu zinatekelezwa kwa mujibu wa viwango. Sasa hiyo viwango ndio kasoro yetu kubwa mpaka sasa hivi. Ule uwanja wa ndege pale Pemba una shimo kati kati. Jambo ambalo ni hatari kidogo. Mimi si mtaalamu lakini nahisi kama ukizungumzia viwango basi pale unapoteza sifa ya viwango ule uwanja. Mpaka leo hauna taa, uzio umejengwa juzi, *alhamdulilah*. Lakini kwa kweli katika hii sekta ya viwango bado tupo nyuma. Nasema ni muhimu sana kuona hii mamlaka kwa sababu mamlaka hii itakuwa moja katika kazi zake ni kuviboresha viwanja, kutoa huduma nzuri, kuangalia viwango na kila kitu. Jambo jengine ambalo nilikua nataka labda hili niulize swali.

Mhe. Spika, viwanja vya ndege vina mipaka yake. Tabaan kama vitakuwa bado havijatengenezewa hati miliki lakini utaratibu huo utakuwa unaendelea. Sasa kuna tatizo la utata limejitokeza. Siku moja hapa Mhe. Waziri wa Ardhi alikuwa akieleza namna ambavyo kuna viwanja vimegaiwa kinyume na utaratibu. Hata mimi siku moja nika - *pose question* kwake yeye. Nilikuwa nina maana yangu kubwa lakini akaikwepa, akaniacha bado nipo kwenye mabano. Uwanja wa Ndege wa Kiembesamaki, unamipaka yake. Lakini kulikuwa kuna maneno mengi labda niite kama uvumi. Kwamba kuna watu waliojenga hili barabara linalokwenda Fumba. Ukitoka Mbuyumnene pale kuna eneo sehemu ya Kisauni na watu wamejenga nyumba nzuri, kuna kigorofa kimoja safi sana nimekiona, nikasikia lile eneo ni sehemu ya Uwanja wa Ndege.

Mimi siku moja Mhe. Spika, nilinadishiwa kiwanja, lakini kabla sijanunua nikafanya utafiti kuna jamaa akanambia ngojea kwanza. Nilipomsikia Waziri akisema vile nikasema hapana. Lakini juzi nilipopita ile njia nimekuta ule ukuta hasa wa Uwanja wa Ndege unakaribia barabarani hapa na lile eneo lipo nje ya ule ukuta. Sasa namuuliza Mhe. Waziri je, eneo lile ambalo lipo nje ya ukuta lipo huku upande wa barabarani bado ni eneo la Uwanja wa Ndege lipo nje ya eneo la Uwanja wa Ndege na watu wanaweza kulitumia kwa shughuli zao za maisha.

Mhe. Spika, miongoni mwa kazi za Mamlaka ukiangalia kifungu cha 3(d) anasema ni pamoja na kusimamia utendaji kazi wa wadau wengine katika Uwanja wa Ndege. Hili ni jambo muhimu sana kwa sababu pale kuna watu wa kila aina wanafanya kazi pale Uwanja wa Ndege, kuna polisi, kuna usalama wa Taifa, kuna Uhamiaji, na watu wengine. Mimi nilichukulia kama nitakuwa nimefahamu vizuri hawa ndio wadau wanaofanya kazi pale. Sasa hawa watakuwa wanasimamiwa utendaji kazi wao na mamlaka hii ya Viwanja vya Ndege.

Mhe. Spika, kuna tetesi kwa sababu naziita hivi kutokana na kuwa sina ushahidi nazo. Lakini ni maneno ambayo kuwa yanazungumzwa sana, kwamba mapato yale ambayo yanakusanywa na Uhamiaji pale Uwanja wa Ndege hayafiki hazina inavyotakiwa.

Najua Uhamiaji ni Chombo cha Muungano, watalii wanakuja pale, wakija dhamana ni wao watu wa Uhamiaji, kuna malipo wanalipa. Lakini kuna tetesi kwamba kwanza hakuna uratibu mzuri wa kuweza kujua kwamba ni watalii wangapi waliokuja na wamelipa kiwango gani cha pesa, kwa hivyo kuna mianya pale ya watu kutia pesa mifukoni.

Nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri wa Mawasiliano kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ikishakutiwa saini na Rais kwa kushirikiana na vyombo vya ukusanyaji mapato ikiwemo *ZRB* na Waziri Afisi ya Raisi mwenyewe walishughulikie kwa karibu sana hili suala.

Kuna mtu kanihadithia kuna kijana alikuwa tayari keshakuwa kwenye Chuo anafanya digirii aliposikia kuna *transfer* ya Uwanja wa Ndege akasema sitaki digirii tena mimi naondoka nakwenda zangu Zanzibar kufanya kazi ya Uwanja wa Ndege. Muda mfupi tu. Mimi simjui nani na wala sikuulizi. Lakini watu wanaona maisha yake yanabadilika kwa *speed* kiasi cha kushangaza. Sasa hii ni *indicator* mbaya, nilikuwa naomba sana lishughulikiwe. Sitaki kumtaja mtu kwa sababu simjui lakini kwa sababu ni mapato ya wananchi napaswa kuyatolea tahadhari.

Jambo jengine Mhe. Spika, katika bodi ya Wakurugenzi kuna kifungu Nam. 2 inasema: Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti isipokuwa awe mwenye taaluma na uzoefu katika fani ya anga, utawala kwa jumla au utumishi wa umma. Mimi nilikuwa nafikiri Mhe. Spika, huku tunakokwenda tunaingia katika soko la ajira la Afrika Mashariki. Kule tutakuta watu wana elimu zao kubwa na tabaan kwa sababu kuna ushirikiano, siku nyengine kutakuwa kuna vikao vya pamoja vya kujadili mambo. Tukimuweka mtu kwa sababu hii ipo kwenye mabano, mtu anaweza akaona ana taaluma yake ndogo sana halafu aka-*qualify* kwa kutumia kifungu hiki, kuteuliwa nafasi kama hiyo, lakini anapokwenda kushiriki kwenye Vikao vya Afrika Mashariki ikawa sawa sawa na wale waliokwenda katika Bunge la Kuunda Katiba ya Jamhuri ya Muungano aliyemtaja Mheshimiwa Mwana Mapinduzi pale akina Pasganda mawazo yao hayakuwa yakiona mbali na ndio leo kukawa na manung'uniko ya namna hii.

Mhe. Spika, hofu yangu kubwa huyu mtu akiwa hayupo katika *level* inayotakiwa basi anaweza akawa hana ushauri mzuri katika vikao anavyovihudhuria na vyengine itakuwa vinajaribu kuangalia maslahi ya Zanzibar. Ushauri wangu hapa ateuliwe mtu mwenye elimu anayejulikana kwamba anaweza kushirika katika ushindani wa namna hiyo.

Mhe. Spika, mimi binafsi naunga mkono sana Mswada huu kwa sababu ni muhimu sana mia kwa mia. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kuniruhusu kuchangia mchango huu. Kwanza kabisa sina budi kumshukuru Waziri, Naibu Waziri na wizara yake kwa ujumla kwa kuleta Mswada huu. Kama itakuwa ni Mswada wa mwanzo kwa alivyoupanga kiufundi na kiutaalamu. Itakuwa ni darasa kubwa kwa bodi nyengine. Mimi nitagusia katika bodi ukurasa wa 197.

Mhe. Spika, unasemka kwamba Mwenyekiti atateuliwa na Raisi, nafaikiri ndio sheria yetu ya Zanzibar inavyotueleza hivi. Hawa wengine atawateuwa kwa vigezo gani na sifa gani. Isijekuwa mtu mmoja anavaa kofia tatu (yaani ana bodi tatu) kama

tulivyozoea hapo nyuma, akitoka bodi hii anakwenda bodi hii, akitoka bodi hii anakwenda bodi hii, nafikiri hatutofika pahali. Tuangalie mtu uzoefu wake na sifa zake. Huwezi ukenda ukamchukua mtu Nyarugusu ukaja ukamleta pale ukamwambia kwamba aendeshe chombo kwa kuwa mtoto wa kaka au mtoto wa mjomba, nafikiri hatutofika hapo. Tuangalie vigezo hivi vya taaluma na sifa za mtu.

Mhe. Spika, hata kwenye Bodi ya Bandari itakayokuja vile vile tuangalie vigezo hivi. Atafutwe mtu mwenye ujuzi wake na uzoefu wake. Tusijetukatoka humu Wawakilishi tukenda tukapewa nafasi kama zile humu ndani. Mhe. Spika, mimi mchango wangu ni huo kwa muda huu. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru na pia nimpongeze Mhe. Waziri na wizara nzima kwa ujumla kwa kutuletea Mswada huu. Mswada ambao kwa kweli unadhamiria kuweka mazingira mazuri katika huduma za viwanja vya ndege na kurahisisha hatua nzima ya usafiri wa anga hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, mchango wangu wa mwanzo ninde kwenye kifungu cha 6 kuhusu muundo wa bodi. Ningeshauri tu kwamba kama ambavyokuwa Kamati ya Mawasiliano ilivyosema kwamba wajumbe wa bodi hii wengi wao kama si wote ni kutoka serikalini. Ninavyokumbuka Sera ya Usafiri wa Taifa imehimiza umuhimu wa mashirikiano kati ya *public private sectors* au *Partnerships* na wale wa Serikali kwa ujumla kwamba kuwe na ushirikiano baina ya taasisi binafsi na serikali. Sasa ukituwekea wajumbe wa bodi wote wakiwa kutoka serikalini nadhani hata ile Sera ya Taifa ya Usafiri itakuwa hatujaifanyia haki.

Mhe. Spika, mimi niombe kabisa kwamba kifungu hiki cha 6 tungewapunguza wajumbe kutoka serikalini, tukawatafuta wajumbe wa sekta binafsi ambao wanataaluma sawa na hii ambayo sheria imesema, tukawaweka kama ni sehemu ya wajumbe wa bodi hii ambayo inakusudia kuleta mazingira mazuri ya usafiri wa anga.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu tukiwaweka wajumbe peke yao kutoka serikalini tena pengine wengi watakuwa na Idara hii hii ya Wizara ya Mawasiliano, nadhani kutakuwa na hali ambayo haipendezi. Ushauri wangu ni kwamba kifungu hiki cha wajumbe wa bodi tungewapunguza kutoka serikalini, tukaongeza wajumbe wawili kutoka sekta binafsi wenye sifa sawa sawa ambazo zimetengwa kwenye sheria hii. Mhe. Spika, jengine kifungu cha 6(2) hapa tumesema kwamba mtu hatoweza kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi isipokuwa awe ana taaluma ya uzoefu katika fani ya anga, utawala kwa jumla au Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, tusisahau kwamba Zanzibar tuna diploma nyingi za utawala, tuna diploma nyingi za uongozi, kwa hivyo hii *sentence* kwa kweli imejifunga mno. Mimi nakubaliana na Mhe. Ali Abdalla Ali kwamba tungeweka sifa. Kama ambavyo tumesema kuwa mkurugenzi ni lazima awe muhimili wa Chuo Kikuu kwa maana ya digirii ya kwanza au digirii ya pili. Hapa tungeweka wazi kwamba huyo Mwenyekiti wa Bodi ambaye ndiye muhimili mkubwa wa bodi hii basi angekuwa na sifa isiyopungu ya digirii ya kwanza ya fani hii.

Mhe. Spika, lakini tukisema tu mwenye utawala na uzoefu wa utawala, pengine mtu amekaa pale Uwanja wa Ndege miaka 40 kwa vyovyote atakuwa ana uzoefu wa

utawala kwenye huduma hizi za anga, lakini atakuwa hana sifa ambazo zitaweza kutusaidia kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki. Kwa kweli ni lazima tuwe na wataalamu ambao wana sifa hizi na watakaoweza kujenga hoja ili kuondokana na migongano ambayo Zanzibar baadaye ingeweza kutokezea, migongano ya kimaslahi kwenye Sekta ya Anga.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ningeligusia kwenye kifungu cha 11 (2) (c) Mhe. Waziri ametwambia kwenye mswada huu kwamba moja kati ya kazi hizi za bodi hii na Mkurunzi kwa ujumla ni kutekeleza sheria za Usafiri wa Anga za Tanzania zinazotumika katika usimamizi wa Viwanja vya Ndege.

Mhe. Spika, mimi nina wasi wasi kwamba tunataka kujitia kwenye migongano tena. Wakati lengo la serikali ni kuondosha migongano kwenye sheria nyengine za Tanzania kama ambavyo tumeunda Sheria ya Bandari hatukuagiza kwamba Sheria ya Bandari kwamba lazima tutekeleze Sheria za Bandari za Tanzania Bara. Wasi wasi ni kwamba tukilitua jukumu hili maana yake kuna sheria hii itagongana na sheria za Tanzania Bara za Viwanja vya Ndege na hatimaye wenzetu hawa tutawapa jukumu kubwa la kuweza kutekeleza sheria mbili ambazo kwa kweli zitawakwaza.

Mhe. Spika, nadhani kipengele hichi wenzetu hawa na pengine mwanasheria akiangalie zaidi kutushauri vizuri ili tusije tukasababisha migongano kati ya sheria hii ya Zanzibar na Sheria ya Tanzania Bara ambayo baadaye itawakwaza watendaji wetu, kwa lengo zuri tu ambalo tumejipangia. Mhe. Spika, mwisho kabisa niseme tu kwamba sheria hii iende sambamba na kanuni ambazo Mhe. Waziri atakuwa na uwezo nazo kuzitunga. Haitapendeza kwamba sheria tumeweka nzuri, Mhe. Waziri akatunga Kanuni nzuri baadaye utekelezaji wake ukawa haulingani na kanuni hozo na utaratibu wa sheria.

Mhe. Spika, baada ya hapo naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kutujaalia neema yake ya uhai, afya, tukaweza kukutana hapa tena leo hii, kuendelea na mjadala kwa mambo yanayohusu nchi yetu. Pili Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa maoni yangu kuhusiana na Mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar.

Mhe. Spika, nataka niipongeze sana serikali kupitia Wazara ya Mawasiliano na Miundombinu kwa kuja na wazo hili la kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar. Nchi yetu hivi sasa inashuhudia mipango kabambe ya kujaribu kututoa hapa tulipo na kutupeleka katika ujenzi wa uchumi wa kisasa. Hilo limedhihirika katika bajeti mbali mbali ambazo tumezijadili hapa. Bila shaka katika hali kama hiyo haja ya kuimarisha njia za mawasiliano ndani ya nchi lakini hata baina ya nchi yetu na nchi nyengine ni suala muhimu sana.

Katika hilo usimamizi na uendeshaji wa sekta hizi ni muhimu. Kitendo kile cha kutoka katika Sekta hii ya Usafirishaji wa Anga kuwa inasimamiwa na Idara tu ya Serikali kama zilivyo Idara nyengine lakini sasa kuja katika mfumo ambao kuwa utakuwa na mamlaka ya Viwanja vya Ndege ni jambo la kupongezwa na linaashiria maendeleo katika nchi yetu. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba niipongeze sana hatua hiyo.

Mhe. Spika, pili nitoe maoni ya jumla kidogo. Hivi sasa tunajadili Mswada unaohusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, lakini katika hii *Bill Suppliment* tuliyopewa kuna Miswada miwili ndani yake. Mimi kwa maoni yangu nilikuwa naona kwamba Zanzibar tunaingia katika mfumo mpya wa kurudisha sheria nyingi pasi na sababu. Kwa sababu suala la kuanzisha Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege halafu tukaja tukawa na Sheria ya Kusimamia Uwendeshaji na udhibiti wa Viwanja vya Ndege, naona mambo haya yangewezwa kuchanganywa na ikawa ni sheria moja.

Mhe. Spika, moja katika mambo yanayotizamwa katika misingi ya sheria na tunao wanasheria wazoefu hapa, ni suala zima la Sheria kuwa rahisi kufanywa marejeo na kuweza kumfanya anayetumia kuweza kujua au kukitafuta anachokitaka kwa urahisi. Lakini inaonekana nchi yetu siku hizi zaidi ya mfumko wa bei tunajenga pia utaratibu wa kuwa na mfumko wa sheria.

Mhe. Spika, nitoe mfano ingawa hatujadili masuala hayo. Moja katika eneo ambalo linalalamikiwa sana linaleta *confusion* ni suala zima la ardhi. Katika ardhi Mhe. Spika, tuna sheria saba hivi sasa nazo ni:

1) *Land Tenure Act*
2) *Land Dedication Act*
3) *Land Survey Act*
4) *Land Registration Act*
5) *Land Transfer Act*
6) *Land Tribunal Act na tukapitisha*
7) *Condominium Act*

Hizi kwa njia moja au nyengine zote zinahusiana na masuala ya ardhi. Sasa inamfanya mtu anayetaka kujua kwa mfano masuala ya ardhi kwetu hapa atafute kitu hiki kipo upande huu, hiki kipo upande ule. Kwa hivyo haiyendi na ule msingi mzuri tulioujenga ambao wewe pia Mhe. Spika, umo katika fani hii ya Sheria ya kuwa na kitu *consolidation* ku- *consolidate* vitu.

Bahati nzuri Mhe. Spika, suala la *consolidation* katika sheria halipo katika kutunga sheria tu, hata mahakamani kule tukenda, tunakatazwa kuwa na *multiplicity of suite*, kama vitu vinalingana unatakiwa vyote uviweke katika *suite* moja. Vile vile hata kama unamshtaki mtu pengine katenda kosa moja ambalo linamakosa mengi. Sio unafungua kesi hii mbali na hii mbali na hii mbali, uwe unafungua kesi moja halafu unamuorodheshea yale makosa yake.

Sasa nilidhani na mambo haya ya Sheria hizi Mhe. Spika, tungeweza kuwa na sheria moja halafu kama zilivyosheria nyengine zikawa na sehemu tofauti ambazo zinashughulikia yale maeneo tofauti ambayo kuwa yanataka kushughulikiwa. Kwa hivyo nilikuwa nadhani kwa msingi mzuri lakini bahati mbaya tuna Miswada miwili hapa. Nadhani ningelikuwa vizuri tuka – *consolidate*. Nitoe mfano mwengine mzuri

Mhe. Spika wa *good practice* ni sheria tuliyoipitisha nafikiri kikao cha mwezi wa jana, tulivyoipitisha ile Sheria ya *Public Service Act* ile ime–*consolidate* sasa. Kwa hivyo mtu anayetaka masuala yote yanayohusu utumishi wa umma katika nchi yetu, anapokwenda pale anaridhika na anapata mambo yote yaliyokuwa yanahusika na pale.

Hata zile sheria zetu Mhe. Spika, ya vyombo vinavyojitegemea kwa mfano Baraza la Wawakilishi, Mahakama, Idara Maalum, zote zimeingizwa mle mle sasa hivi. Kama tumeweza kufanya vile sijui kwa nini katika hili serikali ikaona kuna haja ya ku-*duplicate* sheria kwa misingi hii. Kwa hiyo nilikuwa naomba hilo kidogo Mhe. Spika, tulitizame.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ya jumla sasa naomba kidogo niupitie Mswada. Kwanza nataka kusema kitu kimoja, nataka kuipongeza sana Kamati ya mawasiliano na Ujenzi. Maeneo mengi ambayo tungependa kuyatolea maoni wameyagusa na yamefanya kazi nzuri sana. Mhe. Spika, nikiondoka hapo nilikuwa nina mambo yafuatayo kuhusiana na Mswada wenyewe. Kwanza nianze na jumla katika ufafanuzi au tafsiri. Utaratibu wa kisheria ni kwamba ufafanuzi au *definition* ya maneno yale huwa yanapangwa kwa *alphabet.* Sasa katika hili kidogo wa Kiingereza na wa Kiswahili kuna baadhi ya maeneo ile *alphabet* haifatwi vizuri. Nilikuwa naomba na hilo walitizame kwa ujumla wake.

Mhe. Spika, pili nataka nigusie kifungu cha 5(1)(a) katika kifungu hichi Mhe. Spika, kinazungumzia kuviendesha, kamati imeongeza neno kuvidhibiti, kuvisimamia, kuvitunza na kuviendeleza Viwanja vya Ndege vya Serikali katika Zanzibar. Mhe. Spika, nilikuwa najiuliza kwamba hivi kweli tunataka tuwe na mamlaka ambayo kazi yake ni kusimamia, uendeshaji, utunzaji na Udhibiti wa Viwanja vya Ndege vya Serikali tu. Najua sasa hivi hatujafika kuwa na viwanja vya Ndege vya binafsi Zanzibar. Lakini tumesema nchi yetu imekaa katika *pass* ya kuelekea katika maendeleo. Sasa je, tukifika huko mbele tukawa tuna *private* hizo alizosema Mhe. Mahamoud, *private aerodromes* au vitu kama hivyo. Nani atasimamia udhibiti wa ubora wake na mambo mengine kama hayo.

Mhe. Spika, nasema hivi kwa sababu kidogo naona hii sheria yenyewe inayo jambo zuri lakini limeachwa hapa kwenye kifungu cha 5. Ukiangalia kifungu cha 18(a) kilichopendekezwa katika Mswada huu. Kinasema hivi:

Kifungu cha 18(a)

> “Mamlaka inaweza kuhusiana na Viwanja vya Ndege vya Serikali au Viwanja vya Ndege visivyokuwa vya Serikali kuteuwa watu au aina ya watu kama itakavyoona inafaa kuwa maafisa walioidhinishwa kwa madhumuni ya sheria hii”

Sasa huku kwenye kifungu cha 18 tumetambua viwanja vya ndege vyote vya serikali na visivyokuwa vya serikali. Lakini huku kwenye sheria inakoanzisha hasa kazi za Mamlaka tumeviwacha viwanja vya Ndege ambavyokuwa sio vya serikali. Kwa hivyo nilikuwa nadhani kwamba hili tulitizame ili tujiwekee mustakballi mzuri. Isiwe tena kila wakati tunahaja kufanya marekebisho kwa mambo madogo mdogo ambayo yanaweza yakajitokeza. Kama havipo maana yake hatuna haja ya kuvizibiti lakini vitakapokuwepo sheria itakuwa tayari ime *take care* juu ya jambo hilo.

Mhe. Spika, kifungu cha 5(1)(g) kinazungumzia kusimamia ardhi iliyondani ya mipaka ya Uwanja wa Ndege. Mimi nilikuwa naomba tu kwa sababu tunapata matatizo haya na hata hivi sasahivi tunayo matatizo haya ya yale maeneo yaliyozunguka viwanja vya ndege. Nilikuwa nasema pengine na kwa sababu hapa neno lililotumika ni kusimamia tu. Ardhi hiyo nilikuwa napendekeza kama itaonekana inafaa tuongeze maneno pale mwisho isomeke 'na maeneo ya karibu ya uwanja wa ndege'.

Ili kuhakikisha kwa jumla zile sheria zinazohusu viwanja vya ndege zinafuatwa sio tu katika lile eneo la viwanja vya ndege, lakini katika zile *plan* ambazo zitakuwepo pale, kuweza kuhakikisha kwamba yale masuala ya *public interest* yanazingatiwa hata na wale watumiaji wa ardhi ambazo zipo pale. *After all* nchi yetu ardhi yote ni mali ya serikali.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 5 (1) (j) kuna maneno mawili yametumika na hili ndio tatizo jengine tunapotafsiri wale wenye tafsiri za Kiswahili na ukitizama za Kiengereza huwa hawana *consistency* ya maneno, ndio mara nyingi tumekuwa tukilizungumza.

Mhe. Spika, kifungu cha 5(1) (j) ukitizama neno lilotumika kuna neno pale limetumika asasi naomba niisome. "Kusimamia na kudhibiti mambo ya usafiri, kupokea na kutunza bidhaa za hatari ndani ya mipaka ya viwanja vya ndege na maeneo ya karibu kwa kushirikiana na asasi nyengine". Kidogo nadhani tunahitaji kuwa na *consistency* katika hilo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 5(3) (e) pale linapohusiana na suala zima la mamlaka katika uwezo wake wa kutekeleza kazi zake, inasema kufanya jambo jengine lolote kama itakavyoelekezwa chini ya sheria hii. Mimi nilikuwa naomba kupendekeza kwamba pengine inaweza ikatokezea huko mbele mahitaji ya mambo yanayohusiana na haya mamlaka ikapewa kazi. Kwa hivyo, tungeongezea tukasema au sheria nyengineyo kwa maana ya kwamba isitufunge kuja kutunga sheria ambayo itaipa mamlaka kazi ya kufanya kazi nyengine nje ambavyo imetajwa katika sheria. Kwa sababu itakuwa imetungwa na Baraza lako bado itakuwa katika misingi ya kisheria katika nchi yetu wala haitahitaji kuja kurudi katika sheria hii kuja kuifanyia marekebisho. Mhe. Spika, nilikuwa naomba kama itaonekana linafaa basi ningependekeza tulitazame.

Mhe. Spika, nije katika kifungu ambacho wenzangu wameshakitolea maoni, katika kamati na maoni aliyotoa Mhe. Hija kifungu cha 6 ambacho kinazungumzia Bodi ya Wakurugenzi. Mhe. Spika, kifungu cha 6 kwanza nataka nikubaliane na ile dhana nzima iliyoletwa na kamati kwamba tumekuwa na sheria nyingi sasa, mimi nimeingia kipindi kifupi lakini sheria tunazoletewa hapa mara nyingi zinazohusu muundo zinakuja na dhara hii ya Katibu Mkuu wizara inayohusika na mambo fulani au mwakilishi wake. Mhe. Spika, tuliwahi kutoa maoni sikumbuki katika sheria gani nafikiri sheria ya uhakika wa chakula na sheria ya mtoto.

Mhe. Spika, Makatibu Wakuu wanakuwa na kazi nyingi sana kwa hivyo ule uwezekano wa kuhudhuria vikao kama hivi unakuwa mdogo. Mhe. Spika, tatizo la kuacha mwanya kama huu ni kwamba huyu mwakilishi wake siku nyengine pengine

atashiriki yeye pengine atashiriki Katibu Mkuu hapapatikani *consistency* katika maamuzi na *continuity* na katika taasisi zetu suala la *continuity* na *consistency* ni suala muhimu sana kuwa na mtiririko wa mawazo ambayo yanaendelea katika vikao.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nasema kama suala la ushiriki wa ile taasisi wizara ile ni muhimu na mimi nakubaliana kabisa kwamba hizi wizara zilizotajwa hapa zote ni muhimu kwetu. Lakini pengine ingefaa tukawa na vifungu vinavyosema kutakuwa na mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ile au mwakilishi wa wizara ile moja kwa moja. Kwa hivyo, itaondoa ule usumbufu wa kwamba leo kashiriki huyu, kesho kashiriki ule na mfumo wetu wa wafanyakazi Mhe. Spika, tunaujua sote mara nyengine hata huko peana taarifa inakuwa mtihani. Kwa hivyo, inapofika pahala pa kujua kiliamulia nini inakuja kuwa shida kunatokezea mgongano. Mhe. Spika, kwanza nataka kuungana na kamati katika hilo.

Mhe. Spika, lakini maoni yangu mahsusi katika kile kifungu kidogo cha (f) pale kwenye wajumbe wengine wasiozidi wawili watakaoteuliwa na waziri wenye ujuzi, taaluma au uzoefu katika mambo ya anga, sheria, fedha, utawala au uhandisi. Mhe. Spika, ukitizama *composition* ya bodi huku juu takriban wote hawa watakuwa ni watu wa serikali, kuna mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais mara nyingi huwa ni kutoka huko huko serikalini, Katibu Mkuu au mwakilishi wake kutoka Wizara ya Fedha, au Katibu Mkuu au mwakilishi wake kutoka wizara yenye dhamana ya mambo ya uwanja wa ndege, Mkurugenzi Mkuu, Mjumbe mmoja kutoka Jeshi la Polisi. Mhe. Spika, hawa tayari wote wanatoka serikalini katika *public sector*.

Kwa hivyo, nadhani hii (f) sasa inge-*specify* hawa wajumbe kamati imesema angalau mmoja, mimi naomba wote wawili watoke katika *sector* binafsi. Kwa sababu kama ilivyosemwa hapa kwamba tumepitisha sera ya usafiri ambayo inazungumzia msingi mkuu wa *public private partnership* na si katika sekta ya usafiri katika mambo yetu mengi sasa hivi tunasema kwamba wakati umefika kuwa na ushirikiano. Mhe. Spika, dunia nzima inafanya mabadiliko katika mambo ya maendeleo hasa katika mambo haya ya miundombinu na mawasiliano, kuna msingi mkubwa wa ushirikiano.

Kwa hivyo, tunazo taasisi hapa ambazo zina *interest* ya moja kwa moja katika masuala haya na zinato ushiriki mkubwa sana, pengine kuna jumuiya hizi zinazooenesha biashara ya utalii hapa, kuna jumuiya za wafanyabiashara, kuna jumuiya za *tour operators*. Mimi naona Mhe. Spika, hawa wangepaswa kupewa nafasi kwa hiyo nilikuwa nataka kupendekeza hawa wajumbe wengine wawili wote wangetoka katika sekta binafsi. Kwa hivyo, napendekeza ingekuwa *specified* hivyo.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 10 (2a) kinachozungumzia sifa za Mkurugenzi Mkuu, imesemwa hapa na imefanyiwa marekebisho kidogo na kamati, lakini kwanza nayaunga mkono mapendekezo ya kamati.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaotoka nje kwa dharura tusichukue muda mkubwa turudi kwa sababu shughuli hii inaelekea haitachukua muda mkubwa sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nasema katika kifungu cha 10 (2a) kwanza mimi nasema nayaunga mkono mapendekezo ya kamati yakuweka wazi zaidi zile sifa za mtu ambazo za kuchaguliwa kwa Mkurugenzi Mkuu. Lakini mimi nilikuwa nataka kusema haya maneno ya mwisho pia kidogo mimi hayanipi raha, yanasema awe

amehitimu kutoka katika Chuo Kikuu bila shaka imependekezwa kwamba angalau kwa kiwango cha shahada ya kwanza ya sheria kwa uzoefu angalau miaka 3. Halafu mwisho anasema au kutoka katika chuo kinacholingana na hicho. Mhe. Spika, maneno haya mimi ningependekeza yaondolewe.

Mhe. Spika, hoja yangu ni kwamba siku hizi tumekuwa na huu mfumko wa bei, mfumko wa sheria Zanzibar pia tuna mfumko wa vyuo siku hizi, kila pahala siku hizi kuna watu wanakuja na vyuo. Kwa hivyo, mara nyengine utaambiwa hiki kimeungana na chuo fulani cha nje huko, mara nyengine katika ukosefu wa ufuatiliaji tunadhani hivyo lakini halafu tunakuja kugundua kwamba vyuo vyenyewe vingi vina matatizo. Kwa hivyo, kwa dhamana kubwa kama hii huyu ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, mimi nadhani sifa yake ingeishia awe ni muhitimu wa shahada angalau ya kwanza ya fani ya sheria kama ilivyopendekezwa na kamati, lakini iwe kutoka Chuo Kikuu au chuo kinacholingana na hicho. Mhe. Spika, chuo kinacholingana na hicho mimi nilikuwa naomba kwamba tuiondowe.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 21 (2) hapa pana misingi mizima ya *transparence* panahusu masuala ya fedha na hesabu za ukaguzi. Mhe. Spika, kifungu hiki kinasema nakla ya taarifa zilizotajwa katika kijifungu cha kwanza cha kifungu hiki na nakala ya ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu kama ipo zitawasilishwa kwa waziri pamoja na ripoti kuhusu shughuli za mamlaka katika mwaka huo wa fedha.

Mhe. Spika, tunaelekea katika zama mpya za uwazi, uwajibikaji. Mimi katika hili sio vibaya pamoja na kwamba ndugu zetu wa damu wananitenda katika mambo mengi, lakini katika hili nawasifu kidogo siku hizi kumekuja utaratibu mzuri wa kuwa na mamlaka kama hizi wanachapisha taarifa kama hizi katika vyombo vya habari.

Mhe. Spika, unakuta mamlaka kama hizi zimenunua kurasa katika magazeti wamechapisha *statement of accounts* ili kudhihirisha kwamba hatuna mashaka na hesabu zetu. Mhe. Spika, hili uzuri wake nini? Hili uzuri wake ni kwamba linajenga imani ya wale watu wanaotaka kuekeza katika hilo eneo, kwamba hapa hapana matatizo ya masuala ya fedha. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kupendekeza kwamba katika kifungu hiki kama serikali haina pingamizi kubwa ikubaliane na pendekezo la kwamba tuongeze maneno na kuchapishwa kwenye gazeti rasmi la serikali na magazeti yanayosomwa na watu wengi nchini. Mimi nadhani Mhe. Spika, itasaidia kujenga *confidence* kubwa zaidi.

Mhe. Spika, sasa nije katika kifungu cha 26 kinahusu adhabu, hapa kidogo naomba nisaidiwe. Mhe. Spika, mimi bahati mbaya ni *lawyer by training* si *lawyer by profession.* Kwa hivyo, mambo mengine nakubali sina maarifa nayo makubwa ambayo wenzangu wanayo, lakini ilikuwa nadhani katika huo uzoefu mdogo nilionao masuala ya adhabu na bahati nzuri Mhe. Spika, uliwahi kuwa Hakimu unayajua, kwamba lazima kuwe kuna *consistency* katika adhabu ya kifungo na faini. Kwa hivyo, kifungu cha 24 (1) kimetaja kosa pale sina haja ya kulisoma nataka niseme ile adhabu inazungumzia au naomba niisome kwa faida ya wajumbe inasema.

“Mtu yeyote atakayeondoa kuangamiza au kuharibu mali yoyote inayomilikiwa au iliyo chini ya uangalizi, au iliyo chini ya mamlaka au ataizuia mali hiyo kutumiwa au kutumika katika hali ambayo imekusudiwa, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa

hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi 500,000 au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka 2 na kusawazisha uharibifu, upotevu wa hasara iliyofanywa".

Mhe. Spika, sasa hapa pana faini ya shilingi 500,000 na *equivalent* yake ni kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka 2. Lakini nikenda katika kifungu cha 26 kinasema. "Mtu yeyote atakayetenda kosa chini ya sheria hii au kanuni zilizotungwa chini yake ambalo hakuna adhabu iliyotajwa, kule kuna kosa *specific* hapa makosa ya jumla ni kwamba atawajibika baada ya kutiwa hatiani kulipa faini isiyozidi shilingi milioni 2, 500,000 au kifungo kisichopungua miezi 6 au adhabu zote mbili kwa pamoja. Mhe. Spika, ni kwamba kule faini ni shilingi 500, 000 lakini kifungo kisichopungua miezi 6, huku faini isiyozidi shilingi 2,500,000 lakini huwa tunazungumzia miezi sita hapana *consistency*. Kwa hivyo, nadhani hili pia tungelilitazama ili kuwa na mfumo mzuri zaidi unaolingana katika masuala haya ya sheria.

Mhe. Spika, naomba na mimi ni *comments* kidogo katika kifungu cha 11 (2c) katika kutoa kazi za Mkurugenzi Mkuu inasema ni kutekeleza sheria za usafiri wa anga za Tanzania zinazotumika katika usimamizi wa viwanja vya ndege. Mhe. Spika, mimi hili kama alivyosema Mhe. Hija linanipa matatizo kidogo. Najua labda tumeweka hili kwa sababu Katiba ya Muungano imetaja usafiri wa anga kuwa ni suala la Muungano. Lakini kama tumeamua kutunga sheria yetu ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege bila shaka imezingatia mambo yote ambayo kwa jumla na katika sheria ile kule yapo.

Mhe. Spika, moja katika jambo zuri kuwa na sheria ni kuwa tunafanya *reference* ya kutunga sheria. Mhe. Spika, wasi wasi wangu tukishakiingiza kifungu hiki pengine leo sheria zinalingana, kesha zinaweza zikaja zikagongana hapa. Mhe. Spika tukishakuwa katika sheria yetu tunaingiza kumtaka Mkurugenzi Mkuu kutekeleza sheria hizi kuja kukitokezea mgongano sheria ipi itasimama hapa, nadhani tuna *invite* mambo hayana sababu. Lakini pengine sasa hivi zinalingana lakini ikija ikibadilishwa hapa ndio tumeshaitambua tutakuwa tunajiingiza katika matatizo. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Spika, sioni kama tunaridhika kwamba sheria yetu ni nzuri na imekidhi mahitaji yetu yote tunayoyahitaji katika masuala mazima ya usimamizi wa viwanja vya ndege kupitia mamlaka haya sidhani kama tuna haja ya kuingiza kifungu hiki ambacho kinatuletea matatizo huko mbele ya safari.

Mhe. Spika, tumetoa mfano hapa na mara nyingi tulipokuwa tukizungumza suala la mafuta tuliambiwa mafuta tusiliingize na mifano hii kwa sababu hili ni suala *specific* linahitaji makampuni ya nje wanaweza hata tukipitisha sheria wakakataa. Lakini tukatolewa mfano wa bandari sasa kama katika sheria za bandari tumepitisha hapa haikuleta *reference* kwa sheria zilizoko kule pamoja na kwamba Katiba imeitambua pia kwa mamlaka ya Muungano. Pia tunatambua kwamba tangu kuundwa kwa Muungano huu bandari haijawahi kuendesha kimuungano, hasa kwa nini tuogope katika suala hili la Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nadhani kwamba katika hili hiki kifungu tungelikiondoa wala sioni kama kitatupa shida yeyote.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nilikuwa na mambo mengine mawili madogo ya jumla hayamo katika mswada lakini yanahusiana na masuala haya ya viwanja vya ndege ambayo tutayatungia sheria. Kwanza Mhe. Spika, nimetoa pendekezo hapa la kwamba katika ile *composition* ya bodi tuone haja ya kuingiza sekta binafsi, lakini

siku hizi tunatumia lugha inasema angalizo. Nilikuwa nataka kutoa ushauri kwa jumla kwa serikali labda ukifika wakati wake litafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, tumekuwa na utaratibu mara nyengine wa kuwaingiza wana siasa na lakini kwa madhumuni ya hapa hasa nizungumzie kwa mfano watunga sheria katika bodi za mashirika, na hili lipo kwetu hapa lakini pia lipo Bara. Mhe. Spika, kumekuwa na maoni kwamba suala hili sio sahihi kwa nini Mhe. Spika? Kwa sababu Katiba zetu zinatambua mgawanyo wa madaraka baina ya Mamlaka ya Uendeshaji Serikali, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Mamlaka ya Utoaji Haki.

Mhe. Spika, moja katika jukumu la chombo hiki katika kifungu cha 5(a) cha Katiba yetu kinasema kazi ya Baraza la Wawakilishi ni Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma ni Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, sisi katika kazi zetu ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Kwa hivyo, tukichukua watu miongoni mwetu halafu wakawa wanashiriki katika bodi ambazo zinafanya maamuzi ya uendeshaji, halafu maamuzi yale sisi ndio wasimamizi wake.

Mhe. Spika, mara nyengine utakuja kumkuta mjumbe anashindwa kuonesha mapungufu kwa sababu na yeye mwenyewe alishiriki katika maamuzi yale. Kwa hivyo, nilikuwa nataka hili serikali ilione kwa ujumla wake pengine huko tunakokwenda katika kuboresha mfumo wetu wa kisheria Mhe. Spika, nadhani tuna haja ya kulitaza hilo kuona kwamba wawakilishi wabakie katika kazi ile ya kusimamia serikali na wataalamu pengine watumike katika bodi kama hizo.

Mhe. Spika, jengine la jumla nataka kusema sheria hii imeweka msingi mzuri wa usimamizi na uendeshaji wa viwanja vya ndege kupitia mamlaka haya ya viwanja vya ndege. Mhe. Spika, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri tuliwahi kumwambia katika michango mbali mbali kwamba hebu aitupie macho tena *VIP*. Mhe. Spika, kama tunaelekea katika zama mpya za ujenzi wa Zanzibar ya kisasa inayojenga uchumi mpya, inayohitaji kujikita katika kuonekana kwamba inasimamia sheria kikamilifu ili kuwajengea imani watu mbali mbali, hata mashirika ya kimataifa yanayosimamia mambo haya ya ufuataji sheria tunataka tuonekane mambo yetu yanaendeshwa kistaarabu na kwa mujibu wa kanuni.

Mhe. Spika, bahati mbaya *VIP* yetu imegeuka kama vile haina mwenyewe, unakuta watu pale wanapiga kelele mara nyingi hawana sifa ya kutumia *VIP*. Mhe. Spika, mimi mmoja situmii *VIP* mara chache sana niwe nimefuatana na kiongozi wangu kama tunasafiri pamoja. Lakini ninachotaka kusema huu ni utashi wangu, lakini unapokwenda mara nyengine kama unataka kumsindikiza mtu unakuta watu hawana haki ya kutumia pale. Lakini sasa umejengwa utaratibu mara moja niko pale nikagundua kitu cha ajabu sana, kuna mtu yeye mwenyewe ni mfanyabiashara tu anatumia halafu kampa fursa kutokana na juhudi ya rafiki yake nae anatumia. Siku hiyo niliyokwenda yule rafiki yake wamekuja jamaa zake nae pia kaja kuwapokea sasa imekuwa kama vile tuko katika msikiti Imamu kila mmoja anakuja kuunga safu.

Mhe. Spika, hivyo katika utaratibu kama huu hausaidii hata kidogo kuona kama tunatunza zile nidhamu za uendeshaji wa mambo yetu. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hili alitazame sana kwa sababu haya aliyoyazungumza hapa mimi natofautiana na Mhe. Mahamoud aliposema kwamba sheria haijataja mambo ya madawa ya kulevya, yale yana sheria zake za uhalifu. Lakini ili kudhibiti hayo Mhe. Spika, ni ule udhibiti

wa hali ya pale inavyoendeshwa, sasa leo tukimuachia kila mtu anatoka na safari yake huko anatumia fursa zile anapita pale kwa sababu anaona kuna unafuu fulani tunaweza tukaja kujikuta tunajiingiza katika matatizo makubwa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hivi karibuni kumekamatwa watu wawili katika Kiwanja chetu cha Ndege, wametoka nje huko wamekuja kukamatwa na madawa ya kulevya Zanzibar. Kwa hivyo, leo tutakapoiachia hii *VIP* ikawa iko wazi kiasi kile kila mtu akishakuwa anamjua mtu fulani tu anatumia, huo sio utaratibu mzuri kabisa. Mhe. Spika, kwa hivyo nilikuwa naomba nimalizie hilo nimuombe Mhe. Waziri alitazame hili kwa ukali kabisa na asimamie kuona anadhibiti wa sehemu zile za *VIP*.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe naomba kuunga mkono hoja hii, na naunga mkono mswada huu wa marekebisho haya ambayo tunayapendekeza namtakia kila la heri Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri rafiki yangu wakafanye kazi ili tujenge Zanzibar mpya. Mhe. Spika, nakushukuru sana, ahsante.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi kidogo yakuweza kuzungumza jambo kwa jambo moja tu. Mhe. Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu wa sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar jambo ambalo tulikuwa tunalifikiria kwa muda mrefu na kwa kweli amefanya jambo zuri na amelileta kwa wakati mzuri.

Mhe. Spika, mimi namshukuru Mhe. Waziri kwa kupata nafasi hii kwa wakati huu tulionao kwa kutuletea shauri hilo, shauri ambalo ni zuri ambalo naamini kuwa Mhe. Waziri ataweka usimamizi mzuri katika viwanja vyetu na udhibiti mzuri ambao utakuwa mara nyingi mambo mengi yalikuwa yanajitokeza yaliyokuwa mabaya nafikiri wakati itakapokuwa tayari mambo yote hayo udhibiti utakuwa mzuri na fursa katika viwanja hivi zitapatikana vya kutosha. Pamoja na huduma nzuri ambayo tunategemea Mhe. Waziri ataziandaa.

Mhe. Spika, halikadhalika tunategemea kwamba kutakuwa na fursa kadha wa kadha katika suala zima la vifaa vya kurukia ndege na kutulia ndege. Kwa hivyo, hilo ni jambo zuri na tuna furahi na naamini kwamba mswada wake ni mzuri na una maelezo ya kutosha, hatuna haja ya kuuchangia sana.

Mhe. Spika, mimi katika mswada huu nilikuwa nina jambo moja tu nataka nimwambie Mhe. Waziri aweze kuliweka katika mswada wake. Unajua mahala ambapo patakuwa na watu wengi kama hapa katika Kiwanja cha Ndege patakuwa na wafanyakazi wengi ambao katika kifungu cha 6 (1) nimeeleza pale kutakuwa na Mwenyekiti, Mkurugenzi, Katibu Mkuu na WAjumbe kutakuwa na Bodi kamili ambayo itakuwa na watu kama hao watakaochaguliwa katika Bodi hiyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa patakuwa na wafanyakazi wengi naamini pahala panapokuwa na wafanyakazi wengi hapatakosa matatizo hata kama matatizo yanaweza kuibuka wakati wowote ningelimuomba Mhe. Waziri jambo ambalo ndio nataka nimwambie kwamba tuwe na *representative* mtu mmoja ambaye anapokea maoni kwa ajili ya wafanyakazi wake walioko pale. Haitowezekana kwamba katika eneo kama lile muhimu kwamba hapatakuwa na matatizo ya wafanyakazi naamini matatizo

yanaweza kutokezea wakati wowote kwa hiyo angalau awepo mtu mmoja kuweza kusikiliza maoni na ushauri au matatizo yoyote yatakayojitokeza ili yale maoni yao na ushauri wao na matatizo yao yaweze kupelekwa mahala. Kwa sababu katika mswada huu haikuonesha kwamba malalamiko yao na matatizo yao yatapokewa na mtu ili yafikishwe mahala panapostahiki.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi sikuwa na mengi nilikuwa nataka nitoe ushauri huo ili kumwambia Mhe. Waziri ni jambo la busara tukawa na mtu mmoja ambaye ataweza kupokea maoni na ushauri wa wafanyakazi. Kwa haya machache na mimi nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, na mimi kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwa wazima na tukafika hapa kujadili mambo ya taifa letu. Mhe. Spika, la pili naomba nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili niweze na mimi kuchangia kidogo kuhusu mswada huu.

Mhe. Spika, mswada huu kwa kweli ni mzuri na utasaidia sana katika kuimarisha viwanja vyetu ambavyo tumo katika jitihada ya kuviendeleza, na mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mgogoni napenda kuunga mkono mswada huu mia kwa mia. Hata hivyo, Mhe. Spika, na mimi nina maoni mawili matatu ambayo naamini yatazidi kusaidia kuimarisha mswada huu.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 193 naomba Mhe. Waziri kwamba katika zile *difinition* basi kuna neno hapa mkataba wa *CHICAGO* ile *spelling* ya *CHICAGO* iwekwe vizuri na sivyo kama vile ilivyo. Halafu katika ukurasa wa 195 hizi kazi za mamlaka ambazo zimetajwa katika kifungu Nam. 5 (1) imezungumzwa hapa kwamba kazi za mamlaka zitakuwa ni kuviendesha, kuvisimamia, kuvitunza na kuviendeleza viwanja vya ndege vya serikali katika Zanzibar.

Mhe. Spika, suala lilikuja katika utaratibu huu ambao tunakwenda hivi sasa je, tunazungumza kuwa na viwanja vya ndege vya Zanzibar vya serikali au hata viwanja vya binafsi. Mhe. Spika, nafikiri jibu ni wazi kwamba ni viwanja vya ndege vya serikali, lakini pamoja na viwanja vya ndege vya binafsi. Mhe. Spika, hapa naomba niseme mambo mawili kwamba sheria hizi ni mbili, kuna sheria hii ambayo inazungumzia Mamlaka ya Vwanja vya Ndege vya Zanzibar halafu kuna sheria ya pili ambayo itajadiliwa baadae inayozungumzia masharti ya utawala, udhibiti na uendeshaji. Kwa hivyo, hizi ni sheria mbili tofauti.

Mhe. Spika, katika sheria hii ya pili kifungu cha 5 na cha 6 kwa sababu hapa tunazungumzia udhibiti wa viwanja vya ndege, na hapa ndio inazungumzia katika kifungu cha 5 na cha 6 inazungumzia uanzishwaji wa viwanja vya ndege vya binafsi. Kwa hivyo, lile suala la kwamba hatukujali viwanja vya ndege vya binafsi linakuwa *taken care* katika sheria hii, kwa sababu hapa ni suala zima la udhibiti na uendeshaji wa viwanja vya ndege. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe watizame na watafautishe baina ya sheria hizi mbili ya uanzishwaji na ya udhibiti na uendeshaji. Hilo la kwanza.

Mhe. Spika, la pili kulikuwa na suala la kusema kwamba kwa nini sheria hizi mbili hatukuziunganisha pamoja? Mhe. Spika, wewe ni mtaalamu wa sheria ninaamini unajua kwamba kwa utaratibu wa siku hizi, kwa utaratibu wa karne ya leo,

unaambiwa kwamba sheria zote ni lazima ziwe rahisi na zinazofahamika. Ule utaratibu wa zamani kwa mfano kuandika *Will page* 20 haina *comma*, *fullstop*, *semicolon*, ule hautakiwi tena na kwa mantiki hiyo, utaalamu wa siku hizi unataka kwamba sheria zote zinazotungwa lazima ziwe ndogo na zinazofahamika.

Ukiandika sheria moja kwa mfano Mhe. Spika, kuna sheria inaitwa *Margin Shipping Act* ya Dar es Salam hata *Margin Shipping Act* ya kwetu ile ni sheria kubwa sana ina nafikiri vifungu 350. Sasa sheria ile kwa utaratibu wa siku hizi haitakiwi na kuna utaratibu kwamba sheria zile zirekebishwe ili kila *subject* inayohusiana mule iwe na sheria yake kwa *easy of reference* wanaita, yaani hata ukimpa mwanasheria na sheria si lazima isomwe na mwanasheria, sheria ni ya watu wote wale watu wanatakiwa wafahamu na ndio maana sisi Zanzibar tukaanza kutekeleza utaratibu huo ambao sasa unakubalika ulimwengu mzima.

Kwa maana hiyo, si vizuri kwa mfano, sheria za ardhi kama alivyozungumza mjumbe sheria saba zile ukazifanya zote ni sheria moja kwa kweli itakuw ani kubwa sana, haifahamiki na hao walengwa ambao si wanasheria wengi watakua ni wananchi wa kawaida kuwa na sheria moja yenye vifungu 500 inayozungumzia ardhi tu ni kumpotosha zaidi kuliko kumrekebisha.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hii nasema kwa sababu serikali imeona ni vizuri katika mambo haya mawili yayatenganishe moja liwe ni suala linalozungumzia kama nilivyosema Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na moja linalozungumzia suala la Utawala wa Viwanja vya Ndege.

Mhe. Spika, hiyo ndio madhumuni kubwa ya kwa nini tukazibagua sheria mbili hizi kutokana na utaratibu uliopo kisheria katika ulimwengu hivi sasa. Mhe. Spika, Zanzibar haiku peke yake, hatuko kisiwa tuko pamoja na dunia nzima. Hilo ni moja.

Lakini la pili, ambalo napenda nilizungumze Mhe. Spika, ni suala zima la kifungu cha 24 ambacho kimezungumzwa na Mhe. Mjumbe pamoja na kifungu cha 26.

Mhe. Spika, katika utaratibu ule ule wa kuandika sheria kuna vifungu vya adhabu na vifungu hivyo kuna vifungu vya aina nyingi, lakini mimi nitazungumzia vifungu viwili. Kuna kifungu ambacho kinaitwa au kinachozungumzia *Minimum Sentencing Act*. Hii unatakiwa kwamba unapokuwa na kosa fulani kuna baadhi ya makosa ambayo yamewekwa katika adhabu hii ya *Minimum Sentencing Act*, yaani unatakiwa uelezee adhabu ya chini kabisa, sasa ile adhabu ya juu unamuachia hakimu au jaji katika *wisdom* yake. Sasa kifungu cha 24 ndicho kilichotumika kwa utaalamu huo, kwamba hii ameelezea *Minimum Sentence* inayotakiwa.

Lakini katika kifungu cha 26 kuna suala la *General Provisions*, yaani adhabu ya ujumla. Sasa Mhe. Spika, adhabu ya ujumla unaielezea tu, kwamba utatoa hiki kwa *penalty* hii anayopewa. Kwa hivyo, kifungu cha 24 na 26 hakihusiani kwa mantiki hiyo, kile cha mwanzo ni Minimum ambapo Hakimu anaweza akenda katika adhabu yoyote anayoona inafaa, lakini hii ya *General* hapa Hakimu au Jaji hawezi kwenda isipokuwa kwa ile *penalty* ambayo amepewa. Hilo ni jengine ambalo Mhe. Spika, ningelipenda nilizungumze.

Mhe. Spika, katika mswada huu kuna suala zima lililozungumzwa la kifungu 10(2)(a). Katika kifungu hiki kinazungumzia uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na hapa tunasema kwamba kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlka ambaye atateuliwa na Rais na mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa atakuwa: (a) imewekwa shahada, amehitimu kutoka Chuo Kikuu kinachotambulika au katika chuo kinacholingana na hicho. Hapa haina maana kwamba ni vyuo vikuu vinavyomea kama alivyosema Mjumbe.

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe mtakubaliana na mimi kwamba kuna fani nyengine hazipatikani katika chuo kikuu. Kwa mfano, fani ya u-*pilot*, hakuna chuo kikuu kinachotoa *degree* ya *pilot. Pilot* hawa nakusudia ni *pilot* wa ndege na meli. Kuna vyuo maalum ambavyo utaalamu huu unapatikana. Sasa vyuo kama hivi Mhe. Spika, ndivyo vilivyokuwa *referred* hapa, yaani unaweza ukawa na elimu ya chuo kikuu, lakini pengine unaweza ukawa na elimu nzuri, kubwa inayotambulika lakini umepata katika vyuo ambavyo vinalingana na hivyo.

Kwa hivyo hapa ndio ilivyokusudiwa Mhe. Spika. Kwa hivyo, kifungu cha 10(1)(2)(a) Mhe. Spika, mimi nahisi ni sawa sawa na hakina matatizo yoyote. Mhe. Spika, kifungu cha 10(2)(a) mimi napendekeza kibakie hivyo hivyo ili kiwe kinakidhi ile haja ambayo inatakiwa.

Kuna wajumbe ambao walizungumzia suala la *Separation of Powers* na wakasema kwamba ni vyema kuwa Wajumbe wa Bodi wawe hawamo yaani watunga sheria akimaanisha kwamba Wawakilishi wawe hawamo katika bodi hizi. Kwa sababu hiyo haitakuwa *separation of power* kama kifungu cha (5)(a) cha Katiba alivyokinukuu.

Mhe. Spika, napenda niseme tu kwamba, ni kweli tuna *concept* ya ku *separation of powers*, lakini *concept* hii Mhe. Mjumbe atakubaliana na mimi kwamba kuna baadhi ya nchi hakuna hasa ile wanayoita *true separation of powers* na Tanzania na Zanzibar ni moja miongoni mwao, vyenginevyo tukenda katika *strict construction* ya *separation of powers* Mhe. Spika, hata mawaziri itakuwa wasiwemo katika Baraza hili. Kwa hivyo, hiyo kwa utaratibu huu nafikiri hapa bado haijakuwa pahala ambapo tungeliweza kujadili suala hili. Hili ni suala la *National Policy* mpaka hapo *policy* itakapokubalika kwamba tuwe na *true separation of powers* kama Marekani ambapo Waziri haingii katika Bunge au Hakimu na Jaji hawaingii katika Bunge kama Uingereza, hapo ndio tunaweza tukakubaliana na mapendekezo ya Mhe. Mjumbe.

Mhe. Spika, la mwisho ambalo ningelipenda niseme liko katika kifungu cha 28, kifungu hicho ni Uhamisho wa Wafanyakazi. Kinasema kwamba, ‘Mara baada ya kuanza kutumika kwa sheria hii, mfanyakazi yoyote wa idara kabla ya kutungwa sheria hii ambaye anahitajika anaweza kuhamishwa katika utumishi wa Mamlaka kwa maelezo na masharti kama itakavyoamuliwa na Mamlaka’. Lakini kifungu cha 28 (2) kinasema kwamba, “Mfanyakazi aliyehamishwa chini ya kifungu cha kwanza cha kifungu hiki atafanya kazi chini ya mamlaka kwa kiwango kile kile cha mshahara na maslahi mengine kama alivyokuwa akipokea kabla hajawa mfanyakazi wa Mamlaka”. Hapa sasa ndio kwenye matatizo, isipokuwa itakavyoamuliwa vyenginevyo na Mamlaka.

Sasa hii hata ukisoma ya Kingereza Mhe. Spika, ina matatizo kidogo kwa sababu mfanyakazi anayehamishwa pahala popote kisheria, sheria ya Utumishi ambayo

tumeipitisha hatopunguziwa mshahara wake. Sasa hapa tukiweka *blanket* hivi kwamba isipokuwa itakavyoamuliwa vyenginevyo na Mamlaka mimi nafikiri hapa tuongeze sentensi kwamba, kwa vyovyote vile mshahara au maslahi yake hayatopunguzwa kwa mujibu wa sheria ile ambayo tumeitunga na tumeikubali hapa. Baada ya kufanya hivyo kwa hivyo, hata mfanyakazi akihamishwa kule atalindwa kwamba ule mshahara wake aliokwendanao kule atakuwa nao na Mamlaka haiwezi kupunguza lakini inaweza ikamuongezea.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, na mimi nakubaliana na mswada huu na naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu kwa mswada wake huu wa Uanzishwaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, kazi zake na mambo mengine yanayohusiana na hayo.
Mhe. Spika, kwa kweli mimi niseme mswada umekuja wakati mzuri na umekuja kwa lengo kwamba sasa kwa kweli viwanja vyetu vimeanza kufanya kazi za ziada kwa kuhudumia abiria. Kwa hivyo, kwa vilivyo hivi sasa vinahitaji usimamizi mzuri, uangalizi mzuri, kushughulikiwa zaidi, na haya yote mwenyewe Mhe. Waziri kavieleza vizuri sana, naomba kunukuu kifungu nambari tano kwenye kazi na uwezo wa mamlaka.

Kifungu Nam. 5(a) kinasema kwamba:

> "Kuviendesha, kuvisimamia, kuvitunza na kuviendeleza viwanja vya ndege vya serikali katika Zanzibar".

Hili ni suala la msingi sana Mhe. Spika, na nafikiri abiria wote sasa wakisikia au wakiona mabadiliko haya watafurahia. Kwa sababu wanapolipa pesa zao za *airport charge* kwa hivyo, huduma wanazozipata ni nzuri. Lakini kwa udogo wa viwanja vyetu ulivyo kwa kweli nafasi haipo ya kutosha. Sasa ndio tumeamua tujenge viwanja vyengine lakini pia tuzifanye huduma zetu ziwe bora zaidi. Kwa hivyo, mimi hili nalipongeza sana wazo la serikali kupitia wizara la kuviendeleza viwanja vyetu.

Mhe. Spika, katika kuvitanua viwanja vyetu labda nianze kusema kwamba kwa uwanja wetu huu wa Abeid Amani Karume sote tunakumbuka ulivyokuwa hapo zamani. Sisi tokea tulipokuwa wadogo mpaka leo tunashukuru Mamlaka ya Uwanja wa Ndege zile amala za zamani wameziacha, ilikuwa gari ya kwetu *Route Nam. 7* ile inakata katikati ya uwanja pale, linafungwa geti manzuiliwa jamani msipite ndege inaruka, ndege inatua, wakati huo na Dakota linakuja. Natoka skuli tunakwenda kuangalia Dakota moja tu kwa siku saa nane, nakumbuka kabisa, saa saba kasorobo inatua, inateremsha watu halafu saa nane linatweka linaruka moja tu kwa siku. Alhamdulillah uwanja ukatanuliwa ukasogea kidogo na mpaka leo alama iliposogea kidogo zipo zile, hatimaye ukaja tena pale tukawa tunazunguka kama *ring road*.

Mhe. Spika, leo tumeitanua kabisa kuna njia ya barabara maarufu kule Mbuyu Mnene au Sarayevo. Majirani wazuri tu wapo nimewapata kina Mhe. Zahra Ali Hamad ndio wameweka mji mpya kule. Sasa hii inaonesha vipi viwanja Mhe. Spika, tulivyovikuza na hii yote tunapongeza juhudi za wizara na serikali katika kuvitanua viwanja vile.

Sasa mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri katika mswada ameelezea mambo matatu yanayohusiana na majirani zake majriani wa uwanja yaani wananchi wa vijiji vya Kisauni, Chakani, Mitondooni na Kiembesamaki. Hawa ndio majirani wa Uwanja wa Ndege kwa kila upande.

Sasa Mhe. Waziri amesema atajitahidi kwenye kifungu (f) kuhakikisha usalama, kusimamia viwango vya usalama ndani ya Uwanja wa Ndege na maeneo ya karibu ya Uwanja wa Ndege ndio vijiji hivi nilivyovitaja.

Pili kwenye kifungu (h) anasema kuhifadhi mazingira ndani ya mipaka ya Uwanja wa Ndege na maeneo ya karibu ya Uwanja wa Ndege. Bado anasisitiza umuhimu wa majirani wa uwanja wa ndege.

Kifungu cha (j) kushirikiana na taasisi nyengine yoyote ya serikali ndani ya mipaka ya viwanja vya ndege na maeneo ya karibu na Uwanja wa Ndege. Hii inaonesha wazi kwamba Mhe. Waziri pamoja na wizara wanajali zaidi kuishi vizuri na majirani zao wa mipaka iliyoko katika vijiji vile. Kwa kweli tunawapongeza sana majirani hawa kwa sababu ardhi zile wamekuwa wakiishi miaka na miaka, wamezaliana, wamejenga, lakini serikali kila ikitaka kutanua ikiwafuata wanakubali wanalipwa fidia wanaondoka na wanasogea. Kwa hivyo, tunawashukuru sana wananchi wa vijiji hivi.

Hivi juzi tu Mhe.Waziri kabla hajaanza kujenga ukuta wake amewapa fidia zao nzuri kabisa na wamefurahishwa kabisa na hatua iliyochukuliwa na serikali. Bado wako wawili watatu tu, lakini tunafuatilia ipasavyo. Sasa mimi nataka kupongeza sana hivi kwamba Mhe. Waziri atavyojali kukaa na hawa wananchi waliokuwa ni majirani zao na hasa kusema kwamba atasimamia uendeshaji wa uwanja akizingatia maeneo ya mipaka.

Lakini nataka kusema kwamba, wananchi wale kabla ya ukuta kuzungushwa na hasa kwenye Kiwanja cha Ndege hichi cha Amani Abeid Karume nyuimba nyingi zilitiwa X na ramani zikachorwa kwamba wasisogee karibu na Uwanja wa Ndege. Sasa pale waliingia hofu kwamba lini hatima yao wataijua, lakini tunashukuru wizara na serikali hivi sasa tayari ukuta umeshajengwa na wameshajijua kwamba wako nje ya maeneo ya Uwanja wa Ndege.

Lakini namuomba Mhe. Waziri atapofanya majumuisho atuhakikishie tu hawa wananchi kwamba wasiwe na wasiwasi sasa kama wana mashamba yao basi walime, kama wana nyumba zao walime, yaani ile mipaka sasa hivi iainishwe zaidi wafahamu kwamba Uwanja wa Ndege Mamlaka yake unaishia wapi. Nafikiri hili litasaidia sana ule ushirikiano niliousema wa awali wa wananchi hawa na pia wale wananchi wajue kwamba mipaka ya Uwanja wa Ndege imeishia wapi na sisi tuko na mashirikiano yawe karibu zaidi.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mimi sina mengi isipokuwa napongeza sana hili suala na naamini litasaidai sana kuviendesha viwanja vyetu vipate ufanisi na wananchi wetu waliopo majirani nao waishi vizuri na mipaka ya uwanja waiheshimu na waifuatilie kwa karibu zaidi.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi hawa na wengine wa Jimbo la Dimani naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na mimi naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia naomba niungane na wenzangu kumshukuru Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao kwa kuja na fikra hii ya kuuleta mfumo mpya wa usimamizi wa moja katika maeneo muhimu katika nchi yetu. Maeneo muhimu kiuchumi lakini pia maeneo muhimu kiusalama wa nchi yetu vile vile.

Lakini la pili naomba niungane na wenzangu pia kwa kuishukuru sana kamati. Marekebisho aliyokujanayo kwanza yametusaidia sisi waandishi wa sheria kuwa makini zaidi, lakini na pili wamesaidia kuufanya mswada huu uwe mzuri zaidi.

Mhe. Spika, marekebisho ambayo kamati wameyapendekeza yale ya msingi pamoja na yale ya kiuandishi mimi kimsingi nakubaliana nayo au nayaunga mkono, ni vyema tukayaangalia wapi pa kuyaimarisha kidogo tu. Kwa hivyo nikianza kwenye taarifa ya kamati waliopendekeza marekebisho nadhani kuna baadhi ya mambo tu ambayo ni vyema kuyaangalia vizuri. Nadhani wakati wa kuandika ile taarifa ya kamati kwa mfano, tukianza na Mapendekezo yao kwenye kifungu cha 9 cha taarifa ya kamati ukurasa wa pili kwenye ufafanuzi wa neno ‘usalama’ maneno ya ‘uingiliaji’ yanafutwa na badala yake kuingizwa neno ‘vilivyo’.

Lakini nadhani ukiangalia mswada walilokusudia hasa ni hali ya usalama sio usalama, yaani katika tafsiri ya hali ya usalama ndio yanakuja yale marekebisho yao. Marekebisho yao waliyopendekeza nakubaliana nayo ni sawa, lakini nadhani kwamba yanafaa zaidi au walikusudia hata wao wenyewe kwamba yaingie katika tafsiri ya neno hali ya usalama.

Eneo la pili kwenye taarifa ya kamati ni kwenye kifungu cha 26 nadhani. Samahani Mhe. Spika, kwanza nianze na mapendekezo yao kwenye kifungu cha 11 kifungu kidogo cha 1(c). ukiangalia wao wamependekeza kwamba kiongezwe kifungu cha 11 kifungu kidogo cha (b), lakini kama tutaongeza kwa mujibu wa mapendekezo ya kamati ina maana kifungu cha 11(c) kitasomeka kama ifuatavyo:-

Tunamzungumzia hapa Mkurugenzi Mkuu, tukija kwenye (c) ‘Mkurugenzi Mkuu atatekeleza wajibu mwengine ambao atapewa na waziri au kama itakavyoona bodi inafaa’. Lakini (d) kinachopendekezwa ni kwamba atatekeleza wajibu mwengine ambao atapewa na waziri kama atakavyoona inafaa. Sasa ukiangalia kama ni maneno tariban ni hayo kwa hayo, tofauti yake ni kwamba hii nyengine imeondoa bodi tu, lakini hiki kinachopendekezwa ni yale yale ambayo yatapewa na waziri.

Sasa mimi nilifikiria kama kuna marekebisho kwenye kifungu hicho cha (c) tukifanyie hicho, nadhani hiki cha (d) kitakuwa hakina haja kukiongeza kwa sababu kitakuwa kinazungumzia neno hilo hilo. Inawezekana kamati walikuwa na mawazo mazuri yak u-*improve* hiki kifungu lakini namna kilivyowekwa kinaleta utata kidogo na cha ziada lakini kinazungumzia dhana moja ya Mkurugenzi Mkuu kuweza kufanya majukumu mengine ambayo ataelekezwa na waziri. Lakini na hapa kwenye (c) kimeongezeka kwamba na bodi nayo kama itakavyoelekeza vile vile labda hakikuandikwa vizuri. Mimi nadhani hicho tukifanyie marekebisho.

Jengine kwenye taarifa ya kamati Mhe. Spika, ni kwenye kifungu cha 26 ambacho kinahusu kifungu cha 19(1). Kwenye kifungu hiki wanapendekeza kwamba neno 'fedha' lifutwe na ibaki rasilimali. Lakini nadhani kifungu cha 19 kinazungumzia fedha na mali za mamlaka. Sasa tuna wasiwasi tukifuta zile fedha kitakuwa kama kwamba tunachozungumzia ni kitu chengine tuofauti na maelezo ya kifungu, kwa sababu sasa kitasomeka rasilimali za mamlaka zitakuwa ni pamoja na ada za mikataba na mirahaba, malipo yaliyokusanywa kutokana na mambo mengine ambayo yote yanahusiana na *funds*.

Sasa mimi nilidhani kwamba kingebaki vile vile fedha na rasilimali, lakini bahati mbaya hatukuzungumzia zile rasilimali nyengine na nilikuwa na mawazo kwamba labda tungeongeza kifungu (f) kikasomeka 'Mali na rasilimali zitakazohamishiwa katika mamlaka baada ya kuanzishwa na mali nyengine zitakazonunuliwa au kupatikana wakati wowote kwa ajili ya mamlaka'. Sasa hiki kingekuwa kime-*cover* fedha pamoja na rasilimali. Nadhani tungezungumzia zaidi fedha ile rasilimali tumeiacha, tukiongeza kifungu hiki kikawa kama ndio (f) kama tutakubaliana mimi nadhani kitakuwa kimekaa vizuri bila ya kufuta neno 'fedha'. Nina wasi wasi tukifuta neno hilo hiki kifungu kitakuwa kinazungumzia kitu chengine *asset* za mamlka wakati *asset* na fedha ni vitu ambavyo vinafanana lakini ni vitu ambavyo tofauti kidogo.

Sasa kwa vile imekusudiwa fedha na rasilimali tungezitaja fedha tukazitaja na hizo rasilimali. Lakini vyenginevyo sijui Mhe. Waziri atakapokuja atasema vipi katika mapendekezo ya kamati, lakini mimi kimsingi kwenye taarifa hii ya kamati nilikuwa nina mambo hayo ambayo nadhani tukiyaimarisha yatasaidia kuimarisha mswada wetu.

Nikiondoka hapo labda nije kwenye hoja ambazo zimezungumzwa na Wajumbe mbali mbali. Mhe. Spika, labda nikianza na ile hoja aliyoizungumza Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa suala la udhibiti wa madawa ya kulevya. Hii Sheria ya Mamlaka inazungumzia kazi zao zaidi na operesheni zao. Mamlaka ni msimamizi wa sheria nyengine zote za nchi ambazo zitahusiana na viwanja vya ndege. Kwa hivyo, kama kuna Sheria ya Madawa ya Kulevya ambayo ipo na taratibu zake za udhibiti kwa upande wa *entry point* yaani upande wa uwanja wa ndege, basi itakuwa ni wajibu wa mamlaka kuisimamia.

Sasa kama hilo limeelezwa, kama hilo halikuelezwa lakini huo ni wajibu wao na pale wanasimamia sio kama mamlaka lakini zipo taasisi mbali mbali Polisi, Vyombo vya Usalama. Moja ambalo tutakuja kuliona pengine tutakapokuja kwenye Sheria ya Viwanja vya Ndege tutaona taratibu ambazo zinachukuliwa kuimarisha usalama katika viwanja vya ndege.

Kwa hivyo, nadhani hilo linasimamiwa na sheria zinazohusika na mamlaka inawajibika kuzisimamia kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa ndani ya sheria hizo ambazo zinahusika. Wao wanachotakiwa ni kuandaa utaratibu tu wa usimamizi ambao umeelezwa katika vifungu mbali mbali na tutakapoona kwenye Sheria ya Viwanja vya Ndege ambao nao pia wanahusika basi tutaona jinsi gani ambavyo wametakiwa kujipanga.

Mhe. Spika, suala jengine Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa alikuwa na wasi wasi kwamba neno *aerodrome* kwenye kamusi au *dictionary* kama alivyosema ni kwamba lina maana ya kiwanja kidogo cha ndege na sisi tunakusudia kuendeleza viwanja vyetu viwe vikubwa kama vilivyo sasa, vimetoka kule alikoeleza Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame mpaka vimekuwa tunashindana na wengine katika Afrika Mashariki.
Lakini naomba nimtoe wasi wasi Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa kwamba kwenye sheria neno linakuwa na maana ile ambayo imetafsiriwa kwenye sheria. Linawezekana likawa katika matumizi ya kawaida lina maana nyengine yaani tunasema *literal translation*, lakini ukilipa tafsiri kwenye sheria linakuwa na maana ile ambayo imetafsiriwa kwenye sheria.

Kwa hivyo, chochote ambacho kimeelezwa na humu kwenye sheria yetu imetafsiri nini maana ya uwanja wa ndege. Katika hiyo tafsiri inajumuisha kiwanja hicho anachosema yeye kidogo na viwanja vikubwa kabisa tutakapopata uwezo wa kuvisimamia. Hili ni jambo la kawaida kwa mfano kwenye sheria tunasema tunatumia neno *'he'* lakini linajumuisha na *'she'*. Yaani kwa mujibu wa sheria ni kama wanawake hawa-*exist*, ni mwanamme ndio huyo huyo mwanamke.

Mhe. Spika, pia kuna mifano ya sheria nyengine kwa mfano Sheria ya Karafuu kwa mujibu wa sheria karafuu inajumuisha na makonyo, inajumuisha na matende. Lakini Mswahili gani utakwenda kumwambia kwamba makonyo ni karafuu mkakubaliana, hamuwezi kuelewana hata siku moja.

Mhe. Spika, naomba nimpe hadithi ndogo tu Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa kwamba jinsi sheria inavyoweza ikawa katika tafsiri kuna watu katika chama chao walikubaliana kwamba mbwa hawaruhusiwi kuingia ndani marufuku kabisa. Lakini wakagundua kuna wenzao wengine hawaoni na inabidi wakapata mwanachama mpya haoni ikabidi lazima yeye aongozwe na mbwa wake aingie nae ndani.

Kwa hivyo, wakarudi kwenye sheria yao wakairekebisha wakasema kwa madhumuni ya sheria hii mbwa anayeongoza mwanachama ambaye hawezi kuona huyo atakuwa paka. Kwa maana hiyo, paka hawakatazwi kuingia mle ndani, kwa hivyo akaweza kuingia huyu bwana na mbwa wake vile vile. Mhe. Spika, hii ndio kazi ya tafsiri inavyofanyika kwenye sheria na madhumuni yake ni kuipa ile tafsiri ambayo ninayoikusudia.

Mhe. Spika, labda nije kwenye hoja ambayo aliizungumza Mhe. Hija Hassan Hija, pia aliizungumza Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Yeye alikuwa na wasi wasi kwamba labda sheria hii inaweza ikagongana na sheria au tusije tukagongana na sheria ile ya *Civil Aviation*. Mhe. Spika, labda nizungumzie hapa hapa Mhe. Jussa pale aliposema kwamba kwa nini tunasema kwamba Mkurugenzi Mkuu atasimamia sheria ile ya *Civil Aviation* inayohusiana na uendeshaji wa viwanja vya ndege. Nae akataka kwamba labda tuwe na sheria yetu moja kwa moja kwa sababu tayari Sheria ya Bandari na Sheria ya Takwimu tumezitunga hapa na tunazitumia kimuungano.

Mhe. Spika, tunasema kwamba kwa mujibu wa sheria wakati mwengine kunapokuwa hakuna tafsiri ya wazi basi *circumstances* zinaleta tafsiri, *context* vile vile inaleta tafsiri. Toka ilipotungwa Katiba ya Muungano Bandari haikuwahi kufanywa kimuungano na Takwimu vile vile haikuwahi kufanywa kimuungano. Ingawa

walipotunga wenzetu Sheria ya Bandari *Tanzania Harbours Authority* na bandari zetu walizitia katika Mamlaka ambayo wataziendesha vile vile lakini hawakuwahi kufanya hivyo.

Suala likaja je, Bandari kwa tafsiri ya Sheria ya Muungano au Katiba ya Muungano ni *infrastructure* ama ni *regulation* ya Bandari. Maana yake kama sasa hivi ilivyo simu. Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe yeyote akiwa na pesa zake anaweza akaanzisha kampuni ya simu na akapata leseni. Chombo cha udhibiti tu ndio kimoja *Tanzania Communication Regulatory Authority* lakini biashara yenyewe ya simu sio ya Muungano. Lakini tulivyoanza ilikuwa mpaka simu yenyewe ni ya Muungano, baadae wala hatukurekebisha katiba aaa imekuja tu wenyewe kutokana na mabadiliko tukajikuta kwamba imebakia ya Muungano, ni *regulations* tu lakini *business* sio suala la Muungano, wala sio suala la serikali hasa.

Mhe. Spika, Bandari ni hivyo hivyo kwamba kwa vile tulikuwa kwa muda mrefu hilo halikufanyika mpaka tukafika pahala tukasema aaa kwa mazingira ya sasa inavyoonesha na kwa mazoea tuliyojijengea na kwa hali yenyewe ilivyo, haiwezekani kwamba Bandari ya Zanzibar ije iendeshwe na Serikali ya Muungano.

Kwa hivyo, tafsiri na kwa sababu hakuna tafsiri ambayo iko wazi tunaposema Bandari ni suala la Muungano ndio maana tukasema kwamba inaonesha labda ni hii *regulation*. Kwa hivyo, uendeshaji basi wacha tuutungie sheria na tuusimamie. Sasa sisi tume-*take advantages* ya kutokuwepo na *clear position* ya suala la tafsiri ya Bandari kama ni suala la Muungano. Ndio maana hatukumshauri mtu wala hatukwenda kwa mtu katika hilo lakini pia hata suala la Takwimu vile vile linaingia hapo hapo. Mhe. Spika, kwanza labda niliweke sawa hilo.

Mhe. Spika, la pili ni suala la mgongano wa sheria hii ya *Civil Aviation*. *Civil Aviation* bahati nzuri ina mambo mengi, *Civil Aviation* sheria inachoweka ni *standards* tu kwamba ukiwa na ndege yako iwe na *standard* fulani ili iruhusiwe kuruka. Hata *pilot* ili uruhusiwe uwe na vigezo fulani. Hata uwanja wa ndege nao una vigezo ambavyo vinatakiwa vitimizwe na vifuatwe.

Kwa hivyo, hili bahati nzuri sheria ya *Civil Aviation essential* iko katika *annexes* za ule mkataba wenyewe wa kimataifa wa *Civil Aviation.* Kwa hivyo, hata nchi wala haipati shida ya kutunga sheria nyengine inachochukua ni kuzi-*apply* zile *annexes.* Wewe unachokizungumza chochote kwenye masuala ya uwanja wa ndege basi kuna regulation zake za *Civil Aviation.*

Mhe. Spika, tunachosema hii mamlaka kazi yake itazisimamia hizo *standard* za *Civil Aviation* zilizowekwa kuhusiana na uwanja wa ndege basi. Kwa hivyo, hapa hatukaribishi kuvamiwa wala hatumvamii mtu, hatukaribishi kuingiliwa wala hatumuingilii mtu katika mamlaka yake katika hili. Sasa nilikuwa naomba tu huo wasi wasi labda tungeuondoa.

Mhe. Spika, hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu mimi nashukuru labda hili ameshalijibu Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria suala la kuwa na sheria moja au mbili labda ningeongezea jambo moja tu dogo. Mhe. Spika, hizi sheria ni mbili tofauti. Wakati mwengine kinachotupa shida kukiona ni kwamba ukizungumza dereva na gari wanasema hata gari ukikaa nayo muda mrefu labda mnafanana. Sasa kuna uhusiano

mkubwa baina ya dereva na gari lakini mamlaka ni dereva kwa hivyo tumemuwekea utaratibu wake. Ndio hii sheria inaweka utaratibu ataendeshaje, atakuwa na uwezo gani, yaani ni kuweka *institutional framework* ya hiki chombo ambacho *essential* kitaendesha hizi *airport* za serikali. Hii mamlaka hasa kimsingi kazi yake ni chombo cha kuendesha *airport* za serikali.

Mhe. Spika, Sheria ya *Airport* au *Aerodrome* ni sheria ya ku-*regulate* hizo *airport* zenyewe za serikali ziendeshweje. Maana yake ni sawa sawa na vile tungekuwa labda na sheria ya ku-*regulate* masuala ya simu lakini ukawa na kampuni ya simu ya serikali. Sasa kampuni ya simu ungeweza kuianzisha ama kwa sheria ya makampuni, ama ukaianzisha kama ni *agency,* ama ukaianzisha kama ni idara, lakini inajulikana kwamba hii inafanya kazi ya kuendesha biashara ya simu za serikali.

Lakini bado udhibiti na usimamizi wa simu una sheria yake ambayo ina-*apply* kwa kila mtu, iwe ni wa serikali, asiwe wa serikali. Sasa Sheria ya *Aerodrome* ni *regulatory law*, tatizo tulilonalo ambalo ni *a little be trick* ni kwamba kwa sasa hivi hatuna chombo peke yake cha kusema tunaanzisha *regulatory authority* wa kusimamia ile sheria. Ndio maana kwa kiasi fulani kuna mambo ambayo Waziri atayasimamia chini ya sheria ile lakini akisaidiwa na Mkurugenzi Mkuu kama ni *technical advisor.* Tutaona kule kuna kamati ya wataalam ambayo inamsaidia Waziri katika kusimamia baadhi ya mambo.

Lakini tungekuwa tunataka kuitunisha serikali tungekuwa na chombo tutakapofika wakati pengine *utility industry* tunataka kui-*regulate* pengine tutakuwa na *EWURA* labda ya Zanzibar ama sijui *SUMATRA* na *SUMATRA* tunayo sijui tunaiitaje hapa kwetu. Lakini tunapokuwa na chombo sasa cha kusimamia pamoja na hizi *airport* basi tunaweza tukasema kwamba yale mamlaka ya kusimamia yatapelekwa huko na yataondoka kwa kiasi fulani. Lakini hizi ni sheria mbili tofauti na madhumuni yake ni kuzungumzia vitu viwili tofauti, moja ni *regulatory* na nyengine ni *kind of operator*, yaani ni msimamizi wa ile biashara yenyewe.

Kwa hivyo, tuliona ilipendeza kwamba tuwe na sheria hizo mbili tofauti ili kuyaweka haya majukumu isije ikaonekana kwamba hii sheria ni ya mamlaka. Hii sheria ni ya serikali kuweka udhibiti na usimamizi wa viwanja vya ndege popote itakavyokuwa na tutaona kwenye ile sheria ina-*include* pia. Kesho kutwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu Mwenyezi Mungu amjaalie anaweza akapata fedha akaamua ajenge nyumba *man shall* ina na *helipad* kule juu sehemu ya kutulia *helicopter* ili asipate shida kuja chini kupanda kule kule juu watu wanafanya siku hizi.

Sasa ile Sheria ya *Aerodrome* pia ina-*regulate* mambo kama haya kwamba aje tu aombe kibali apewe na aweze kuitumia *time* yake hiyo. Kwa hivyo, hii ni *regulatory* na ina *aspect* nyingi zaidi ya hii *operation* tu kama ilivyozungumzwa katika sheria na tuliona isingependeza kuziweka katika sheria moja. Kwa hivyo, nadhani nimejaribu kujibu ule wasi wasi wake Mhe. Ismail Jussa Ladhu wa mfumko wa sheria. Mimi niliipenda hiyo *terminology* naomba niikope kutoka kwake.

Mhe. Spika, jengine Mhe. Ismail Jussa Ladhu alizungumza suala la *consistency* nakubaliana nae na mambo mengine. Lakini jengine alizungumzia nadhani Mhe. Waziri alijibu kuhusu lile suala la chuo kinachofanana nacho. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alilieleza vizuri labda mimi niongeze mfano tu kwamba tuna kada ya uhasibu,

kada ya uhasibu unaweza kuwa na *degree* lakini bado hujatambulika mpaka uwe na *CPA* ambayo huipati chuo kikuu unaipata katika *professional bodies* ambazo zinatoa.

Sasa leo ukisema kwamba mhasibu lazima awe na *degree* mwenye *CPA* hafai dunia haitokuelewa. Kwa hivyo, ndio maana ikawekwa hiyo ni kwa nia njema na kwa kutambua kwamba kada hii ni moja ambayo watu wengi hawakwenda chuo kikuu, lakini ni mahiri kwa sababu wamepita zile *training* ambazo zinakubalika na kwa utaratibu ule ambao *profession* hii imeuweka kwa ajili ya kuwa-*train* watu.

Mhe. Spika, hoja nyengine ni suala la adhabu nadhani limezungumzwa. Lakini nadhani pengine tukiliangalia vizuri mimi nimeielewa *concern* ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba tumeweka *minimum sentence* ya faini ya laki tano ni sawa, lakini ile *minimum sentence* ya kifungo kama vile mbona hailingani.

Mhe. Spika, maana yake kwenye hili mimi nataka nikubaliane na wote wawili. Alichosema Mhe. Waziri hapa ile dhana ni sawa, lakini nadhani ilikuwa kutoku-*zero down, specifical* nadhani alichouzungumza Mhe. Jussa ni ile *consistency* kwamba *minimum sentence* ya hapa tumesema ya faini ni laki tano, lakini mbona ya kifungo ni miaka miwili.

Mhe. Spika, hapa mimi nakubaliana nae kwamba ni kweli inaonesha tatizo letu hatujakuwa sasa hivi na *Penal Policy* au *Sentencing Policy,* wenzetu wanayo na nadhani ni kitu kizuri kitatusaidia mambo kama haya kuwa na kigezo. Maana yake sasa hivi tuko *very subjective* kuliko kuwa *objective*.

Sasa hili mimi ningesema labda kama *minimum sentence* ni laki tano ya faini kifungo basi kingekuwa labda isiyopungua mwaka mmoja au isiyopungua miezi sita nadhani ndio itakuwa inalingana. Kwa hivyo, mimi ningependekeza labda tukubaliane kwamba *minimum sentence* ya faini iwe ni laki tano, *minimum sentence* ya kifungo kiwe ni miezi sita naona italeta *logic*. Kwa sababu ikiwa ni *minimum sentence* ina maana hakimu ataanza pale lakini anao uwezo wa kumfunga mtu muda kwa kulingana na kosa lenyewe na mazingira yenyewe ambayo yatakuwepo.

Mhe. Spika, jengine alilozungumzia Mhe. Ismail Jussa Ladhu ni kuhusu kifungu cha 11 (c) nadhani nimelijibu. Labda kwa kumuongezea mfano tunayo Polisi ni Jamhuri ya Muungano lakini wanapokuja Zanzibar wanasimamia sheria za Zanzibar. Kwa hivyo, sioni kama hilo ni tatizo.

Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa sababu yale ambayo alikuwa ameya-*raise* Mhe. Ismail Jussa Ladhu labda moja tu katika yale maangalizo yake kuhusu *composition* ya bodi. Mhe. Spika, Mhe. Jussa alisema kwamba si vizuri kuingiza wanasiasa kwenye bodi hoja aliyoitumia ni kwa *separation of powers.* Ndio maana Mhe. Waziri nadhani alijibu vile alivyojibu kwamba ukitazama hata katiba yetu kwenye *separation of powers* haiko imechanganywa. Sisi hatujawa na *policy* ya *treaty separation of powers.*

Sasa ukitumia *policy* ya *separation of powers* mimi nadhani *policy* yetu iko *clear* kwamba *so far* hatujakuwa na *clear demarcation* wa huku anaingia huku na wa huku anaingia huku ndio utaratibu ambao tumejiwekea. Lakini mimi nimeipenda rai ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba ni vizuri kuiangalia kwa ajili ya kukuza *accountability*.

Mhe. Spika, mimi nadhani ile rai yake ni nzuri sana kwa sababu chombo hichi ndio kinachokwenda kitayasimamia hayo mashirika, kitayapitia sasa siku ile imekuja Kamati ya Baraza la Wawakilishi Mwenyekiti sijui unasimama wapi na wewe ni Mwakilishi wa jimbo lolote lile. Lakini tumekuja Kamati ya Baraza kuja kukagua au kuja kuhoji, kuuliza, sasa hapa inaleta ile *conflict* ya *interest*.

Sasa ndio maana nasema kwamba wana-*advocate* suala hili kwa nia ya kukuza *good corporate governance* kanuni ambayo sasa hivi ni muhimu sana katika uendeshaji au usimamizi wa utawala bora. Yaani mbali ya hii *democratic governance* kwamba iwe nzuri lakini *corporate governance* yaani uendeshaji wa hizi taasisi nao unatakiwa uzingatie misingi ambayo italeta uwazi zaidi, italeta uwajibikaji zaidi.

Lakini hili ni suala la sera na ndio maana hata yeye kalitoa katika angalizo. Mhe. Spika, mimi nasema ningeafikiana nae katika hoja ya kukuza uwajibikaji, katika hoja ya kukuza uwazi, mimi nadhani ni kitu kizuri cha kukizingatia.

Mhe. Spika, nikushukuru tena kwa kunipa muda na kunivumilia na baada ya kueleza hayo mimi naunga mkono hoja pamoja na marekebisho yake na yale ambayo baadhi ya mapendekezo na kuyakubali. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hapa kwa siku ya leo lakini pia kwa kujua umuhimu na mahitaji halisi ya mswada huu.

Mhe. Spika, napenda tena nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kutoa mchango wangu katika mswada huu. Kwanza niseme naishukuru michango karibu yote iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe, ni michango mahiri, michango mizuri yenye kuonesha ufahamu na kuendana na umuhimu halisi wa mswada huu.

Lakini pia Mhe. Spika, namshukuru kwa dhati sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa namna alivyojaribu kufafanua na kusaidia kujibu hoja. Lakini pia nimshukuru kwa ufanisi mzuri wa tafsiri zake mwalimu wangu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, mimi ningejaribu kutoa mchango wangu kwa kujaribu kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya sehemu zile ambazo Waheshimiwa Wajumbe niliowataja waliotangulia watakuwa kama wameyaacha. Miongoni mwa maeneo ambayo hawakuwahi kuyaeleza ni kutokana na hoja za Mhe. Abdulla Juma Abdulla alikuwa ana shaka kidogo kuhusiana na maeneo ya viwanja vya ndege.

Mhe. Spika, kwanza niseme nakubaliana na rai aliyoitoa Mhe. Abdulla ya kuona umuhimu wa kudhibiti eneo la kiwanja cha ndege na maeneo jirani yanayozunguka uwanja wa ndege.

Mhe. Spika, kama tutakuwa hatwendi mbali baada ya mswada huu ukiangalia katika mswada wa *Hydromark* umejaribu kuelezea vizuri umuhimu wa kuyadhibiti maeneo yanayozunguka uwanja wa ndege na maeneo yenye majengo yanayoathiri shughuli za uratibu wa viwanja vya ndege.

Lakini pia Mhe. Spika, Mhe. Abdulla Juma Abdulla alitaka kujua namna gani viwanja vya ndege pamoja na kwamba mswada huu haukuelezea utaratibu wa udhibiti wa mapato akatolea mfano wa Idara ya Uhamiaji. Napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi pamoja na kwamba maelezo yale ya mapato humu hayakuelezwa wazi lakini utaratibu uliopo hivi sasa ni mzuri wa kuona kwamba mapato yale yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji yanaingia katika Mfuko wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa utaratibu maalum ulioandaliwa.

Mhe. Spika, kwa kuendelea na hayo takriban Waheshimiwa Wajumbe wengi sana wameonesha *concern* yao katika *section 6* inayoelezea *component* ya Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi. Ni kweli hofu hii ina msingi mkubwa sana na nadhani hofu iliyojengeka ni sehemu mbili. Ya kwanza kwa namna gani mswada huu utajaribu kushirikisha taasisi binafsi katika ile dhana ya serikali ya kuona kwamba vyama binafsi na taasisi binafsi nazo zinashiriki katika shughuli za serikali katika utekelezaji wa malengo ya kuendeleza nchi yetu.

Lakini la pili *accountability* kwa kuona kwamba Makatibu Wakuu walioelezwa humu ni sehemu ya watendaji na wasimamizi wakuu wa wizara. Hivyo basi, ile *continuity* na *consistency* yao inaweza ikapata tatizo kwa kuona wao kuendelea kuwa Wajumbe wa Bodi. Nadhani Mhe. Waziri atauona uzito huo tutalizingatia na ninaamini watakaoteuliwa aidha wawe Makatibu Wakuu au Wajumbe wao watautambua umuhimu wa ushiriki wao katika vikao vya maamuzi vinavyotokana na mswada huu.

Mhe. Spika, naomba nikiri mapendekezo ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliyoyaeleza kutokana na tafsiri ya maneno hasa msingi alioeleza wa kufuatana na *alphabet*. Naomba nikiri hili ni jambo muhimu na tutalichukua na tutalifanyia kazi.

Mhe. Spika, labda na mimi kidogo niongezee alipoishia Mhe. Mwanasheria Mkuu juu ya sifa za Mkurugenzi Mkuu. Naomba niungane kwa kuomba kwamba kifungu hiki kiendelee kama kilivyo kwa kutambua kwamba mtu huyo awe na taaluma ya Chuo Kikuu au taaluma ya kutoka chuo chengine kinacholingana na hicho Chuo Kikuu.

Kwa mfano kama wenzetu wa kada ya urubani, wanakuwa wanapanda daraja kwa mujibu wa utendaji wao kazi na muda. Kwa hivyo, mimi naamini tusijifunge sana kwa kuzingatia tu upeo au elimu ile ya kupata darasani, lakini tuwape fursa na wenzetu hawa wanaojiendeleza kwa utendaji wa kazi, kozi na mafunzo mengine yenye umuhimu kwa kadi kama hii.

Mhe. Spika, nadhani mengi yaliyoelezwa na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Mhe. Mwanasheria Mkuu, wamejaribu kuyaeleza. Naomba tu niseme kwa niaba yangu mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Chwaka, tunaunga mkono mswada huu pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na kwa ruhusa yako naomba na mimi kuchukua nafasi hii ya kujibu, kufafanua, kutoa ushauri kwa michango ambayo imetolewa na wajumbe wako wa Baraza hili tukufu.
Mhe. Spika, kwanza nataka niwashukuru sana wajumbe wako, kwa namna ambavyo mahudhuria ya leo yanavyoonekana, maana leo ni Jumamosi na kwamba yele mazito sana ya buti sio kuwa hayatokuwepo, lakini yatapungua.

Mhe. Spika, mswada huu kama tulivyoueleza awali una umuhimu wake kwa nchi yetu ya Zanzibar. Mswada huu umechangiwa na wajumbe wako 12 na wewe ukiwa wa 13 kwa maandishi. Wajumbe 11 wamechangia kwa kusema hadharani, wenzetu *backbenchers* wanaita shimoni. Wajumbe wenyewe nataka niwatambuwe kama ifuatavyo.

1. Mhe. Rashid Seif Suleiman ambaye aliiwakilisha kamati, kwa hivyo nachukua kamati kama ni mchangiaji mmoja.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
3. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
4. Mhe. Jaku Hashim Yakoub
5. Mhe. Hija Hassan Hija
6. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
7. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
8. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria
9. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
10. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali
11. Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano
12. Mhe. Asaa Othman Hamad - kwa maandishi na
13. Wa mwisho lakini sio kwa umuhimu ni wewe binafsi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mswada huu unaonesha ule uzito wake uliopo maana yake mpaka Spika na yeye kuchangia basi ujuwe kwamba ngoma nzito.

Mhe. Spika, mswada huu inawezekana kabisa ukawa umesomwa leo na wajumbe wako wakaupitisha leo hii hii. Wajumbe hawa 12 wewe ukiwa humo, sio kwa sababu wengine hawana la kuchangia, lakini tafsiri yangu mimi ni kwamba wawakilishi wako wanafuata kanuni. Hakuna haja ya kurudia yale yale, labda utaratibu wa mswada huu ni kama ilivyo taratibu nyengine. Umeanza na mtu tu kabuni, kaibua, ukaingia serikalini, ukaja miundombinu, ukenda kwa Mwanasheria Mkuu, ukenda Baraza la Mapinduzi, ukenda kwenye Kamati za Baraza na leo hii tuko kwenye *final*.

Kwa hivyo, yote yaliyopita *final* leo iko hapa na ndio nikasema kwamba usione kwamba wachezaji wengine hawakuingia uwanjani, kwa sababu ni wagonjwa hapana. Ni kwa sababu wachezaji ambao wamo kiwanjani hawa 13 au 12 basi walitosha kabisa. Kwa sababu mswada wenyewe kama ambavyo umesifiwa. Mhe. Spika, kamati ilifanyakazi juu ya mswada huu siku tatu. Tunamaliza kikao hapa, tunakutana katika ukumbi mwengine hapo juu. Kwa hivyo, urahisi huu, mimi nasema urahisi, ingekuwa mswada huu haukuwekwa vizuri sana basi siajabu kwamba tungekesha. Kwa sababu wajumbe wasingekubali mswada huu kupita bila wao kuridhika na ndio maana nikasema kwamba wajumbe hawa 12 wamekidhi haja ya wajumbe wengine wote.

Mhe. Spika, ufafanuzi uliotolewa na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Naibu Waziri wa wizara hii, mimi sitaki nirudie tena. Kwa sababu sidhani kama nina ufundi mkubwa wa kisheria angalau unaofika robo tu ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Mhe. Mwanasheria Mkuu na hata Naibu Waziri wangu. Kwa sababu Naibu wangu pia ni mwanasheria. Kwa hivyo, hawa wajumbe watatu yale mambo yote ya kisheria mimi nimeridhika nayo, ila

kuna mahali mwengine mimi kama waziri ninatakiwa hapa nitowe fatwa ya mwisho, basi hayo nitayasemea.

Mhe. Spika, sitaki niende moja kwa moja kwa kila mtu, lakini kuna mambo ya msingi ambayo ni vizuri niyaseme. Kwanza kabisa nakubaliana kabisa na marekebisho yote yaliyofanywa na kamati ya Baraza na yale ambayo wajumbe wamechangia kuyarekebisha yale ya kamati, yamo mawili au matatu.

Mhe. Spika, kuhusu sifa za Katibu wa Bodi, nazikubali kama ambavyo zimependekezwa, awe mwanasheria na awe na angalau shahada ya kwanza ya taaluma hii.

Kuhusu suala la adhabu Mhe. Spika, nakubaliana kabisa na ilivyopendekezwa na vile ambavyo Mhe. Mwanasheria Mkuu ametuelekeza hapa. Kwa sababu baada ya sheria hii kupitishwa na sisi wajumbe, itarudi tena kwa Mwanasheria Mkuu ili ikawekwe vizuri kwa mujibu wa haya makubaliano yetu tuliyopitisha. Baada ya hapo Mhe. Mwanasheria Mkuu atampelekea Mhe. Rais kwa ajili ya kuwa *assent*, kadiri atakavyoona Rais ndio hivyo hivyo. Naamini kwamba ataikubali.

Mhe. Spika, mimi nina hakika Rais anatusubiri sisi na ndio maana nilivyosema awali kwamba mswada huu haukuletwa kikao kingine kinachokuja labda Oktoba, kwa sababu kuna watu sasa hivi wanasubiri mswada huu upite ili wapate kinga kisheria, ili huo uwekezaji katika uwanja wa ndege uweze kuanza mara moja. historia ya kwa nini tunafanya mswada huu leo, Mhe. Spika, unajua zaidi. Ilikuwa mswada huu, kwa taarifa ambayo nilipewa awali, mara baada ya hotuba ya bajeti ya tarehe 15/06/2011, ilikuwa tunakaa hapa kuanzia tarehe 16, 17 mpaka tumalize, halafu ndio tena tuingie katika mjadala wa bajeti ya wizara moja moja, kwa ule umuhimu wa mswada huu ulivyo.

Kwa hivyo, Waheshimwa Wajumbe, hii ni kwa taarifa yenu. Vie vile ni kwa namna ambavyo mnapoondoka huko, kwa nini mkajadili miswada baada ya bajeti ni kwa sababu yaumuhimu na namna ambavyo Rais wetu na serikali yake hataki kuwacheleweshea maendeleo endelevu Wazanzibari, hata kwa dakika moja. Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika hili wajumbe wote waliosimama hakuna hata mmoja aliyesema kwamba mimi nitaunga mkono baada ya hili au hili. Wote wamesifu, wamepongeza na wameunga mkono kwa niaba ya wananchi wao na wao wenyewe. Kwa hivyo, hii ni faraja kubwa.

Mhe. Spika, Mahmoud ameelezwa vizuri na Mhe. Mwanasheria Mkuu kuhusu tafsiri hasa ya *aerodrome* sitaki niirudie ni hiyo hiyo, ni tafsiri ambayo popote utakapokwenda duniani tafsiri ni hii. Kwa hivyo, sisi hatungeweza kubuni yetu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla, ameeleza vizuri na nimtowe wasi wasi tu kwamba mambo mengi katika viwanja vya ndege vyetu viwili, uwanja huu wa kimataifa na ule wa Pemba, yamekuwa shaghala baghala kwa sababu viwanja vya ndege hivi vilikuwa vinaendeshwa kiidara na kiidara mnajua maana yake nini. Bajeti yetu ina *ceiling*, unapeleka kwamba mimi nataka bilioni moja, unaambiwa aah! Huko huko. *Ceiling* ni dari maana yake huwezi kuruka zaidi ya hapo, ukiruka zaidi unajigonga, unapewa milioni zako 300. Sasa milioni 300 hizi ufanye lipi na uwache lipi.

Mhe. Spika, ni imani yangu kabisa kwamba mamla hii itakayoundwa kwa muda wa kipindi kifupi kabisa, si uwanja wa ndege wa Pemba wala sio wa hapa Unguja, kila mtu ataona mabadiliko, tena mabadiliko ambayo yeye hakuyategemea. Waheshimiwa Wajumbe, tuupitisheni mswada huu ili tuone mamlaka hii itakavyofanya mabarekebisho na mabadiliko katika viwanja vya ndege vyetu hivi.

Kwa hivyo, mashimo yale kwenye uwanja wa ndege, uwanja wa ndege kuwa hauna taa, uwanja wa ndege kuwa hauna uzio. Yote hayo yatashughulikiwa na mamlaka yenyewe kwa sababu mamlaka hii itakuwa na fedha kwa kadiri ambavyo tumekubaliana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, lakini nina hakika zitakuwa ni za kutosha kuweza kukimu mahitaji yao. Nina hakika Mhe. Spika, masuala haya ya kuwa uwanja wa ndege hakuna hata *tissue paper*, uwanja wa ndege hata mzungu ana kipepeo anajipepea, uwanja wa ndege hakuna kiti cha kukalia. Hayo yote yatakuwa ni historia tu.

Mhe. Spika, nataka nichukuwe fursa hii kujibu suala kuhusu eneo la uwanja wa ndege. Mhe. Spika, eneo la uwanja wa ndege zamani likiitwa Kisauni, halafu ukaitwa uwanja wa ndege wa Zanzibar. Sasa ni *Abeid Aman Karume International Airport*. Mhe. Spika, eneo lile lina mipaka yake na inajulikana. Sio inajulikana na serikali tu, hata wenyeji wa pale wanalijua. Lakini kwa sababu hakukuwa na udhibiti, ndio eneo lile limevamiwa mno. Sasa hivi tunapata kazi ya kununua. Mtu anajua kabisa kwamba *beckon* au kigingi cha uwanja wa ndege mwisho ni hapa basi anakwenda kujenga mbele yake.

Mhe. Spika, uwanja wa ndege una majirani wengi umezungukwa. Ukitoka kwenye ukuta wa uwanja wa ndege hatua nne au tano kuna nyumba ya mtu. Mhe. Spika, ukuta ule ambao umejengwa kule sio pale ulipotakiwa ujengwe, umejengwa ndani ya eneo. Umejengwa ndani ya eneo kwa sababu gani, kwa sababu ya umuhimu wa kwamba ni lazima kuwe na ukuta, hilo moja. Lakini tukasema umuhimu huu kama tungeuanza kule ambako ulitakiwa uanze basi serikali ingeshindwa kujenga, *compensation* ingekuwa kwa mabilioni. Lakini bado tunalitambua kwamba ni eneo letu.

Mhe. Spika, nataka nichukuwe nafasi hii kuwaambia wananchi ambao wako karibu na ukuta, kwamba ukuta ule uko ndani. Iko siku Mwenyezi Mungu mkubwa, nchi hii itakuwa tajiri ya kuweza kuwaondoa wote na tukapata eneo letu lote, lakini watakuwa wameondoka kwa kuridhika kwa fidia watakayopata. Tusiendelee tena kujenga, tusiuze viwanja maeneo yanajulikana. Katika awamu hii ya kwanza ya bajeti yetu, tutarudia tena kuweka mipaka yote, ili mtu ajuwe kabisa kwamba mimi sasa hivi niko ndani ya kiwanja cha ndege.

Mhe. Spika, kiwanja chetu kimefika mpaka Buyu baharini kwa taarifa yenu. Kuna mita chache tu, lakini huko Buyu sasa hivi kumeshajengwa mpaka mahoteli. Mhe. Spika, nasema ni udhibiti, hapakuwa na udhibiti mzuri. Lakini kwa vyovyote vile suala la ukubwa wa kiwanja cha ndege au maeneo yake, sio suala tu kwamba serikali inataka, lakini kwa usalama wa waliokaribu na kiwanja cha ndege.

Mhe. Spika, katika miaka ya 1970 mimi nilikuwa mwanafunzi hapa *Karume Institute Technical Collage*. Kwa mara ya kwanza ndege aina ya DC 9 ilitua,

wengine watakuwa wanakumbuka, sisi tulikuwa wanafunzi mule, wengine tulikamatwa pwani, tunakimbilia wapi hatujui, tunaona kiama, viyoo vya madirisha vyengine nyang'anyang'a, kwa mara ya kwanza hiyo.

Sasa leo kiwanja kimoja cha Uganda, nimesoma katika gazeti moja, ilitua ndege kwa mara ya kwanza zile kuta ambazo zimejengwa kama hizi za Baraza, basi nusu ya zile kuta zilizojengwa zilianguka kwa mshtuko na kwa *vibration*, kwa sababu hazikujengwa kwa *specification* ya ndege kama zile. Sasa siku ikija kutua ndege hapa kubwa lecluse halculizi na yatatua *Inshaallah*, uwanja wetu unaruhusu, ukakuta mapaa ya nyumba za karibu yote yameng'olewa nani atalipa, au majumba yamebomoka nani atalipa. Kwa hivyo, sio suala la kwamba hatutaki watu wajenge pale, tunataka watu wawe salama na uwanja wa ndege, isiwe uwanja wa ndege iwe kama nakama.

Mhe. Spika, tutawachukuwa wawakilishi wa maeneo yale, Kiembesamaki na Dimani, tutawachukua masheha, madiwani na serikali ya wilaya na mkoa, tukaone kwa pamoja mpaka unatoka hapa mpaka wapi mpaka wapi na kwamba watakaokaa katika maeneo hayo, basi wajuwe kuwa wanakaa katika maeneo ya uwanja wa ndege mapema kabisa. Sasa utaratibu wa kuwaondoa, nasema hayo ni mambo ya baadae ya serikali, lakini bila shaka hawatoondolewa kama vile sio wananchi wa hapa au kama vile hawana haki. Tunachozungumza ni kwamba wasiendelee na gharama zaidi ya kujenga, hivyo hivyo walivyojenga basi ibaki hivyo. Nafikiri nimeeleweka.

Mhe. Spika, kuhusu wajumbe wa bodi. Nakubali kabisa kwamba wajumbe wawili watakaoteuliwa na waziri wawe wanatoka katika sekta binafsi. Lakini hawa wajumbe wengine, kwa ufafanuzi ambao wenzangu wameutoa nakubali kabisa. Kwa sababu wajumbe wa waziri ni watano tu.

Vile vile suala la mwanasiasa kuingia na hili nakubaliana nalo kabisa Mhe. Spika, kwa sababu ya huo uwajibikaji. Lakini hapa kuna *very big but*. Mwenyekiti wa bodi naye ni mjumbe, huyu anateuliwa na Rais. Kwa hivyo, hii kwamba wajumbe wasiwe wanasiasa, kasoro yule ambaye mwenyewe Rais atamteuwa, anaweza kuwa mwanasiasa au anaweza kuwa yote, kwa sababu uwezo wake yeye sisi hatuwezi kuuliza. Lakini hawa wajumbe wengine watano, bodi ya mamlaka hii ni *technical*, ni ya kifundi kabisa, sio ya kisiasa. Unapozungumzia viwanja vya ndege ni mambo ya kifundi. Kwa hivyo, hata hawa wajumbe wawili kutoka sekta binafsi na wao watakuwa na sifa ambazo zitawawezesha kufanyakazi vizuri katika bodi hii.

Nije kwa Spika. Mhe. Spika, anasema kwenye mswada mzima hakuona kifungu ambacho kinazungumzia mizigo. Mizigo ni pamoja na dawa ya kulevya, kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu. Mhe. Spika, katika masuala ya mizigo ni masuala wanaita *ground handily*, ndege inakuja mzigo inatolewa inaingizwa, ndege zinasafishwa, abiria wanachekiwa. Hii hatukuiweka kwenye sheria kwa sababu ni katika kazi za mamlaka ya viwanja vya ndege pamoja na wadau. Lakini kabisa kwa kazi za mamlaka hii, malalamiko kuhusu mizigo, abiria, *departure lounge, arrival lounge*. Nakuhakikishia Mhe. Spika, wewe mwenyewe utapenda na utapenda hasa kwamba mimi niende zangu uwanja wa ndege angalau nikaone tu ile raha iliopo.

Mhe. Spika, naamini kwamba wewe una *automatic pass* ya kuingia uwanja wa ndege, wakati wowote unaotaka. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kuhusu suala hili limekuwa *technical to country* katika *ground handily*, ambayo humu haikutajwa lakini ni miongoni mwa kazi za, ukisikia kudhibiti, kuvitunza, kuviendeleza na kuvisimamia iko katika pale, lakini hatukuifafanua kwamba mizigo iwe vipi, abiria wawe vipi na *ground handily* iwe vipi.

Mhe. Spika, kuhusu sheria ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu aliifafanua katika kifungu 12(c) wajumbe wame-*rise concern* yao. Mimi nakubaliana kabisa na Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini pia napenda sana *concern* ya wajumbe, nayo vile vile niitambuwe. Kwa mujibu wa Mwanasheria Mkuu kifungu kile kikawepo, kisipokuwepo hakuna dhara yoyote. Amesema kabisa, hata sheria ya bandari ile wanaita ni *regulatory*, lakini haitukatazi kufanya shughuli zetu na hata hizo shughuli zetu Mhe. Spika, tunazifanya kwa mujibu wa sheria za anga, kikao, siasa za kimataifa.

Kwa hivyo, nasema kifungu kile cha 12(c) kama kilivyo kinaweza kikabaki tukafanya shughuli zetu, wala hakituathiri na kinaweza kabisa hata kikiwa hakipo na ikawa hakituathiri. Sasa hili nalichukua ili wakati Mhe. Mwanasheria Mkuu atakapoona kuna haja ya kuwepo au kutokuwepo kabla waraka huu haujapelekwa kwa Mhe. Rais. Lakini kwa ufahamu wangu na ilivyo ni kwamba hata kikiwa hakipo na hata kikiwa kipo matumizi yake ni sawa sawa.

Mhe. Spika, Mhe. Asaa Othman Hamad amezungumzia suala la *(PPP), Public Private Partnership* ambalo hakuliona humu. Lakini nasema kwamba hizo ni shughuli nyengine ni katika kazi za mamlaka hii. Yeye amesisitiza kwamba hili labda lingeingizwa basi ingekuwa ni kivutio zaidi kwa wawekezaji.

Mhe. Spika, mswada huu wa *Zanzibar Airport Authority* pamoja na mswada ambao tutaujadili baadae. *The Airdromes Act of Zanzibar*, miswada hii miwili inatosha kabisa kwa *serious investor* kuja ku-*invest* Zanzibar katika masuala ya anga. Ni *protection* yao ya kutosha na ni kwa sababu hiyo hiyo, suala la utawala bora wa serikali hii, kila kitu kiko wazi, mwekezaji ana haki zote, ana haki ya kushtaki na ana haki ya kushtakiwa. Lakini kutakuwa na sheria ambayo yeye inamlinda, bila sheria hizi Mhe. Spika, watu wengi wana *hesitate*.

Mhe. Spika, ndio maana hadi leo mradi ambao siku zote ulikuwa unazungumzwa hapa kwamba Kampuni ya Kituruki inataka kuekeza kuna hiki na hiki, ni hadithi tu, hakuna hata moja. Matayarisho yote yamekamilika, lakini nikasema hapana hatuwezi kutia mguu wetu kama hakuna sheria na ni sheria hii pamoja na nyengine ambayo tutaijadili ndio itakayowafanya pengine baada ya Mhe. Rais kuwa *assent* kukubaliana hata tarehe ya lini tusaini *contract* kwa ajili ya maendeleo ya viwanja vyetu vya ndege, vivutie viwe vizuri zaidi na kila mtu apende.

Kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wajumbe hatujafika mbali, lakini hiyo hiyo *improvement* ya hivi karibuni *Oman Air* ilianza na ndege mbili kwa wiki, biashara ikakua, ikawa ndege tatu kwa wiki. Leo ninavyokuambia ni mara nne kwa wiki na jana Balozi tena sio mara nne kwa wiki kuwa ni *shedow* tu hapana, ndege zinajaa

wakati wa kwenda na zinajaa wakati wa kurudi. Mhe. Balozi jana ananiambia kwamba sasa hivi tunafikiria kuja kila siku, s*even frequencies a week*, wameanza na *two frequencies* na hiyo ni *improvement* ndogo tu.

Mhe. Spika, tukipitisha sheria hii nakuhakikishia kuna siku utasema ndege zetu jamani hapana, ndege nyengine zisije. Zinapokuja ndege basi kuna mengi, wanafikiria kuanzisha *flight* kutoka Zanzibar kupitia Muscat mpaka China kuna mji maarufu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Abubakar Khamis Bakary anaujua, biashara huku ni kubwa mno. Sasa ikifika hali hiyo na iko karibu sana, basi wafanyabiashara wetu watachukua vitu kutoka China moja kwa moja mpaka tena kwa bei rahisi.

Mhe. Spika, nasema tu umuhimu wa sheria ni kwamba ni kivutio kwa wawekezaji.

Mhe. Spika, nimesema kwamba mambo mengi yaliyozungumzwa yametolewa ufafanuzi na wala nisingependa hata kidogo kurudia hayo kwa hayo, kwa sababu waliotoa ufafanuzi na ufafanuzi fasaha tena nakubaliana nao. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo pamoja na makofi hayo Mhe. Spika, naomba kuwasilisha na kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiye na Wizara Maalum): Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, 2011

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, 2011

Kifungu 1	-	Jina Fupi na Kuanza Kutumika pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 2	-	Ufafanuzi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 3	-	Kuanzisha Mamlaka pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 4	-	Mhuri wa Mamlaka pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 5	-	Kazi na Uwezo wa Mamlaka.
Kifungu 6	-	Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Marekebisho yake.

Kifungu 7 - Kazi za Bodi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 8 - Uwezo wa Bodi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 9 - Katibu wa Bodi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 10 - Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 11 -

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba marekebisho yaliyofanywa na kamati waliongeza kifungu cha (d), ambacho mimi nahisi kinarejea kile kifungu cha (c), yaani kinarejea kifungu cha 11(1) (c) kile cha (d) kilichoongezwa.

Kwa hivyo, nadhani kama haya marekebisho yatakuwa sio sahihi unless labda sikuyafahamu. Lakini nahisi kama kile kifungu cha (c) kinajitosheleza bila ya kukiongeza kifungu cha (d).

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maamuzi yake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri marekebisho yaliyotajwa hapa na kamati ni neno. Tukiangalia kifungu (c) na mimi wala silijui neno hili la Kiswahili kama lipo ‘atatekeza’ na iwe ‘atatekeleza’. Kwa hiyo, kamati warekebisho hilo neno na lisomeke atatekeleza kifungu cha 11(1)(c) neno la kwanza kabisa.

Kwa hivyo, marekebisho sasa itakuwa ni mambo mawili neno hili na yale aliyoyasema Mhe. Mwanasheria Mkuu ambayo Mhe. Waziri amekubali.

Kifungu 11 - Kazi za Mkurugenzi Mkuu pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 12 - Uwezo wa Mkurugenzi Mkuu.
Kifungu 13 - Uwezo wa Waziri pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 14 - Mgongano wa Maslahi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 15 - Uwezo wa Jumla wa Bodi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 16 - Mamlaka kupata Ardhi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 17 - Kukasimu Madaraka pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 18 - Ofisa Aliyeidhinishwa.

Kifungu 19 -

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, marekebisho ambayo yanapendekezwa na kamati hapa ilikuwa ni kuondoa neno ‘fedha’. Wakati nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba nadhani hili neno fedha tungeliacha kama lilivyo, isipokuwa tuongeze aya ya (f), kwa sababu kuanzia (a) mpaka (e) vinazungumzia fedha tu na wala hakuna kitu kinachozungumzia rasilimali.

Kwa hivyo, nikapendekeza tungeongeza maneno “Mali na rasilimali zitakazohamishiwa katika Mamlaka, baada ya kuanzishwa na mali nyengine zitakazonunuliwa au kupatikana wakati wowote kwa ajili ya Mamlaka.” Ili kifungu hiki kikae sawa basi nilipendekeza marekebisho hayo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, wakati tulipokuwa tukijadili suala hili na kamati tulichukua muda mrefu na Mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu alitaka ibaki hivi ilivyo. Lakini kamati ikapendekeza hivyo ilivyopendekeza.

Sasa kwa sababu kuna kifungu (f) kinachoongeza, basi nakubaliana na Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwamba kifungu cha 19(1) isomeke Fedha na rasilimali ni pamoja na halafu iendelee (a), (b), (c), (e) na (f) kama alivyopendekeza Mhe. Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

Kifungu 19	-	Chanzo na Usimamizi wa Fedha pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 20	-	Bajeti.
Kifungu 21	-	Hesabu na Ukaguzi.
Kifungu 22	-	Taarifa ya Mwaka.
Kifungu 23	-	Vitega Uchumi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 24	-	Hasara kwa Mali za Mamlaka.
Kifungu 25	-	Makosa yanayofanywa na Taasisi yenye Hadhi ya Kisheria.
Kifungu 26	-	Adhabu za Jumla pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 27	-	Watumishi waliopokazini Kuendelea na Utumishi.
Kifungu 28	-	Uhamisho wa Wafanyakazi.
Kifungu 29	-	Kanuni za Maadili.
Kifungu 30	-	Kuendelea kwa Mashtaka ya Kinidhamu.
Kifungu 31	-	Kinga kwa Kitengo Kilichofanywa kwa Nia Njema.
Kifungu 32	-	Kukabidhiwa Mali.
Kifungu 33	-	Kanuni.
Kifungu 34	-	Zuio la Kutokuchukuliwa Mali ya Mamlaka.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu pamoja na mabadiliko na masahihisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, 2011

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kusoma kwa mara ya pili Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Mambo yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Katibu: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Kazi zake na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo, sasa umepitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. *(Makofi)*

Mswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege ya 2011

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, awali ya yote nataka niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kuupitisha Mswada wa Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vya Zanzibar, tena wakiwa na nguvu mpya ya kusikiliza, kupokea na kujadili mswada wa pili wa wizara hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa ruhusu yako naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, kwa Kuingereza ni *Airdromes Act*.

Viwanja vya Ndege Zanzibar vimekuwa vikiendeshwa bila ya kuwa na sheria mahsusi inayosimamiwa na taasisi inayohusika. Matokeo ya kutokuwa na Sheria za Usimamizi wa Viwanja vya Ndege, imesababisha kuendesha bila ya kuwepo utaratibu maalum wa kufuatwa pindipo inapotokezea mwekezaji anayetaka kuwekeza katika maeneo ya viwanja vya ndege kama vile uanzishwaji wa Viwanja Binafsi utoaji wa huduma za Usafiri wa Anga na Taasisi Binafsi.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege *Draft Bills for Airdromes Act* ni utekelezaji wa Sera ya Usafiri na Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar, ambazo zinahimiza kuwepo kwa mipango madhubuti ya udhibiti wa huduma za usafiri Zanzibar. Hivyo, kutayarishwa mswada wa sheria hii kutasaidia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kusimamia kwa umakini zaidi shughuli za kila siku za viwanja vya ndege.

Madhumuni ya Mswada:

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inaomba kuwasilisha Mswada huu wa Sheria ya Viwanja vya Ndege (*Airdromes Act*), ambayo itahusiana na uendeshaji, usimamizi wa kazi katika Viwanja vya Ndege Zanzibar.

Kwa ujumla Mhe. Spika, Rasimu ya Mswada huu imegawika katika Sehemu Kuu Saba na ina jumla ya vifungu 31.

Sehemu ya Kwanza ni utangulizi wa sheria. Mhe. Spika, sehemu hii inazungumzia masharti ya kiutangulizi, yanayohusiana na jina la mswada, kuanza kutumika kwa sheria, matumizi yake, ufafanuzi wa maneno na misemo yenye maana maaluma katika sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Pili ya mswada huu Mhe. Spika, inahusiana na uanzishwaji na usimamizi wa Viwanja vya Ndege. Sehemu hii ina jumla ya vifungu vinane ambavyo vinazungumzia taratibu za uanzishwaji na udhibiti wa Viwanja vya Ndege Zanzibar na namna vitakavyosimamiwa. Vile vile Kamati ya Ufundi, masharti ya kibali cha ujenzi, maombi ya kibali cha ujenzi pamoja na masuala mbali mbali kuhusiana na usimamizi wa shughuli za Viwanja vya Ndege kama vile afya, utuaji na urukaji ndege viwanjani.

Sehemu ya Tatu ya mswada inahusu usimamizi na hatua za usalama. Mhe. Spika, sehemu hii ina jumla ya vifungu vitano vinavyoelezea udhibiti wa ardhi kwa ajili ya utuaji wa ndege, haki ya kutumia ardhi kwa ajili ya viwanja vya ndege na uzuiaji watu kuingia ndani ya viwanja vya ndege bila ya ruhusa. Aidha kifungu hiki kinazungumzia uundwaji wa Kamati ya Usalama na muundo wake.

Sehemu ya Nne ya mswada huu ni kuhusiana na utuaji na urukaji wa ndege. Sehemu hii ina vifungu vinne vinavyoelezea kanuni za ndege kutua uwanjani na uondokaji wake. Pia inaelezea uwezo waliopewa watendaji waliopewa jukumu la kusimamia kazi za ulinzi na usalama na taratibu za kisheria kwa ndege zinazoachwa holela kiwanjani.

Sehemu ya Tano inahusu ada na tozo za viwanja vya ndege. Mhe. Spika, sehemu hii ina vifungu vinne vinavyozungumzia ada zitakazotozwa kwa watumiaji wa viwanja, malipo ya kutua na kuegesha, pia uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Uwanja wa Ndege. Aidha inaelezea utaratibu utakaotumika baina ya mawaziri husika kuhusiana na ugawaji wa mapato hayo.

Sehemu ya Sita inahusu usalama wa ndege, viwanja vya ndege na vifaa vya kuongozea ndege. Mhe. Spika, sehemu hii ina jumla ya vifungu vinane vinavyohusiana na usalama katika viwanja vya ndege, masuala kama vile uhatarishaji wa usalama, vifaa vya kuongozea ndege na ndege zenyewe, umiliki wa vitu vya hatari kiwanjani, utupaji wa taka viwanjani au karibu na viwanja na adhabu kwa atakayeshindwa kuzifuata taratibu za kiusalama viwanjani.

Sehemu ya Saba inahusu mambo mengineyo. Mhe. Spika, sehemu hii ya mwisho ya mswada huu ina vifungu vitatu, vinavyozungumzia mambo mengineyo na yanayohusiana na hayo, ikiwemo makosa na adhabu, uwezo wa Mhe. Waziri kutengeneza Kanuni, kwa ajili ya kuwezesha kutekelezaji bora wa masharti ya madhumuni ya sheria hii.

Mhe. Spika, ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, wataujadili Mswada huu wa Sheria ya Uanzishaji wa Viwanja vya Ndege

Zanzibar *(Airdromes Act)* na kutoa ushauri wao ipasavyo na hatimaye kuupitisha kwa kauli moja mswada huu kuwa sheria iliyotungwa na Baraza lako tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, hoja imeungwa mkono na sasa tuanze mjadala. Kwa hivyo, nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kwa mara ya pili, kwa ajili ya kutoa Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada wa Sheria wa Kuweka Masharti ya Utawala, Udhibiti na Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege Zanzibar pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na hivyo kuweza kukutana leo, kwa ajili ya kujadili na hatimaye kupitisha Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Utawala, Udhibiti na Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege Zanzibar pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, kwa kuwa tunakusudia kuwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itakayovisimamia Viwanja vya Ndege vya Zanzibar, Mamlaka ambayo kimsingi inalenga katika kubadilisha mfumo wa usimamizi wa viwanja vyetu. Mswada huu ni muhimu sana ili kujenga misingi na taratibu kwa ajili ya kuleta ufanisi.

Mhe. Spika, kwa kuwa leo asubuhi hii niliitaja Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi naona hakuna haja tena kuirudia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kazi ya kuupitia mswada huo, kamati yetu imependekeza marekebisho kadhaa yenye lengo la kusaidia kuboresha mswada huo, yakiwemo marekebisho ya kilugha, lakini pia marekebisho ya kimsingi.

Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba niainishe baadhi ya marekebisho ya msingi ambayo kamati yetu inayapendekeza.

Mhe. Spika, kwanza kamati yetu inapendekeza kifungu cha 3(1) ambacho kinampa mamlaka Mhe. Waziri kutangaza eneo lolote kuwa ni Uwanja wa Ndege, kurekebishwa kwa kutaka kabla ya kutumia mamlaka hayo, Mhe. Waziri kuzingatia Sheria zinazohusiana na Ardhi. Hivyo, tunapendekeza kuingizwa maneno yafuatayo mwanzo wa kifungu hicho “Kwa mujibu wa Sheria za Ardhi zilizopo”.

Pamoja na kuamini kuwa Mhe. Waziri aliyepo atazingatia sheria katika kutumia mamlaka yake, ni vyema kukawa na misingi ya sheria inayoelekeza wazi wazi utaratibu wa kuzingatia Sheria za Ardhi katika kutumia mamlaka hayo.

Aidha kamati yetu inapendekeza kurekebishwa kwa kifungu cha 4(1)(d) ambacho kinampa mamlaka Mhe. Waziri kuteua idadi ya watu wengine katika Kamati ya

Ufundi bila ya kutaja idadi maalum kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, kamati inapendekeza kuweka idadi maalum ya watu wasiozidi watatu.

Mhe. Spika, kamati yetu pia inapendekeza kuongezwa katika Kamati hiyo ya Ufundi, Mhandisi wa masuala ya ujenzi. Hii ni kutokana na majukumu ya kamati hiyo ambayo ni kumshauri Mhe. Waziri katika mambo yanayohusiana na Kibali cha Ujenzi wa Viwanja vya Ndege. Kamati yetu inadhani mjumbe huyo atasaidia katika kumshauri vyema Mhe. Waziri katika masuala hayo kutokana na taaluma na uzowefu wake.

Mhe. Spika, kamati pia katika kifungu cha 4(2) ambacho kinaelekeza majukumu ya Kamati ya Ufundi, inapendekeza kurekebishwa. Kamati yetu inapendekeza kuongezwa kwa majukumu ya kamati hii kwa kuipa pia jukumu la kumshauri Mhe. Waziri katika suala la uendelezaji wa viwanja vya ndege mbali ya ile kazi ya kumshauri Mhe. Waziri katika masuala yanayohusiana na kibali cha ujenzi.

Mhe. Spika, baada ya kueleza mapendekeza hayo ya marekebisho ya mswada huu, kamati yetu inatoa wito kwa Mamlaka na Wizara inayohusiana na Viwanja vya Ndege kuhakikisha taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria katika utawala, udhibiti na uendeshaji wa viwanja vya ndege unaheshimiwa na kufuatwa kama ilivyoelekezwa chini ya sheria.

Mhe. Spika, kamati yetu inaunga mkono mswada huu na kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe kutoa maoni yao, ili kusaidia kuwa na taratibu nzuri za kisheria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuwa leo nimesoma mara mbili hapa na mimi ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka Jimbo la Ziwani, naomba niseme maneno machache kwa ruhusa yako Mhe. Spika, kwa kuufuatilia mswada huu binafsi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ziwani kwa misaada yao na kuniunga mkono hadi hii leo. Lakini Mhe. Spika, tokea mwanzo nasoma Kiswahili na ndio Lugha yangu, Waswahili wanasema ‘Mngojea maiti hungojea na kilio’, yaani usingojea mpaka maiti usingojee mpaka maiti akifika ndio ukaanza kulia utaonekana ni mchawi. Kwa hivyo hivi viwanja vya ndege tulivyokuwa navyo kile cha Pemba Mhe. Spika, hakina taa, kwa hivyo ndege wakati wa dharuba ya mvua na usiku haziwezi kutua na ndicho tulichokuwa nacho kwanza kabal ya hivyo vikubwa.

Mimi nikija hapa Unguja hakuna hata speka ya kutangaziwa je, Mhe. Waziri ikiwa abiria atakosa ndege kwa kuwa yuko chooni kosa litakuwa la nani, kwa hivyo tunaomba tungojee maiti na sisi tuanze kulia tujirekebishe hivi.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba kunga mkono mswada huu mia juu ya mia nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nikushukuru tena kwa kuniona na kunipa fursa kwa mara ya pili leo hii kuchangia mswada huu wa pili Mswada wa Sheria ya kuweka Masharti ya Utawala, Udhibiti na Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege vya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, niendelee kumpongeza rafiki yangu kaka yangu Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu tena niongezee bosi wangu wa zamani katika Chama kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii na matunda yanaonekana Mhe. Spika, tumepitisha punde hivi Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na sasa tunajadili Mswada huu unaohusu Utawala, Udhibiti na Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege vya Zanzibar.

Kwa jumla na taka kusema kwamba mswada huu umekaa vizuri na mimi nitakuja kusema kwamba nauunga mkono mia kwa mia, isipokuwa niseme moja tu la kumuwaidhi rafiki yangu pia Mhe. Mwanasheria Mkuu, hii miswada hasa ya Kiswahili ikitafsiriwa naomba waipitie kwa kina kwa sababu huu ukiupitia Mhe. Spika, unaweza kudhani kwamba tafsiri ya Kiswahili imefanywa na jama anayetoka pengine Kashmandi wakati anachukua mafunzo ya Kiswahili pale Taasisi kwa miezi sita halafu ndio wakatafsiri, unakuta uwanja ya, matumizi wa. Sasa Mhe. Spika, inanitia mashaka kidogo inanikumbusha hadithi moja naomba niseme kidogo.

Pale Lumumba Mhe. Spika, walikuwepo walimu wa jamii hii ambayo Kiswahili kilikuwa hakijakaa sawa sawa sasa siku moja mwalimu mmoja anasomesha kwenye darasa ikawa katika kusomesha anawaambia wanafunzi katika kutamka katamka watu nyingi, sasa huku nje kulikuwa na mwalimu Mkuu wa jamii ile ile akawa anapita akamsikia akaona kakosea huyu akaingia darasani, akaansa kumshambulia yule aliyekosea naomba radhi kidogo lakini naomba nisema akasema tizama vile kumbavu moja, nataka sema kisaili ya watu kujua haijui sio watu nyingi watu mingi. *(Kicheko)(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, ndio nikisoma miswada sio huu tu nikisoma miswada mingi inayokuja ya Kiswahili inanipa mashaka hayo kwamba hii imeandikwa na katika jamii zile kwa sababu huwa anastaajabu kuwa ile ya Kiingereza ambayo ni lugha ya kigeni kwetu inakuja imeandikika vizuri, lakini hii ya Kiswahili ambayo ndio lugha yetu ya taifa lugha tunayoitumia kila siku kuwa imejaa makosa kama haya. Sasa Mhe. Spika, haipendezi kila siku wajumbe turekebishe ya, wa, cha vitu kama hivi niliwahi kusema kwa mwanasheria ambae amepita sasa hivi ni Jaji Mkuu na nimuombe tena Mhe. Mwanasheria Mkuu ofisi yake katika hili wakipitia wawe washaitapa wajiridhishe ili makosa kama haya yasiendelee kujirejea.

Mhe. Spika, kama nilivyosema nikiondoa hayo kwa jumla mswada ni mzuri na mimi naupongeza naomba nipendekeze marekebisho machache hapa na pale, kwanza naomba nianze na kifungu cha tatu kifungu kidogo cha pili panapozungumzia kuanzishwa kwa uwanja wa ndege. Kifungu hiki kinasema.

“Waziri kwa madhumuni ya mambo ya anga anaweza kujenga, kutengeneza au kuweka katika uwanja wa ndege sehemu yoyote ambayo anaona itafaa jengo, muundo,vizuizi, hali inayofaa mazingira mazuri, mnara wa ishara, matangazo alama na vitu vyengine kadiri atakavyoona inafaa kwa ukamilifu ubora zaidi na matumizi salama na yaliyo bora ya uwanja wa ndege kama ni sehemu ya uwanja wa kutua ndege”.

Sasa Mhe. Spika, nilikuwa nataka hapa mwisho nataka tuongeze wa kutua na kurukia ndege kwa sababu *Air Port* sio kutua tu, inakuwa inafanya kazi zote mbili kwa hivyo napendekeza tuongeze hivyo kutua na kurukia ndege.

Pili Mhe. Spika kifungu cha 4(1) (d) nilikuwa na mapendekezo lakini nafurahi na naipongeza tena kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya kwamba wameliona hili, hapa ilikuwa imesemwa idadi ya watu wengine, iliandikwa idadi ya watu mwengine ndio katika ile niliyosema. Lakini nadhani imekusudia idadi ya watu wengine kama ambavyo waziri ataona inafaa, lakini nafurahi kwamba Kamati imeona na imeweka idadi pale kwamba angalau wasiozidi watatu na mmoja akiwa mwandishi. Kwa hivyo napongeza sana kamati kwa kuliona hilo.

Mhe. Spika, nikiondoka hap naomba vile vile katika nukta ambayo nilitangulia kusema ambayo inafanana katika kifungu cha 8(1) (d) Ukurasa wa 214 inasema. "Kuzuia kuenea kwa maradhi yanayoambukiza kwa njia yoyote ya ndege inayoondoka katika kiwanja chochote cha ndege". Nafikiri tuongeze pale kuzuia kuenea kwa maradhi yanayoambukiza kwa njia yoyote ya ndege inayoondoka au inayowasili katika kiwanja chochote cha Ndege, nilikuwa nadhani kwa madhumuni yale yale kama nilivyosema ya kuwa tumakava maeneo yote na hilo tulijumuishe.

Kwa msingi huo huo Mhe. Spika, kifungu cha 11 ambacho kipo katika ukurasa wa 215 katika mstari wa tatu pale inasema. "Ili kuepusha hatari kwa ndege zinazoruka". Sasa nataka nipendekeze tuongeze zinazoruka na zinazotua katika hali ya kisa au kutoona halafu iendelee kama vile ilivyo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ya marekebisho kama nilivyosema madogo madogo tu kwa sababu kwa jumla mswada umekaa vizuri, nizungumze lile ambalo nililizungumza katika mswada uliopita kuwa *consistence* ya adhabu, mimi namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba yeye anaonekana Kiswahili changu anakielewa zaidi kuliko Mhe. Abubakar Khamis Bakari, kwa sababu tuliporekebisha pale alinielewa kwamba alichokikusudia sio kuwango gani kikubwa na kipi kidogo au kwamba kuna *specific na general role* lakini kile alichokisema yeye kwamba haiwezekani kwa misingi ya kisheria ukawa huku una kifungo cha miezi sita, faini ya milioni tatu huku ukawa na kifungo cha miezi mitatu faini milioni ishirini hayakubaliki hayo.

Sasa hili limejitokeza katika mswada huu kwa ukubwa zaidi Mhe. Spika, kuliko hata ule uliopita kwa hivyo hili nilikuwa naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu baadae watakaa walitazame kwa ujumla sioni sasa hivi mimi nipendekeze turekebishe vipi. Lakini nasema utayaona hayo Mhe. Spika, na niyataje kwa haraka haraka kuwasaidia, kwanza kifungu kidogo cha 3 kilichoko ukurasa wa 215 pale nilikuwa naona pameandikwa mtu akayemzuria ofisa aliyeidhinishwa kufanya kazi iliyoelezwa katika amri atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita.

Sasa nikawa najiuliza kwa kosa kama hili tu wakati kuna mengine makubwa tumeweka faini na kifungo hapa tumeweka kifungo tu hapana haja ya kuwekwa faini hapa ili kukawa kuna mbadala, naomba Mwanasheria Mkuu asaidiane na wizara walitazame hili.

Lakini nikiondoka katika hili Mhe. Spika, yale niliyoyasema naomba niyaseme tu nivitaje vifungu vyote halafu tutafute njia ya kuviwekea *consistence* kwa kufanya marekebisho ya mswada huu, kwanza kifungu cha 13(1) pale pana adhabu inayozungumzia atakayekuwa ametenda kosa atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu.

Sasa ondoka hapo Mhe. Spika, katika mswada uje katika kifungu cha 16 kifungu kidogo cha tatu ukurasa wa 217 kinasema akipatikana na hatia kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

Halafu niondoke mie sasa twende katika kifungu cha 24 hichi kabla sijakitolea maoni lile suala la *consistence* ya adhabu kwanza naomba nikigusie kwa ujumla wake. Hiki kinasema. “Mtu yoyote yoyote atakayeharibu au kuzuia jambo lolote abalo litapelekea hatari katika anga au katika kifaa chochote muhimu au usalama wa ndege atakuwa amefanya kosa.”

Sawa cha pili kinasema “ Mtu yoyote atakayefanya jambo lolote ambalo linaweza kupelekea hatari kwa ndege yoyote inayoelekea Zanzibar ikiwa angani atakuwa amefanya kosa na baada ya ndege kutua tu katika uwanja wa ndege wa Zanzibar atawajibika kushtakiwa kama vile kosa limetokea uwanja wa Ndege wa Zanzibar.

Sasa Mhe. Spika, nilikuwa nasema kwamba je hili tumelitizama kisawa sawa kwa sababu tuchukue mfano, ndege ya watalii kutoka Itali inaelekea Zanzibar mara baada ya kuondoka Rome wakati bado ikiwa katika Anga za Italia abiria mmoja baada ya kupewa pombe na kulewa humo ndani ya ndege akafanya kosa, anadhibitiwa hadi Zanzibar kwa sheria hii kwa sababu inaelekea Zanzibar atakuwa amefanya kosa hapa kwetu. Sasa Zanzibar itakuwa na faida gani kuichukua dhima ya jambo ambalo halimo ndani ya mipaka yake.

Pili nani atalipia mashahidi kutoka nchi za nje kwa kesi kama hiyo. Ikiwa huko kwao sio kosa sisi tunalifanya kosa hapa tunawapa nafasi lile shirika la ndege kuja kutumia kwa sababu hili kwenu ni kosa wakakupeni wakakuachieni mzigo kuja kukaa hapa tunashitaki, kwa hivyo mnajiingiza katika gharama ambazo hazina sababu. Sasa ,mimi nilikuwa nasema pengine kuna nia njema lakini hebu tutizame tunataka kweli kujiingiza katika gharama kama hizo hazitotokea mara kwa mara lakini zinaweza kutokea, nilikuwa naomba tulitizame hilo

Lakini mbali na hilo Mhe. Spika, lile la adhabu sasa kama litakuwa linaendelea kuwa ni kosa hapo panazungumzia mtu akifanya kosa atawajibika kulipa faini isiyopungua shs. 500,000 au kifungo kisichopungua miaka miwli.

Mhe. Spika, ukija katika kifungu cha 29 kosa kwa taasisi pale panasema unalipa faini isiyopungua shs. 4,000,000 na isiyopungua shs. 2,000,000 au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita nadhani nimeeleweka kwa kifupi hakuna *consistence* maana yake kama kifungo miezi sita basi tuende hivyo, au kama miezi mitatu lakini haiwezekani huku faini shs. 20,000,000 kifungu miezi sita, au miezi mitatu, au huko faini Shs. 500, 000 kifungo miezi sita havilingani hivyo. Kwa hivyo nilikuwa naomba hili tulitizame vizuri.

Kifungu cha 28 hivyo hivyo Mhe. Spika, kifungu kidogo cha tatu pale inasema mtu atakayetenda kosa atalipa faini isiyopungua Shs. 1,000,000 au kifungo kwa kipindi kisichpungua miezi mitatu, kwa hivyo hayo Mhe. Spika, yako katika maeneo mengi tu, lakini nilitoa katika ulinganifu mzuri katika sheria kifungu cha 27 kinasema mtu akitenda kosa katika kushingwa kufuata masharti ya usalama atatozwa faini isiyopungua shs. 20,000,000 au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano sasa hapa naikubali. Kwa sababu hapa kile kifungo na faini viko juu ya makosa yote mengine yaliyotajwa pale, kwa hivyo pana *consistency* katika hili lakini kule kwengine naomba vifungu virejewe.

Labda watungaji wa sheria waliobobea waje wanisaidie kwamba tunaambiwa katika haya mambo ya penalti au makosa na adhabu mara nyingi katika sheria huwa yanawekwa pamoja, sasa katika mswada huu kila sehemu inazungumzia kosa lake halafu pamewekwa na adhabu zake. Je hii ndio utaratibu mzuri ama ule wa kuwekwa pamoja naomba nieleweshwe hapo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kabla sijakaa mwisho katika yale ya lugha hili ni *very serious* na ndio maana nimeliweka mwisho naomba tujirekebishe Mhe. Spika. Kifungu cha 13 ukurasa wa 216 kwa bahati mbaya hili hata Kamati hawakuliona anasema naomba nikisome.

Kifungu cha 13 kifungu kidogo cha 2 Mhe. Spika. “Mtu hatokuwa na hatia ya faini au kifungo chini ya kijifungu cha kwanza cha kifungu hiki isipokuwa kama itaelezwa kwamba wakati unaohusika taarifa ya onyo na uwajibikaji wa mtu inayopita katika chini ya kifungu hiki inayowekwa katika hali inayoonekana kwa urahisi na kusomeka na wananchi, sehemu hiyo au mikapa ya kuwekea ndege au mtu huyo amejulishwa kwa maneno baada ya marekebisho au ameonja kuhusiana na kupita huko”.

Mhe. Spika, sasa hili la kuonjwa hili ni *very serious* na halikuonekana na kamati naomba tulirekebishe. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa niaba yangu na wananchi wa Mji Mkongwe na nampongeza Mhe. Waziri kwa hatua hizi namtakia kila la kehri na tuone ishaalla Zanzibar inapiga hatua kubwa sana katika masuala haya ya uendelezaji wa usafiri wa anga, na uendelezaji wa viwanja vyetu vya ndege ili Zanzibar kweli irejee kuwa ni kituo kikuu cha mawasiliano na Biashara katika ukanda huu, ile ndoto yetu ya miaka mingi ya kuifanya Zanzibar kuwa Hong Kong ya Afrika ya Mashariki ishaalla itimie, Mhe. Spika, naunga mkono hoja *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi naomba nitoe mchango wangu mfupi sana katika Mswada huu kwa mara ya pili kwa Mhe. Waziri kwa leo moja mchango ambao utakuwa sio mkubwa sana.

Mhe. Spika, mchango wangu wa mwanzo ni kifungu cha 6(3) mswada unafahamu kwamba kwa mujibu wa sheria hii Masharti ya Sheria ya Mipango Miji hatotumika katika ujenzi au uendeshaji wa viwanja vya ndege vya Serikali, Mhe. Spika, Zanzibar ni visiwa na visiwa vidogo sana, taratibu za mipango miji hadi hii leo bado hatujaweza kuzidhibiti lakini sheria hii imesema kwamba haitojishughulisha na suala zima la mipango miji. Nadhani sentensi hii kidogo sio sahihi ni vyema mamlaka hii sheria hii basi angalau kungekuwa na mashauriano kati ya mamlaka hizi na wenzetu hawa mipango miji ili tukaweza kuweka sambamba udhibiti mzima wa shughuli hizi, kungekuwa na mawasiliano angalau udhibiti wa sheria hii na wenzetu wa mipango

miji kwa ajili ya kuweka usalama na utaratibu mzuri wa ujenzi katika maeneo ya viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, mchago wangu mwengine ni kifungu cha 10 ambao unaeleza suala zima la usalama wa ndege, kifungu cha 10 (1) mpaka (3) kimeeleza usalama wa ndege lakini kimeeleza zaidi katika maeneo ya nje ya ndege, kwa maana maeneo ya viwanja, maeneo ya hatarishi nyengine lakini mswada huo haukuzingatia hasa usalama wa ndege ndani ya ndege yenyewe. Mhe. Spika, kwa mfano ndani ya ndege zetu hapa Zanzibar kunatokea makosa mengi sana, kwa mfano ndege itakuwa imeeleza kwamba si ruhusa kutumia masuala ya simu au vifaa vya *electoronic*. Lakini humu kwenye mswada haukueleza matumizi yale ya kwenye ndege. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anisaidie usalama wa ndege yenye ndani ya ndege kwa maana ya pilot wenyewe na abiria wenyewe mswada huu umezingatiwa vipi.

Mhe. Spika, jengine hata suala hili halikuzungumzia matumizi ya nafasi ya rubani, kwa mfano tumekuwa tukisema hapa kwamba ndege nyingi za Zanzibar rubani amekuwa ni mmoja. Mhe. Spika, rubani ni mwanadamu kama litatokezea tatizo la rubani kupata tatizo lolote lile la kiafya maana yake ndege hiyo inakwenda hatarini. Mhe. Spika, mswada huu nadhani ungezingatia kwamba sasa kuna haja ya kuona ndege zenye rubani wawili ili ubinadamu ukitokezea kwa mtu mmoja basi mwengine aweze kuokoa tatizo lile la ndege na usalama wa abiria wetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo kwa usalama wa ndege kungekuwa na uendelezo wa taarifa au taaluma za usalama ndani ya ndege kwa maana ya kwamba wafanyakazi wa ndege wenyewe waweze kutoa maelekezo kisheria kwa abiria juu ya usalama wa ndege kwa maana ya mavazi *life jacket* na mambo mengine. Lakini sasa imekuwa ni mazoea unapanda ndege unaambiwa kwamba utaondoka hapa saa 3:00 na utafika Pemba saa 3:30, hakuna maelezo mengine yoyote kwamba wale abiria wanaelewa shughuli nzima za mavazi ya *life jacket* na usalama wa ndani ya ndege. Mhe. Spika, nadhani sheria ingesema kwamba ni jukumu la wenye ndege kwa maana ya wafanyakazi na marubani kutoa taaluma hii kisheria sio ni jambo la hiari kwamba ukitaka unatoa taaluma au ukitaka hutoe taaluma.

Mhe. Spika, msinikumbushe mwaka juzi tulipokuwa kwenye kamati mlango wa ndege ulifunguka tukiwa angani, wajumbe wako wanatoka Pemba kuja Unguja wamechukua mizigo yao mabegi na masusu ya pweza basi ndege ilifunguka mlango tukiwa angani. Kama kesi ile ingetokezea mswada huu haukusema nani alisababisha makosa yale hivyo tungetaka kujua sheria inasemaje. Kwa hivyo, usalama wa ndege ndani yandege ungezingatiwa sana kwenye msaada huu Mhe. Waziri angefikiria kwamba kuna haja ya kutolewa usalama wa ndege kwa abiria ndani ya ndege wenyewe. Kwa maana ya kwamba unaweza ukapokea watu pale lakini hawajui taratibu zozote na hakuna maelekezo yoyote na hatimae inasababisha athari ambazo ndege pamoja na abiria wenyewe wanaweza wakapata mazara makubwa. Mimi namuomba Mhe. Waziri hilo anielimishe na hasa suala zima la rubani wawili ndani ya ndege zetu, kuna umuhimu sana wa kuwa na rubani wawili kwenye ndege zetu hasa hizi ndege za hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono mswada huu.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia katika mswada huu wa Mhe. Waziri wa Mawasiliano, kwani mswada ni mzuri na una maelekezo mengi lakini hatuna budi na sisi kutoa yale ambayo tunahisi yanahitaji kutolewa.

Mhe. Spika, mimi nataka nizungumzie katika sehemu hii ya sita ambao usalama wa ndege pamoja na viwanja vya ndege. Mhe. Spika, kuna kitu pale ambacho chini yake kuna kamati ya usalama ya uwanja wa ndege, inaelezwa hapa kwamba kutakuwa na Kamati ya Usalama ya Uwanja wa Ndege ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao.

1. Meneja wa Uwanja wa Ndege - Mwenyekiti
2. Wajumbe wawili kutoka kitengo cha Usalama cha Uwanja wa Ndege
3. Wajumbe wawili kutoka jumuiya ya Watoa huduma za Uwanja wa Ndege.

Mhe. Spika, hapa mimi ninachotaka niongeze kwenye huu usalama wenyewe namuona hapa mtu wa kwanza amekuwa ni Meneja wa Uwanja, mara nyingi Meneja wa Uwanja anakuwa na mashirikiano na Mkurugenzi Mkuu, sasa hapa hakutiwa Mkurugenzi Mkuu lakini katika kuongeza kifungu cha tatu inasema.

“Bila ya kuathiri masharti ya kijifungu cha pili cha kifungu hiki Mkurugenzi Mkuu anaweza kutoa maelekezo ya jumla au maalum kwa kamati ya usalama kuhusiana na mambo yenye mamlaka hayo”.

Sasa yeye isiwe wa kutoa tu lakini huyo ajumuishwe kwa sababu hapa inaonyesha hawa wanafanya kazi pahala pamoja, Mkurugenzi na Meneja Mkuu wanafanya kazi pahala pamoja hatoweza kuchangia, si vizuri kwamba yeye atoe ushauri au maelekezo wakati yeye hayumo katika kamati hii. Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri kama itawezekana huyu Mkurugenzi awe ni mmoja katika hawa asiwe yeye ni mshauri kwenye kifungu cha pili tu.

Lakini la pili vile vile ambalo nataka nizungumzie katika huu usalama wa ndege mara nyingi labda watakuwa abiria wanaopanda katika ndege watakuwa labda hawawezi kujua ni mambo gani na mambo gani ambayo wanastahiki kuwa nayo, au mambo gani na gani hawastahiki kuwa nayo. Kwa mfano katika mikoba ya wanawake inawezekana mwanamke ametia vitu ndani ya mkoba wake ambao pengine hastahiki vitu vile kuwa navyo, sasa nafikiri hilo linajulikana na ni maarufu kabisa kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri katika masuala haya angeweza kutoa maelezo kinaga ubaga ili kwa raia wajue kwamba katika kupande ndani ya ndege kuna mambo fulani na fulani hutakiwi kuyachukua hata ukiwa nayo ndani ya mkoba wako.

Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa maelekezo yangu hayo kwa hivyo naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsanteni sana *(Makofi)*

Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa lakini nimesimama hapa kuunga mkono hoja na namshukuru Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kutuletea mswada huu katika wakati muafaka.

Kama Mhe. Waziri alivyotueleza wakati akifunga mjadala uliopita kwamba miswada hii itatoa matumaini kwa watu wanaotaka kuwekeza kwenye sekta hii kuja kuwekeza

katika nchi yetu, kwa sababu zile sheria ambazo walikuwa wanazisubiri tayari itakuwa sasa hivi zipo, kwa hivyo mimi sina mchango mkubwa isipokuwa niseme tu kwamba naunga mkono hoja.

Mhe. Waziri mwenyewe atakapokuja hapa atajibu hoja zake mimi wala sitaki kumsaidia Mhe. Waziri katika kujibu hoja, lakini Mhe. Spika, mimi kuna mambo ambayo nayashauri naona kama tayari hayajawachwa na mswada huu kwa mfano ukiangalia hii sehemu ya sita ya mswada kifungu cha 21 mpaka kifungu cha 28. Kwa ujumla vifungu hivi vinazungumzia usalama wa viwanja vya ndege usalama angani, usalama ndani ya ndege haidhuru utakuta havikutajwa vitu vyote vile kama vile simu havikutajwa wazi wazi. Lakini ukisoma kwa undani unaona vitu vyote hivyo vimo labda kwa mfano ukisoma katika kifungu cha 25 naona tayari hapa kimechanganya mambo mengi, ukiangalia 25(1) (d) kinasomeka kama ifuatavyo.

Kifungu 25(1) (d) kinasema "Kuwa na vitu vya hatari katika uwanja wa ndege, pia anasema kifaa chochote ambacho hakina sifa zilizoelezwa kwenye aya a, b, c au

Kifungu cha 25(d) "… (a), (b) au (c) na ambacho kimetengenezwa au kimeundwa kwa matumizi yanayoweza kusababisha madhara au kuumiza mtu, au kuharibu au kuangamiza mali au ambacho kimkusudiwa na mtu au aliyenacho kukitumia iwe yeye mwenyewe binafsi au vyovyote itakavyokuwa, na mtu mwengine atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kupewa adhabu ta kifungo kwa muda usiopungua miaka mitatu."

Halafu hii hii ukiangalia ya 26(d) yaani kuwa na silaha ya moto, mlipuko na kadhalika ndani ya ndege. Ukiangalia ile Mhe. Spika, ibara ya 26(d) inasomeka kama ifuatavyo:

Kifungu cha 26(d) "kifaa cha mlipuko au kitu chochote cha hatari au kifaa chengine cha aina yoyote ambacho kinachoweza kutumika kuhatarisha usalama wa ndege au wa watu, waliyomo kwenye ndege."

Nadhani inakidhi haja kwamba hata vile vitu ambavyo havikutajwa lakini vyengine vinaweza vikasababisha kuripuka na kuleta maafa, nadhani hapo ipo. Mambo mengine nadhani Mhe. Waziri tumuachie katika kanuni aendelee kuvifafanua vizuri zaidi katika kanuni. Lakini nadhani silaha Mheshimiwa ni nyingi na vitu vya hatari ni vingi. Sifikirii kwamba vyote ataweza kuvitaja katika sheria hii. Nafikiri Mhe. Waziri ni vyema tungemuachia mengine aeleze katika Kanuni, nafikiri yatajieleza vizuri zaidi kuliko kila kitu kukiweka katika sheria hii, nadhani sheria itakuwa kubwa sana.

Mhe. Spika, mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri na timu yake, katika hii Sehemu ya Tano ambayo ni Kodi na Malipo ya Uwanja wa Ndege. Muda mrefu waheshimiwa wawakilishi kwa muda wa miaka mingi tulikuwa tunalilia hii Idara sasa iwe ni Mamlaka. Kilio chetu hasa kutaka iwe Mamlaka kuona kwamba pale ile Mamlaka iwache ile tabia ya kila siku kwenda kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali kwenda kuomba pesa kama vile Idara ya Serikali. Lakini hilo wamelizidisha katika mswada huu.

Ukiangalia katika Sehemu ya Tano ya Mswada huu jambo hilo wamelizingatia sana. Kwa maana hata ile ada sasa kisheria itakuwa inagawanywa kwa sehemu zinazohusika na Mamlaka ya ukusanyaji pesa, lakini pamoja na wao watakuwa wana haki yao. Jambo jengine zaidi ambalo mimi limenivutia katika mswada huu ni kwamba wataanzisha mfuko wa maendeleo ya Uwanja wa Ndege. Kwa kweli hili ni jambo zuri sana. Kwa sababu hali tuliyonayosasa hivi hata wewe unahitaji kununua Vim kwenda kusafisha vyoo kwanza mpaka ukaombe pesa serikalini, ukanunue vim, ununue sabuni, ununue *toilet paper* uweke chooni. Sasa mambo kama haya yataondoka na mamlaka itakuwa na uwezo wa kuvitunza viwanja vyetu vya ndege na vikaonekana kwamba ni viwanja vya kimataifa.

Mheshimiwa haya ndiyo yalikuwa muda mrefu waheshimiwa tulikuwa tunayalilia na Mhe. Waziri na wenzake wameyaona. Mimi sina sababu kwa nini nisiunga mkono hoja katika suala hili. Jengine ambalo amenifurahisha Mhe. Waziri na watu wake ni katika hii sehemu ya nne ya Mswada. Inayozungumzia kutuwa na kuondoka kwa ndege. Hapa pameelezwa wazi wazi jinsi usalama utakavyokuwa katika maeneo haya ya uwanja wa ndege. Ni jambo moja zuri sana na nadhani hata wale wananchi waliokuwa na tabia ya kwenda kutanga tanga na kuzururazurura katika viwanja vya ndege na kuwatia hofu watalii na wageni wengine wanaoingia Zanzibar nadhani itapungua, nakushukuru sana juu ya jambo hilo.

Jengine zaidi hata hawa wenye ndege na wao, chini ya kifungu hiki sehemu hii ya nne na wao kwa upande wao watakuwa na nidhamu watakapoingia. Watakuwa wanajua kwamba hapa tunaingia katika Viwanja vya Ndege vilivyokuwepo kisheria kwa hivyo na wao watakuwa wanakwenda kwa mujibu wa sheria za ulimwengu zinazohusiana na usalama wa ndege.

Mhe. Spika, kwa mchango huu mdogo nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii angalau kuzungumzia machache tu katika Mswada huu. Mhe. Spika, kama walivyosema wenzangu kwamba huu ni Mswada muhimu ambao utasaidia sana katika kuimarisha viwanja vyetu vya ndege. Kwa hivyo ni wajibu wetu baada ya kujadili na kurekebisha mambo madogo madogo, tuukubali. Mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya jimbo langu la Mgogoni naukubali Mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, kuna mambo manne tu, ambayo napenda niyazungumze, lakini mawili kwa kweli ni kukubaliana na Mhe. Jussa alipozungumzia kuhusu kifungu cha 3 na kifungu cha 8. Kifungu cha 3 alipendekeza kusema kwamba katika uwanja wa ndege ni sehemu ya uwanja wa kutua na kurukia ndege. Hiyo nakubaliana na yeye. Halikadhalika katika kifungu cha nane pale aliposema kwamba ndege inayoondoka au inayowasili. Hayo nahisi Mhe. Spika, hayana matatizo.

Lakini katika kifungu cha 24(2) Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe alizungumzia na akasema kwamba mtu yeyote atakayefanya jambo lolote ambalo linaweza kupelekea hatari kwa ndege yoyote inayoelekea Zanzibar ikiwa angani atakuwa ametenda kosa na baada ya ndege kutua katika uwanjwa wa Ndege wa Zanzibar atalazimika kutua

atawajibika kushtakiwa kama vile kosa limetengeka katika uwanja wa ndege wa Zanzibar. Akajaribu kuuliza *rational* yake hasa katika kifungu hichi.

Mhe. Spika, katika masuala ya usafiri hasa ya ndege na ya meli, kunautaratibu wake, kuna *regulation* zake. Kwa masuala ya usafiri wa anga hasa tunatawaliwa na mambo mawili makubwa, *IATA* role na *ICAO* role, yaani *International Air Transporter Association* na *International Civil Aviation Organization*. Sasa hizi zina *role* maalum. Ili kwa kiwanja au kwa ndege kukamilika hasa katika utaratibu wa kimataifa ni lazima utaratibu huu ndio utekelezwe katika nchi husika.

Mhe. Spika, mimi nilifanya kazi katika Shirika la Ndege la Air Tanzania mwaka 1977, pengine Mhe. Ismail Jussa alikuwa bado yupo *Std II*. Wakati huo nilikuwa ni mshauri wa kisheria katika Shirika hilo. Mhe. Spika, utaratibu uliopo hasa kwa ndege na meli, kwa ndege kuna kitu kinachoitwa *Ilets flights* na kwa meli kuna kitu kinachoitwa *floating ilets*. Sasa *Ilets flights* ni ndege ambayo inachukua mambo mawili, inachukua *registration* ya pale ambapo imekuwa *registered*. Lakini pia kwa mujibu wa kanuni kule inakokwenda nako pia sheria zake itabidi ndege ile iheshimu.

Kwa hivyo, alipotoa mfano wa ndege ya Italy kwamba kule pengine sio kosa huku ni kosa, *simple rules za* sheria zinasema kwamba madhali umo katika nchi ya watu na wewe umo mule ni lazima uheshimu sheria za nchi ile. Hiyo ni ya kwanza. La pili ni kwamba pale ambapo umo ndani ya ndege ni kwamba *International Rules* za *ICAO* na *IATA* zinasema kwamba mtu ambaye atafanya kosa katika ndege ile basi ama atahukumiwa katika ile nchi ambayo ile ndege imekuwa *registered* au atahukumiwa katika ile nchi ambayo ndege ile itawasili.

Kwa hivyo kifungu hiki ni muhimu, kwa sababu ikiwa hatuna kifungu hiki yule mtu akifika pale hatuwezi kumstaki, itakuwa yule mtu atawachiliwa. Wakati mwengine zile ndege abiria anaweza akaleta matatizo ya hatari. Kwa hivyo ni lazima tuwe na kifungu ambacho kinaonesha kwamba mtu yule anaweza akashtakiwa pale. Kwa hivyo hii ni kulinda Zanzibar kwamba yule mtu tunaweza tukamshtaki bila ya yeye kushtaki sasa kwamba ameonewa bila ya sheria yoyote katika nchi.

Kwa maana hiyo Mhe. Spika, mimi naona kwamba kifungu hiki cha 24(2) ni muhimu kuwepo katika kuendeleza na kuimarisha kiwanda chetu. Sawa sawa kama alivyosema Mhe. Spika, na suala la meli ni hivyo hivyo. Meli ina sehemu mbili, pale ambapo meli imekuwa *registered* na pale ambapo meli inakwenda. Kwa hivyo wahalifu wote wanaweza wakashtakiwa huku au wanaweza wakashtakiwa kule.

Haina maana kwamba huku inapotoka ikiwa sheria ile haipo au ikiwa kosa lile si kosa, lakini kule unakokwenda ikiwa ni kosa lazima kwa mujibu wa taratibu uweze kushtakiwa kwa sheria za pale nchi ambapo ndege ile imefika. Suala la pili ni suala la *penalty* ambazo Mhe. Mjumbe amesema kwamba kuna sheria nyengine zinasema kwamba *penalty* zote ziwe sehemu moja na kuna sehemu nyengine anahisi kwamba kama katika sheria hii anasema kwamba kila pahala pameweka *penalty* yake.

Mhe. Spika, huu ni utaratibu wa *drafting* kuna mambo mengi ambayo yanatizamwa kabla ya kuandikwa sheria. Inaweza ikawa kuna sheria moja ambayo *penalty* zake zote unatakiwa uziweke mwisho kabisa, uziweke katika *section* moja tu ikiwa sheria ile inazungumzia tatizo moja tu. Lakini unapokuwa na sheria ambayo inazungumzia

mambo kadhaa, kwa hivyo kila jambo lile unaliwekea *penalty* yake na humu ndimo ilivyofanywa Sheria hii. Kwa sababu kuna makosa mengi katika sheria hii. Kuna kosa kwa mfano la kupita katika uwanja wa ndege. Kwa hivyo, pale ni lazima uweke *penalty* yake ili kuonesha kwamba yule mtu anayepita katika uwanja wa ndege basi atakuwa ni mkosa.

Lakini kuna kosa ambalo mtu wa kawaida au mfanyakazi amemzuia mtendaji kufanya shughuli zake, hilo ni kosa jengine. Kwa hivyo pale unapozungumzia yale ni lazima uweke *penalty* yake kuonesha kwamba ukifanya kosa hili basi utapata adhabu hii. Kwa hiyo katika *principle* za *drafting* ni utaratibu huu wa kawaida, inategemea sheria ile ambayo unaiandika inamaudhui gani, kama ni maudhui moja tu basi *penalty* zote unaziweka kumoja, lakini kama inamaudhui mengi basi unaziweka kwa mujibu wa utaratibu.

Mhe. Spika, ni sawa sawa tukalieleza Baraza lako katika sheria ya Adhabu, Katika sheria ya adhabu kila kosa lina adhabu yake, kila kosa linautaratibu wake. Huwezi ukasema kwamba adhabu zote uziweke pahala pamoja tu, haiwezekani. Inategemea hasa maudhui. Maudhui ya sheria hii Mhe. Spika, inamakosa mengi, ukifanya hivi itakuwa ni kosa, ukiuka hapa itakuwa ni kosa. Kwa hivyo ni lazima uoneshe kila sehemu na kosa lake. Pia na uandishi huu kwa hapa ni uandishi ulio sahihi. Katika *penalty* mimi nasema ni sawa sawa na kwamba imetizama ile maudhui ya sheria yenyewe ambayo ndio utaratibu hasa mzuri wa uandikaji wa sheria.

Baada ya hayo Mhe. Spika, nasema kwamba mimi nakubaliana na Mhe. Ismail Jussa kwa yale mawili lakini yale mawili sikubaliani nayo kwa utaratibu huu ambao nimeuelezea. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wafahamu utaratibu huu ambao ni mzuri na utasaidia katika kuimarisha sheria yetu ya viwanja vya ndege. Mhe. Spika, baada ya kwisha kusema hayo naomba tena nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuleta Mswada huu ambao ni muhimu na mimi naukubali asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru, maana kwenye kupata wanasema ama utapata kwa kununua ama kukodi au kurithi, lakini kupo kupata kwa heba yaani zawadi, sasa na mimi nashukuru kwa kunipa heba kwenye nafasi zako za kuchangia. Na mimi naomba niungane na wachangiaji waliotangulia kwanza kuishukuru tena sana Kamati kwa walivyoupitia Mswada huu kwa umakini. Niseme kwamba utatusaidia kutuongoza na sisi waandishi wa sheria tuwe makini zaidi. Kwa kweli naishukuru kwa dhati kabisa Kamati.

Pia nadhani baada ya muelezo wa Mhe. Waziri, nadhani mengi kayatolea ufafanuzi lakini labda niongeze mawili matatu. Kwenye hoja ya Mhe. Ismail Jussa naomba nimshukuru kwa dhati kabisa hasa pale alipotukumbusha kwamba tuwe makini. Tutakuwa makini haya ya viwanja, pengine ni *influence* ya Shirikisho au Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sasa nitawaambia wenzangu tusiigize sana Kiswahili cha wenzetu, tuigize Kiswahili cha kwetu ambacho ni fasaha kabisa.

Marekebisho aliyoyapendekeza Mhe. Jussa mengi ameyazungumza Mhe. Waziri, lile la kuruka na kutua nadhani ni sawa. Lakini kuna hili suala la adhabu ambalo anasema hakuna *consistency*. Mimi rai yangu kwa sababu sheria hii ina makosa katika vifungu mbali mbali, basi tukubaliane tu tuipitishe kama ilivyo baadaye tutaipitia kwa makini, tutaleta *miscellaneous amendments* ili tuyaweke sawa. Tukitaka kuyaweka sawa hii

leo tunaweza kuanza kuiandika tena upya. Kwa sababu makosa yenyewe sio makubwa sana ni ya utaratibu wa kuyapanga tu. Basi naahidi tutayaangalia na kwa sababu zipo sheria nyengine ambazo tunahitaji kuzifanyia mapitia baadaye tutatayarisha *miscellaneous* ya *amendments* tutaleta. Kuhusu suala la kifungu cha 24 Mhe. Waziri amelieleza vizuri sana na sina haja labda ya kurudia kwamba ni vizuri kuwa na kosa lile. Labda kumtoa wasi wasi tu Mhe. Jussa kwamba si kila kinachokuwemo kwenye sheria basi mtu atashtakiwa moja kwa moja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe mnaokwenda nje kwa dharura, muda wa kumwita Mhe. Waziri kufanya majuisho unakaribia, basi tuhakikishe tunarudi ukumbini si muda mkubwa kutoka sasa. Mhe. Mwanasheria Mkuu endelea.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Nilikuwa nasema kwamba lile la kushtakiwa si kila mtu anayefanya kosa anashtakiwa lakini kuna mambo mengi ambayo yanazingatiwa na lile jambo ambalo halina maslahi kumshtaki basi hilo hatoshtakiwa, haya si kila kosa. Hichi kifungu kime *qualify* kwamba ni yale makosa tu ambavyo yanahusiana na kuhatarisha usalama wa ndege. Sio kwamba kalewa pengine kwao si kosa akifika hapa atakuwa sahihi. Kama ni kulewa ambako kutasababisha hatari kwa ndege au kwa usalama wa ndege basi hilo ndio kosa ambalo linazungumzwa katika kifungu hichi.

Jengine nije kwenye ile hoja aliyoizungumza Mhe. Hija. Namshukuru kwanza kwa kututanabahisha. Lakini suala la kwamba sheria labda haizungumzii makosa mengine yanayohusiana na ndege hasa makosa ya ndani ya ndege. Labda nitanabahishe kwamba hii sheria ni ya viwanja vya ndege, yaani udhibiti na usimamizi wa viwanja vya ndege. Ndio maana utakuta mambo yaliyoelezwa ni kuhusiana na usalama wa kiwanja cha ndege chenyewe. Lakini kwa sababu kiwanja cha ndege kinatumika na ndege, kuna baadhi ya mambo ambayo yanahusiana na ndege ndio maana unayakuta kwenye hii sheria.

Lakini kwa sehemu kubwa ya masuala hayo ambayo anayazungumza Mhe. Hija sio kwamba hayamo kwenye sheria. Lakini kuna sheria ya *civil alleviation* na kanuni zake nyingi, mengi ambayo hayomo, takribani yote ambayo hayamo katika sheria hii basi utayakuta katika sheria ile. Ni sheria ambazo zinapaswa zitekelezwe na zisimamiwe.

Kwa hivyo naomba nimtoe wasi wasi kwamba sheria hii kwa ilivyo haipaswi kuzungumzia masuala hasa ya *aviation,* lakini inazungumzia suala linalohusiana na ndege pale tu kunapokuwa na uhusiano mkubwa baina ya ndege na matumizi ya uwanja wa ndege. Lakini zaidi imekusudiwa kuhakikisha usalama wa viwanja vye ndege, udhibiti wake, uendeshaji wake na utunzaji wake vile vile. Lakini na uendeshaji wake Air Port yenyewe kuhusiana na usalama ambao bila shaka utakuwa ni usalama wa ndege vile vile. Nadhani kwenye hili zipo sheria nyengine ambazo zinahusika na msuala yale ambayo yalikuwa yanampa wasi wasi Mhe. Hija.

Mhe. Suleiman yeye alizungumzia suala la *DG* au Mkurugenzi Mkuu chini ya kifungu cha 21 kwamba kwa nini asiwe mjumbe wa Kamati ya Usalama badala ya kuwa atoe maelekezo ya jumla. Mhe. Spika, Mkurugenzi Mkuu ni *over rolling charge* wa kusimamia viwanja vyote vya ndege kwa mujibu wa sheria hii. Yaani vile viliopo kwa viliopo sasa kwa mfano tulichonacho hapa Unguja, kilichopo Pemba, lakini na

chengine chochote ambacho kitaanzishwa hapo baadaye inawezekana kikawa cha binafsi.

Katika kila uwanja wa ndege kunakuwa na *Air port Manager* na watu wengine wanaohusika na usalama wa air port. Sasa wale kwa ujumla ndio wanaoshughulikia. Masuala ya usalama ni masuala ya kila siku, linaweza likajitokeza jambo la jumla linaweza likajitokeza jambo *specific*. Kwa hivyo ile Kamati moja katika kazi zake ni kuyasimamia yale. Hilo linaweza likajitokeza kwenye kiwanjia hikiyapa Unguja, linaweza likajitokeza kwenye kiwanja cha Pemba au chengine.

DG suala la kwanza litakuja akishakuwa yeye mjumbe Mwenyekiti wake awe *air port manage* ambaye ni mdogo wake. Hilo litaleta tatizo vile vile, bado *responsibility* ile ni ya *air port manage* kwa sababu *DG* tukitaka awe mjumbe itabidi awa mjumbe wa kamati ya hapa, aende akawe mjumbe wa Kamati ya Pemba, awe mjumbe pia wa kamati itakayoanzishwa pengine kwenye air port nyegine ambayo inaweza ikaanzishwa.

Kwa hivyo suala hilo ndio maana wameachiwa air port manage na watu wake. Lakini linaweza likajitokeza jambo ambalo hizi kamati haizajioni na yeye akataka zifanyiwe kazi. Au wameliona lakini wanavyoli- *handle* sio sawa sawa. Ndio maana sheria inampa uwezo kwamba anaweza akatoa maelekezo ya jumla kwa hivi kamati ili kusimamia kama yeye ndiye msimamizi wa jumla wa hizi air port katika masuala ya usalama. Hiyo ndiyo mantiki yake ya kuwepo kifungu hichi.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, mimi naunga mkono huu Mswada pamoja na marekebisho ambayo yamependekezwa na Kamati. Naomba wenzangu tuunge mkono ili tuwezeshe usimamizi wa viwanja vyetu vya ndege hasa wakati huu ambao tunaelekea kwenye wawekezaji binafsi katika masuala mbali mbali ya viwanja vya ndege ili yawe na udhibiti ambao ni mzuri na unajulikana, badala ya kuwa na mashirikiano na wawekezaji binafsi kwa kutumia mikataba. Ni vyema tuwe na sheria ambayo itaweka masharti na pia ile mikataba ita–*regulate* tu mahusiano baina ya serikali au baina ya mamlaka na wawekezaji. Lakini mambo mengi yatakuwa yameelezwa ndani ya sheria na yatakuwa yanamuongoza kila mtu katika hilo.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono Mswada. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundo Mbinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, sina budi na mimi kurejea tena shukurani kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu unaohusiana na Mswada huu kuhusu masuala ya Udhibiti na Uendeshaji wa Shughuli za Viwanja vya Ndege kwa Upende wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kuanza moja kwa moja na mimi nijaribu kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizoletwa. Mhe. Spika, Mhe. Rashid Seif Suleiman alitoa maoni yake yanayohusiana na vifaa na huduma za Air Port kwa maana kwamba alitoa mawazo yake hasa katika masuala ya matangazo na mengineyo.

Mhe. Spika, napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba mawazo yake yale tumeyapokea na naamini katika sheria tuliyoipitisha muda mfupi uliopita wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege suala lake hilo litafanyiwa kazi na hivi sasa tayari maboresho yameshaanza kuonekana katika Uwanja wetu Kimataifa. Mhe. Spika,

Mkurugenzi Mkuu tayari ameshaanza kuweka vifaa vya usalama zikiwemo *camera* za kunasia matukio na mambo mengine. Naamini mtiririko huo utaenda hata katika hivyo vipaza sauti na matangazo kadri hali inavyokwenda mbele ndivyo maboresho na huduma hizi zinazidi kuongezeka.

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba na Mhe. Mwanasheria Mkuu kuna baadhi ya vipengele ambavyo vilikuwa vinawapa hofu baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi ambao walihitaji kupata ufafanuzi. Mimi niseme kwamba naungana na ufafanuzi uliotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na ule wa Waziri wa Katiba na Sheria. Pia katika kumtoa hofu Mhe. Hija ni kwamba yale matumizi ya simu ndani ya ndege pamoja na sheria nyengine zinazohusiana na masuala ya *civilization*, lakini hata katika hii sheria yetu ukiangalia kifungu cha 24 kimeeleza kwamba utaratibu ule ni miongoni mwa yale mambo ambayo yatakuwa ni makosa kuyafanya, hivyo ukifanya utakuwa umeenda kinyume na taratibu na sheria za nchi, kama kuna Mamlaka ya kuweza kuchukua hatua kwa makosa kama hayo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Hija alikuwa na hofu juu ya utaratibu unaoendelea wa ndege zetu ndogo hizi zinaendeshwa na rubani mmoja akitaka kujua namna gani tunaweza kulidhibiti hili ni mtoe hofu Mhe. Hija kwamba jambo hili ni utaratibu wa kimataifa kwa mujibu wa sheria zinazoongoza masuala ya *civilization*. Mhe. Spika, ni kwamba kuna uzito maalum unazingatia ndege, chini ya uzito ule basi *pilot* mmoja anaruhusika kurusha ndege. Mhe. Spika, naamini ndege zile zinazorushwa na *pilot* mmoja zina-*full* katika eneo hilo.

Mhe. Spika, kwa kuendelea tena katika hili naomba niungane na Mwanasheria Mkuu kwa kuomba Baraza lako hili tukufu liupitishe mswada huu na kuona yale mapungufu yaliyosemwa hapa hasa katika maeneo ya adhabu na makosa kwamba tutawatafutia fursa kwa kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuja kuleta marekebisho hapo itakapobidi. Lakini kwa muda huu nadhani ni vyema na busara tukaweza kuupitisha mswada huu ili kuweza kupata mahitaji hayo tunayoyakusudia. Baada ya kusema hayo mimi binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Chwaka tunaunga mkono mswada huu mia kwa mia.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii siku ya leo mwezi 28 uwanja ni wangu na naamini kwamba yote tuliyoyapanga kufanya leo na kesho inawezekana kabisa kumalizika leo. Mhe. Spika, kwanza nataka niwashukuru wajumbe wote waliochangia na niende moja kwa moja kwa kuwataja, mswada huu ni mfupi sana lakini ni muhimu kweli kweli umechangiwa na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza lako tukufu. Aliyewakilisha kamati hii ni Mhe. Rashid Seif Suleiman lakini nae pia Mhe. Rashid amechangia kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka Jimbo la Ziwani.

Mwengine aliyechangia kwa kusema ni:-

1. Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe
2. Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani
3. Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde
4. Mhe. Haji Faki Shaali - Waziri Asiyekuwa na Kazi Maalum

5.	Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-	Waziri wa Sheria na Katiba
6.	Mhe. Othman Masoud Othman	-	Mwanasheria Mkuu wa Serikali
7.	Mhe. Issa Haji Gavu	-	Naibu Waziri wa Miundombinu Na Mawasiliano.

Mhe. Spika, na mchangiaji mwengine alikuwa ni Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi kwa maandishi.

Mhe. Spika, mimi nawashukuru wachangiaji wote kwa sababu wamemaliza kazi yangu ambayo nilikuwa nifanye hapa, na wamemaliza kwa sababu ni wajibu wao. Mwanasheria Mkuu amezungumza mambo ya kisheria, Waziri wa Katiba na Sheria na yeye vile vile na amefafanua zaidi mambo mengine ambayo hata sio ya kisheria. Vile vile Naibu Waziri wa wizara hii Mhe. Issa Haji Gavu amejitahidi kufafanua kwa yale ambayo waheshimiwa wawili walikuwa hawajamaliza.

Mhe. Spika, mimi niende haraka haraka katika masuala ambayo kwanza nakubaliana kabisa kwamba ambavyo imependekezwa kwamba kila mahali ambapo kuna ndege kuruka halafu hakuna kutua, basi yale maneno mawili yawe yanafuatana, ndege kutua au kuruka. Kwa sababu hiyo ndio itafanya huu mswada wetu kabisa uwe hauna kasoro ndogo ndogo.

Mhe. Spika, hiyo imeelezwa na wajumbe wengi akiwemo Mhe. Jussa, Mhe. Mwanajuma na waheshimiwa wengine. Lakini vile ile Mhe. Spika, Mhe. Haji Faki Shaali alizungumzia kuhusu mfuko wa maendeleo ya viwanja vya ndege. Hii tumesema tuiweke katika sheria kwa sababu mfuko huu ni kama fimbo ya kipembe, silaha zote zikimalizika basi unakwenda kipembeni unachukua fimbo yako, na hiyo ndio unamalizia kazi. Kwa hivyo, nashukuru kuwa wajumbe wameona kulikuwa na umuhimu kweli wa kuweka hilo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Haji amependekeza na ameshauri na shauri lake tunalichukua kwamba kanuni zitakazotengenezwa basi zihakikishe kwamba mapungufu madogo madogo kwa sababu sheria haitakuwa na kila kitu na ndio maana kukawa na kanuni kujaza nyama hii *skeleton* ya sheria. Kwa hivyo, hilo tunalichukua na tutalifanyia kazi.

Mhe. Spika, mwisho kabisa Mhe. Naibu Waziri alizungumzia hapa kuhusu suala la rubani mmoja, ni kwamba nilieleza katika mkutano huu huu wakati najibu swali kwamba miongoni mwa sababu za kwa nini ndege zinakwenda na rubani mmoja hasa hizi ndogo. Ni kwamba moja ilikuwa ni upungufu wenyewe wa watendaji hawa, lakini kwa kweli sababu za msingi hasa ukiachilia mbali ya rubani mmoja au kwa nini hawaendi wawili, ni kwamba sheria vile vile inawaruhusu na ninukuu kifungu cha sheria hiyo.

“All aircrafts with maximum take of weight of not more than 12,500 pounds can have one pilot”.

Kwa hivyo, hii *Costal, Aircraft, Zan Air* ndege kama hizi, hivyo msiwe na wasi wasi kwamba labda wale wanavunja sheria. Lakini nasema kwamba tungekuwa na *pilot* wa kutosha tungewashauri wakawa na pilot wawili ingawa kukitaka kutoa jambo hata mkiwa sita haisaidii kitu.

Mhe. Spika, halafu Kamati ya Usalama wajumbe wake ni kwamba hatukubuni lakini tumepata *annex* za kikao. Kuna vifungu vya sheria ambazo *air port* zote zinatakiwa zifuate kwa hivyo hata ile Kamati ya Usalama nayo imefuata sheria zile zile na masharti yale yale. Kwa hivyo, hawa hakuna cha siasa wala nini, ni watu ambao wanajuulikana kwamba lazima wawemo katika kamati ile.

Mhe. Spika, kama nilivyosema ni mswada mfupi kabisa lakini niende kwenye siasa kidogo "mngoja maiti hungoja akilia". Mhe. Spika, siku nyingi kwa sababu mswada huu ulikuwa haujajadiliwa wala haujaletwa suala la Pemba tulikuwa hatulitaji hasa linavyotaka kutajwa, lakini mtakumbuka kwamba suala la wawekezaji katika *air port* kama mnavyosema wako tayari na walikuwa wanaisubiri sheria hii ianzishwe.

Mhe. Spika, mimi kwa mawazo yangu na muono wangu ni kwamba mara baada ya sheria hizi kuwa tayari kutumika ile *contact* baina ya serikali na mwekezaji chini ya utaratibu wa *PPP (Public Private Partnership)* serikali itakuwa pamoja na Kampuni ya Kituruki na ni kampuni tatu kwa pamoja lakini zote ni za Kituruki, tutaingia kwenye makubaliano na katika makubaliano hayo ni kuvifanya viwanja vyetu vya ndege kuwa vizuri zaidi. Kwa hivyo, kutakuwa na uwekezaji kwenye Kiwanja cha Ndege cha Abeid Amani Karume lakini katika *funds* hizo zaidi ya asilimia 70 zitatumika kwa Kwanja cha Ndege cha Pemba.

Mhe. Spika, kilichopangwa kufanyika katika contact hiyo ni kukiendeleza kwa kuongeza urefu wa *run way* kwa mita 300. Kwa hivyo, uwanja wetu wa ndege wa Pemba utakuwa na urefu wa kilomita 1.9, sasa hivi una kilomita 1.5. Kwa hivyo, kiwanja hicho kitawezesha kabisa ndege kubwa *boing* 737 ya abiria 120 kutua pale, lakini sio hilo tu kiwanja hicho kitakuwa na uzio wa uhakika sio wa kubahatisha, sikwambii kupita mbwa lakini hata paka atakuwa hapiti. Vile vile tutajenga jengo jipya la abiria la kisasa na lile lililopo litafanyiwa matengenezo ya hali ya juu, lakini kama hivyo hakutoshi kutakuwa na taa zitakazosababisha uwanja ule kutua ndege masaa yote.

Kwa hivyo, matarajio yetu ni kwamba baada ya kupitisha miswada hii miwili na ndio leo mmoja tayari umeshapita *alhamdulilah rabilaa alamina* na huu wa sasa hivi karibu sana utapita. Kwa hivyo, *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na kwa baraka ya mwezi huu na siku ya leo siku ya viwanja vya ndege basi suala la uwanja wa ndege wa *air port* pengine Oktoba au kikao hicho kinachokuja itakuwa ni watu kupongeza.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri niwahoji sasa Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubali hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

(Hoja ilijadiliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

SEHEMU YA KWANZA - UTANGULIZI

Kifungu cha 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu cha 2 Ufafanuzi

SEHEMU YA PILI – KUANZISHWA NA USIMAMIZI WA VIWANJA VYA NDEGE

Kifungu cha 3 Kuanzishwa kwa Uwanja wa Ndege
Kifungu cha 4 Kamati ya Ufundi Pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 5 Masharti ya Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege
Kifungu cha 6 Maombi ya Kibali cha Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege
Kifungu cha 7 Kibali cha Kiwanja cha Helikopta
Kifungu cha 8 Udhibiti wa Afya katika Kiwanja cha Ndege

SEHEMU YA TATU – USIMAMIZI WA HATUA ZA USALAMA

Kifungu cha 9 Usimamizi wa Uwanja wa Ndege
Kifungu cha 10 Usalama wa Ndege na Marekebisho yake
Kifungu cha 11 Udhibiti wa Ardhi kwa Maslahi ya Anga
Kifungu cha 12 Haki ya Kuingia katika Ardhi
Kifungu cha 13 Kupita bila ya ruhusa katika Kiwanja cha Ndege na Marekebisho
yake

SEHEMU YA NNE – KUTUA NA KUONDOKA KWA NDEGE

Kifungu cha 14 Kutua kwa Ndege katika Kiwanja cha Ndege pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 15 Kinga Dhidi ya kuingia katika Kiwanja cha Ndege
Kifungu cha 16 Uwezo wa Ofisa katika Kiwanja cha Ndege
Kifungu cha 17 Ndege iliyotelekezwa

SEHEMU YA TANO – KODI NA MALIPO YA UWANJA WA NDEGE

Kifungu cha 18 Malipo ya Uwanja wa Ndege
Kifungu cha 19 Ada ya Kutua na Kuegesha
Kifungu cha 20 Mfuko wa Maendeleo wa Uwanja wa Ndege pamoja na Marekebisho yake

SEHEMU YA SITA – USALAMA WA NDEGE, VIWANJA VYA NDEGE NA UWEKAJI WA VIFAA VYA MAWASILIANO YA ANGA KUKINGA VITENDO VYA HATARI

Kifungu cha 21	Kamati ya Usalama ya Uwanja wa Ndege
Kifungu cha 22	Tangazo la eneo lisiloruhusiwa
Kifungu cha 23	Kuingia katika Uwanja wa Ndege na Marekebisho yake
Kifungu cha 24	Kuhatarisha Usalama wa Anga au Ndege
Kifungu cha 25	Kuwa na Vitu vya Hatari katika Uwanja wa Ndege
Kifungu cha 26	Kuwa na Silaha ya Moto, Mlipuko na kadhalika ndani ya Ndege Pamoja na Marekebisho yake
Kifungu cha 27	Kushindwa Kufuata Masharti ya Usalama
Kifungu cha 28	Kutupa taka ndani au karibu na Uwanja wa Ndege na Marekebisho yake

SEHEMU YA SABA – MASHARTI MBALI MBALI

Kifungu cha 29	Kosa kwa Taasisi
Kifungu cha 30	Uwezo wa Kutunga Kanuni
Kifungu cha 31	Sheria ya Kuwa na Nguvu na Marekebisho yake

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kufanya marekebisho sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

(Hoja ilijadiliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege ya 2011

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na taadhima naomba sasa Mswada wa Sheria Kuhusiana na Usimamizi wa Viwanja vya Ndege usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

(Hoja ilijadiliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulipitishwa na kukubaliwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa kunipa mashirikiano ya kuendesha shughuli zetu, tumeendesha shughuli vizuri nafikiri tulitoa demokrasia ya kutosha katika kuchangia, kupinga jambo ili kuomba ufafanuzi wa Mhe. Waziri ni jambo la kawaida katika vyombo hivi. Kwa kawaida ukitumia vipaza sauti hizi wakati mwengine mjumbe anaweza kuwa mkali kidogo, nayo ni masuala ya kawaida ukali ukizidi mno basi huwa anaombwa na kiti ashushe *pressure* kidogo ili aweze kujieleza vizuri, tumefanya hivyo na ndio hadi leo tunamaliza shughuli zetu hizi ambazo tumejipangia katika mkutano huu.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe mimi sina budi niwashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya na kazi hii nzuri imewezekana kwa sababu Makatibu wetu walikuwa makini wameifanya kazi nao naomba niwapongeze sana. Lakini nisiache kuwashukuru sana kabisa waandishi wa habari na hasa watu wetu wa TV. Kwa hivyo, kupitia Waziri wa Habari na Naibu wake nataka nichukue nafasi hii kuwapongeza sana ndugu zetu hawa ambao kwa muda wote wamekuwa wanarusha shughuli zetu na wananchi wanaziona moja kwa moja. Waheshimiwa Wajumbe pia hata wasikilizaji pale niwashukuru kwa sababu nao kwa muda wote walikuwa watulivu kusikiliza majadiliano haya na hiyo ilizidisha kufanikisha shughuli zetu vizuri. Waheshimiwa Wajumbe sasa tusitishe shughuli zetu ili kutoa nafasi kesho saa 3:00 kamili za asubuhi tarehe 31 tuje tumsikilize Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

(Saa 7:45 mchana Baraza liliakhirishwa hadi kesho tarehe 31/07/2011 saa 3:00 asubuhi)